ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.

12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Pili – Tarehe 12 Disemba, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hotuba ya uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara, sura 134 na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Panya Ali Abdalla (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani hati ya muhtasari ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Amri ya Barabara Sura ya 134. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuendelea na maswali, pale ukumbi wa juu kuna wageni mbali mbali ambao kama kawaida huwa wanaomba kuja kuona shughuli za vikao vyetu vya Baraza.

Kwa leo wageni wetu ambao wapo pale juu ni wanafunzi wa mwaka wa tatu wa sheria kutoka Chuo Kikuu cha Zanzibar Tunguu, jumla yao ni 56 na msafara huo unaongozwa na Mbunge, kumbe na wao wanalo bunge hawa. Kwa hivyo, Mbunge wa darasa hilo ambaye ni Mhe. Masoud Salum Moh'd, maana mtu anayechaguliwa na watu lazima apewe heshima maalum, pamoja na Waziri wa Sheria na Katiba wa chuo hicho ndugu Juma Muhaya. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kwa ujumla wanachuo pamoja na wakuu hao wa msafara huo karibuni sana katika shughuli zetu za vikao vya Baraza la Wawakilishi, leo ni kikao cha pili tunaendelea na shughuli zetu na nyinyi mutajionea Mhe. Mbunge yule pamoja na Waziri wa Katiba wa Chuo. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa kweli makofi yote hayo ni ya kwenu kwa ajili ya kukaribishwa katika ukumbi huu.

Vile vile, nimemuona Mhe. Waziri wa Katiba anasema hivi sasa kuna nani ambaye anafanya mapinduzi. Kwa hiyo, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria wewe ni wa serikali na yule ni wa chuo. Wanafunzi karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na maswali.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 6

Uhakiki wa Daftari la Wapiga Kura

Salim Abdalla Hamad (Kny: Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Kwa kuwa katika mwezi wa June, 2013, Zanzibar tumefanya chaguzi mbili ndogo katika kisiwa cha Pemba kwa maana ya Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Chambani na ule wa Wadi ya Udiwani wa Ng'ombeni katika Wilaya ya Mkoani. Vile vile, kwa kuwa katika kipindi kirefu Daftari la Kudumu la Wapiga Kura bado halijafanyiwa uhakiki kwa kuingizwa wapiga kura wale waliotimiza sifa za kuwa wapiga kura, sambamba na kuwaondosha wale wote waliopoteza sifa.

(a) Je, kufanya uchaguzi katika sehemu hizo bila Uhakiki wa Daftari si kurudisha nyuma Demokrasia.

(b) Je, ni mara ngapi daftari hilo limefunguliwa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo tangu kumalizika uchaguzi mkuu wa mwaka 2010 hadi leo hii.

(c) Ni kwa kiasi gani Wadau wa Uchaguzi wa Zanzibar walishirikishwa katika zoezi hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, na mimi kabla ya kujibu swali niungane na wewe kuwapongeza vijana wetu waliokuja kututembelea na niwatakie heri na mafanikio makubwa. Aidha naomba nimtanabahishe Mhe. Abubakar Khamis Bakary Waziri wa Katiba na Sheria kwamba watu wanamtambalia na wameshafika Barazani. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 6 lenye vifungu (a), (b), na (c) naomba nitangulize maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, ni kweli kabisa kuwa katika mwezi wa Juni 2013 zilifanyika chaguzi ndogo mbili katika Wilaya ya Mkoani, Pemba ambazo ni Uchaguzi Mdogo wa Jimbo la Chambani ulioendeshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*) kujaza kiti cha Mbunge wa Jimbo hilo na baadae ukafanyika Uchaguzi Mdogo wa Wadi ya Ng'ombeni uliondeshwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (*ZEC*) kujaza nafasi ya Diwani wa Wadi hiyo.

Mhe. Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza wananchi wote waliojitokeza kuitumia haki yao ya kidemokrasia ya kumchagua kiongozi wanaemtaka katika eneo lao. Aidha, nawapongeza pia viongozi waliopata ushindi katika chaguzi hizo zilizoendeshwa kwa uwazi na haki bila ya kutokea malalamiko yoyote.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swala lake Nam. 6 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kufanyika kwa Chaguzi Ndogo hizo ni kukuza demokrasia na si kurudisha nyuma demokrasia, kwani Mbunge wa Jimbo la Chambani na Diwani wa Wadi ya Ng'ombeni walichaguliwa kwa njia ya kuwashirikisha wapiga kura walioandikishwa kisheria katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura la maeneo husika.

b) Mhe. Spika, kazi za uandikishaji wa wapiga kura wapya na uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura zimeanza rasmi tarehe 29 Juni 2013. Kazi hizi zinafanyika kwa mara ya kwanza tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Kabla ya hapo, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limetumika mara nne kwa ajili ya kuendesha chaguzi ndogo zilizojitokeza mwaka 2011, 2012 na 2013.

c) Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kabla ya kuanza rasmi kwa kazi za uandikishaji wa wapiga kura wapya na uendelezaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, iliendesha semina mbali mbali za wadau wa uchaguzi ikiwemo Semina moja kwa Viongozi wa Vyama vya Siasa Kitaifa iliyofanyika katika hoteli ya Bwawani tarehe 21 Mei, 2013. Semina hiyo baadaye ilifuatiwa na semina pamoja na mikutano ya Wadau wa Uchaguzi kwa Mikoa na Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza natoa pongezi kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri. Lakini hata hivyo, nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa sababu ni haki ya kila mzanzibari aliyetimiza umri wa miaka 18 kupiga kura katika uchaguzi mkuu na ikiwa masharti yaliomo kwenye kifungu cha 7 cha Katiba ya Zanzibar Sehemu Ndogo ya Pili, masharti ambayo yatamkosesha kupiga kura hayamuhusu. Vile vile, katika nchi hii kuna watu wengi tu walipiga kura katika chaguzi zilizopita, lakini kwa sababu ya kutokuwa na vyeti vya kuzaliwa hawapigi tena.

Pia, katika zoezi la juzi lililoendelea la uandikishaji wa watu wapya na kuondoa wale ambao hawamo tena, pia ilijitokeza kwa sababu ya utashi wa masheha wengi wakakosa haki yao. Je, Mhe. Waziri, kwa sababu kumkosesha mzanzibari kupiga kura ni kumuondolea haki yake na kinyume na demokrasia.

Mhe. Waziri, haoni kuwa ipo haja hivi sasa ya kuona yale yote ambayo si ya lazima kubakia katika kumkosesha mtu haki yake ya kupiga kura yanaondolewa na tufuate Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano, ambayo vipengele hivi havichukuliwi na huku ni lazima uwe na cheti cha kuzaliwa na mtu anaonekana umri wake na wengi wanavyo vitambulisho wakati wazanzibari wenye sifa kama hizo wanavyo vitambulisho vya Tanzania Bara, lakini hapa hakuna.

Kwa hivyo, haoni Mhe. Waziri, kwamba ipo haja ya kufanya hivyo na hasa kwa sababu Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar haishauriwi na kitu chochote isipokuwa inakwenda sambamba na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kuhusu kuifanyia marekebisho sheria ya Uchaguzi. Hivi sasa Mhe. Spika, kazi hiyo inafanywa na Tume ya Uchaguzi, ili pale ambapo kuna mapungufu ya aina yoyote, basi mapungufu hayo yatarekebishwa.Vile vile, tayari tumeshafanya makongamano mbali mbali pamoja na semina kwa kuwashirikisha wadau kwa ajili ya kupata maoni yao.

Mhe. Spika, naomba niseme tu kwamba idadi ya walioandikishwa kuwa wapiga kura Zanzibar kiasilimia tukilinganisha na ile idadi ya watu ni ya zaidi ya asilimia 60. Kwa hivyo, Mhe. Spika hii inaonesha wazi kwamba wale wapiga kura waliopo na wanaotimiza vigezo wanaandikishwa bila ya matatizo.

Katika mwaka huu wa 2013 tulitarajia kwa mujibu wa idadi ya watu, basi watu wote wanaopaswa kupiga kura wawe ni 695,715. Watu ambao waliandikishwa huko nyuma walikuwa ni 407,698. Vile vile, hivi juzi wakati tukifanya zoezi la kupitia Daftari la Kudumu waliongezeka watu 41,261.

Mhe. Spika, ukitizama idadi ya *estimation* ya *population* kama nilivyosema kwamba 625,713 na watu wenye *Zan ID* watu 600,000 wazanzibari wanazo *Zan ID*. Kwa hivyo, ukitizama hasa tofauti Mhe. Spika ni watu 25000 tu. Sasa ikiwa watu 600,000 wanazo *Zan ID*, tulitarajia kwa sababu tunayo idadi ya walioandikishwa watu 400,000, basi tulitarajia mara hii wajitokeze watu 100,000.

Lakini waliojitokeza ni watu 41,261 na wala hakuna mzanzibari yeyote ambaye ametimiza sifa na akawa na *Zan ID* yake akenda pale kutaka kujiandikisha kama mpiga kura akakataliwa na kama yupo, basi tuletewe orodha hiyo ama wapelekewe Wakuu wa Wilaya na tuletewe tuone kama yupo anayekataliwa mtu ambaye anatimiza masharti ya kupiga kura. Sasa kama kuna mapungufu yoyote basi ni Baraza hili Mhe. Spika, ndio linalotunga sheria na tutaileta sheria ili tuone, basi hayo mapungufu yaliomo ndani ya sheria.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie wananchi wa Zanzibar wote, kwamba wale ambao wenye haki ya kupiga kura, basi tume yetu haina kitu cha kumzuia. Lakini Mhe. Spika, jambo la kustaajabisha kwamba sisi idadi hii inayoonekana ndogo ya uandikishaji, lakini wakati wa Kura ya Maoni idadi ilikuwa ni ndogo zaidi na waliopiga kura walikuwa ni watu 206339 na wala hakukutokea manung'uniko yoyote ya idadi.

Kwa hiyo, jambo la kustaajabisha ni kwamba wakati mwengine tusichanganye na mambo ya jazba za siasa katika uandikishaji. Jambo la msingi hapa kama kuna mapungufu basi tuelezane mapungufu yenyewe, ili nchi ibakie ya umoja, amani na utulivu na kila haki ipatikane. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante na kabla sijauliza swali dogo la nyongeza naomba angalau unipe sekunde 30 kwa ajili ya kutoa neno la shukurani kidogo kwa wananchi wa Jimbo la Kwahani.

Mhe. Spika, jana katika kuadhimisha Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Mzanzibari yalifanyika Mashindano ya Nage katika Uwanja wa Kisonge na kwa bahati nzuri Jimbo la Kwahani limeweza kuingia nusu fainali kwa kuwafunga ndugu zao wa Jimbo la Kwamtipura kwa magoli 76 kwa 34. Kwa hivyo, naomba niwapongeze vijana wa Jimbo la Kwahani kwa ushindi mzuri

na ninawatakia mafanikio mema katika nusu fainali itakayofanyika na Jimbo la Kikwajuni. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba uniruhusu niulize swali la nyongeza ambalo ni dogo sana. Ili uwe mpiga kura halali kuna vitu unastahiki uwe navyo nacho ni kitambulisho cha kupigia kura, ili upate kitambulisho cha kupigia kura kuna vitu unahitajika uwe navyo (sifa za kuwa mpiga kura) moja wapo ni sifa ya kuwa ni Mzanzibari. Vile vile, ili uwe Mzanzibari kuna vitu au sifa ambazo unahitaji uwe nazo na sifa moja ya kuwa Mzanzibari suala la kuzaliwa, yaani uwe na *birth certifícate* ya Zanzibar.

Sasa hivi karibuni tu kupitia vyombo vya habari tumepata kusikia kwamba kuna vyeti vya kuzaliwa vilivyoghushiwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, sijui kama hili amelisikia au hajalisikia na kama amelisikia Mhe. Waziri, basi nataka kujua wizara yake imelikabili vipi suala hili, kwa ajili ya kuepusha kutoa fursa ya watu ambao wenye vyeti vilivyoghushiwa kuja kupata haki ambayo si yao. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze kwa kuwafunga magoli mengi wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, maana ukifunga ile unawafunga wote, Hivyo, hongera sana na Mhe. Hamza Hassan Juma atakusikia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, serikali imepata taarifa kwamba kuna baadhi ya watu wanaoghushi vyeti vya kuzaliwa na hivi sasa tumo katika zoezi kubwa kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kuwatafuta wale wote ambao wanaghushi vyeti na hatua hizo zimeanza kutoka kwa wizara husika.

Kwa upande wetu sisi kama Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, basi tumewataka ndugu zetu wa Jeshi la Polisi kuiharakisha kazi hii haraka sana, ili wale wote wenye vyeti vya kughushi hatua za kisheria zichukue mkondo wake na kama itakuwa wamefanya mbinu yoyote ya kupata haki yoyote kwa vyeti hivyo vya kughushi, basi haki hiyo itakuwa batili na utaratibu wa kisheria utachukua nafasi yake.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye sehemu (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, katika uandikishaji wa wapiga kura wapya uliomaliza hivi karibuni tulipata tetesi au taarifa kwamba uandikishaji wa wapiga kura katika majimbo matano, kwamba uandikishaji wake kumbukumbu zake zimeharibika.

(a) Mhe. Waziri, anaweza kulihakikishia vipi Baraza hili pamoja na wananchi juu ya sababu zilizopelekea kumbukumbu hizo kuharibika au kupotea.

(b) Ikiwa hilo lilitokea sasa serikali inatuhakikishia vipi kwa sababu uchaguzi ni suala nyeti na ikiwa Tume ya Uchaguzi imepoteza kumbukumbu, hivi serikali inatuhakikishia vipi wananchi kwamba tuwe na imani kuwa Tume ya Uchaguzi itaendelea kutunza kumbukumbu za wapiga kura ambazo zimetumika fedha nyingi sana kwa ajili ya kuzitayarisha.

(c) Kwa wale katika marudio kuna watu ambao hawakujitokeza kwa mara ya pili kwenda kuandikisha na kwa kuwa wale walikuwa tayari wameshaandikishwa. Je, serikali au Tume ya Uchaguzi inaweka utaratibu gani kwa wale ambao tayari wameshaandikisha, ili watakapopata nafasi waende wakajiandikishe kama ambavyo walijiandikisha katika uchaguzi wa huo wa marudio.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nataka nimuhakikishie kwamba Tume yetu ya Uchaguzi ya Zanzibar iko makini na inafanya kazi kwa kufuata sheria iliyotungwa na Baraza hili tukufu na siku zote itaendesha chaguzi kwa dhamira moja tu, ambao ni uchaguzi huru na wa haki na kila mwananchi apate haki yake.

Mhe. Spika, yanapotokezea matatizo yoyote katika shughuli za uandikishaji au shughuli nyengine zozote zile basi matatizo hayo hurekebishwa kwa nia njema kabisa, kwa sababu sisi kama binadamu hakuna mwanadamu ambaye ni mkamilivu. Kwa hivyo, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi, kwamba yanapotokea matatizo, hatua huchukuliwa kurekebishwa matatizo hayo, ili kuhakikisha kwamba Daftari letu la Kudumu la Wapiga Kura linakuwa safi hivi sasa na linatoa haki kwa Wazanzibari wote wanaopaswa kupiga kura na tutaendelea kufanya hivyo.

Vile vile, kwa wale wote ambao kwa namna moja au nyengine walipata matatizo katika uandikishaji, basi tunawahakikishia kwamba sasa hatua za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura umeanza na wala hii haitokuwa ni mara ya kwanza, isipokuwa tumeanza na tutaendelea kufanya hivyo. Mhe. Spika, na pale ambapo kuna tatizo na mtu yeyote anaona anakosa haki yake basi kupitia Ofisi za Tume za Uchaguzi zilizoko katika Wilaya zetu anayo haki hiyo ya kupeleka malalamiko hayo, ili marekebisho yafanyike.

Mhe. Spika, nataka niwahakikishie kwamba wale wote ambao wenye matatizo aina moja au nyengine, basi tutachukua kila hatua kuhakikisha

kwamba kila jambo tunarekebisha na daftari letu liwe safi, liwe sahihi na liwe tayari kwa ajili ya kupiga kura wakati ukifika wa kupiga kura.

Kwa hivyo, tutafanya shughuli hiyo ya kufanya tena maboresho katika Daftari letu la Kudumu la Wapiga Kura kabla ya Uchaguzi Mkuu, ili tuhakikishe kwamba tunapoingia katika Uchaguzi Mkuu basi mambo yako sawa na sahihi na wala hakuna dosari yoyote.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nilimuomba Mhe. Waziri anieleze sababu zilizopelekea hayo matatizo kutokea naona hajajibu mpaka hivi sasa, kwamba tulihitaji sababu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, hapa sina sababu zilizotokea wakati uandikishaji unaendelea. Kwa hivyo, hili naomba nilichukue na tutamjibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Nam. 23

Ukosefu wa Vifaa vya Uchunguzi katika Hospitali ya Jimbo la Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 23 naomba kutoa maelezo yafuatayo. Kwa kweli chombo hichi ni cha wananchi na tumekuja kufanya kazi za wananchi na wala si cha Mhe. Issa Haji Ussi, wa Jimbo la Chwaka wala Mhe. Hija Hassan Hija, isipokuwa hapa tumekuja kufanya kazi za wananchi.

Kwa hivyo, kwa masikitiko makubwa sana jana katika swali la msingi ambalo ni la jamii kuhusu paa la Hospitali Kuu linavuja na Mhe. Naibu Waziri alikataa kulijibu swali lile na kwa utaratibu wetu Mhe. Spika, wewe ndiye mwenye haki ya kukataa swali na hili ni la jamii, wananchi wanateseka wanaroa. Sasa tukiachia hali kama hii Mhe. Spika, Waswahili wanasema “huruma hailei mwana”.

Jambo la tatu Mhe. Spika, kabla kujibu Waheshimiwa Mawaziri au Manaibu Waziri, kwenda kutembelea lile eneo, maana yake unakuja kujibiwa swali ambalo halina kichwa wala miguu kwa masikitiko makubwa nadhani wangefuata nyayo za Naibu Waziri wa Elimu Mhe. Zahra Ali Hamad, jana amekwenda Muyuni kwa ajili ya kwenda kuangalia Skuli, kwa sababu kile

kitu anachokijibu anauhakika nacho, lakini tukiendelea hivi kuja kujibu wanachotaka hatuwafanyii haki wananchi.

Kwa mfano mimi ninahangaika mvua na jua kuyaleta maswali ya jamii, lakini ikifika hali kama hii mtu kuja kujibu na wala hatuwezi kufanyakazi namna hii. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Spika, naomba nijibiwe swali langu Nam. 23.

Hospitali za Jimbo la Muyuni ikiwemo ya Kitogani na Muyuni zinakabiliwa na ukosefu wa vifaa muhimu vya uchunguzi vikiwemo BP – Mashine pamoja na kifaa cha kuchunguza wingi wa damu mwilini.

(a) Sababu gani za msingi zinapelekea vifaa hivyo kukosekana na kuathiri upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

(b) Kwa nini Wizara ya Afya haina utamaduni wa kuweka vifaa vya akiba hasa kwa kuzingatia wananchi wengi ni wanyonge na kimbilio lao kubwa ni hospitali za umma.

(c) Gharama ya vifaa hivyo ni kiasi gani hadi wananchi wakose huduma yake.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nafikiri kuhusiana na suala la paa utatafuta utaratibu wa kuuliza swali la msingi Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Mashauri hayo kwamba kama kuna swali ambalo limeulizwa na linahusu eneo fulani, nimeshauri kwamba ni vizuri basi wanaohusika mawaziri wakaangalie, ili kujua hali halisi mambo yako vipi. Kwa kweli hilo ni shauri zuri nafikiri mawaziri wanaweza kuchukua jambo hilo na mawaziri watajiweka vizuri kuhusu jambo wanalojibu liko kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, kumekuwa na *experience* huko nyuma ambazo zimejitokeza, Waziri alikuwa anajibu swali wakati sivyo ilivyo kwenye *field*, sasa ni vizuri wakati mwengine kwenda kuangalia na kuweza kuona hali halisi iko vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, sababu zinazofanya baadhi ya vituo vya afya kukosa vifaa kama BP- mashine na vya kupimia kipimo cha wingi wa damu ni kuharibika kwa vifa hivyo, kwani baadhi ya vituo vina matumizi makubwa na idadi iliyokadiriwa ikifika vinaacha kufanya kazi kama vilivyo vifaa vyote vya kieletroniki vya kisasa.

Manunuzi ya vifaa vya hospitali wizarani ni ya jumla na taratibu zote za manunuzi ni lazima zifuatwe. Lakini timu za Utawala ya Afya za Wilaya (*District Health Management Team*) huwa wanayo bajeti yao ya kila robo mwaka ambayo ni ya uhakika na wanatumia kwa mujibu wa vipaumbele vyao. Kwa mfano wakiamua kununua vifaa hivyo kwenye kituo husika wanaweza kufanya hivyo badala ya kusubiri mgao wa jumla.

Njia nyengine inayotumika Mwakilishi anayejua nini mahitaji ya vifaa vilivyo katika jimbo lake na kuomba ruhusa Wizarani ili apewe idhini ya kufanya manunuzi hayo. Mfano Mwakilishi wa Jimbo la Uzini keshafanya hivyo mara mbili.

a) Wizara ya Afya haina utamaduni wa kuweka vifaa vya hakiba hasa kwa kuzingatia idadi ya vituo ni kubwa na mahitaji ya vifaa vyengine pia yapo na bajeti yenyewe ni ile iliyopo kwenye makadirio na matumizi ya mapato ya serikali ya mwaka ambayo ninajua kwamba haipo.

b) Gharama za vifaa hivyo ni kama ifuatavyo:

BP machine	shs. 95,000
Mashine ya Kupimia wingi wa damu	shs. 350,000
na *sticks* zake kiboksi kimoja	shs. 200,000

Wizara itashindwa kukubaliana na mapendekezo ya Mwakilishi ya ununuaji wa vifaa reja reja kwa kila kituo kwa sababu utaratibu wa manunuzi Wizarani haupo hivyo. Ila Mwakilishi kama anaweza kufanya hivyo kwa vituo vyake vitano vya Jimbo la Muyuni ambapo itamgharimu BP mashine kwa shilingi 275,000 na 1,750 kwa ajili ya mashine ya kupimia wingi wa damu na milioni moja kwa *stick* ya kuanzia na baadae kununua tena kila zinapohitajika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kusikitisha na kukatisha tamaa ya Wizara ya Afya, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa nini kituo kile kisifungwe hivi sasa kutokana na Wizara kushindwa kutekeleza kununua vitu hivyo muhimu, hii ni sawa na hadithi ya kuwa na sanduku ukalitia chumbani wakati halina nguo.

b) Kwa kuwa matibabu ni haki ya kikatiba kwa kila Mzanzibari, je, Wizara inawaambia nini wananchi wanaohangaika kupata matibabu hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, hatufungi kituo kwa kukosa kifaa hicho, hatujawahi kufanya hivyo wala hatutofanya. Wilaya itashauriwa wanunue kifaa hicho ili kazi ziendelee. Ingawa kununua wao ni jukumu lao na wakiona kwamba kwao ni kipaumbele. Lakini hata hivyo, tutawashauri wafanye hivyo ili shughuli zinazotaka kufanyika zifanyike. Na kweli matibabu ni haki ya kila mwananchi kikatiba na kisheria na ndicho kinachotendeka. Kukosekana kwa BP machine hakujawakosesha watu kutopata matibabu.

Hicho ni kipimo ambacho wanapimiwa wajawazito ambao si wagonjwa isipokuwa wanakuja kwa vipimo vya kawaida. Bahati nzuri Wilaya ya Kusini vituo vipo karibu. Mtu wa Muyuni anaweza kufika Kibuteni anaweza akafika Kizimkazi Dimbani, anaweza akafika Muungoni. Kama ni BP machine hakuna Muyuni basi vituo hivyo vyengine vinaweza vikamsaidia kufanya hiyo shughuli.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru sana kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri, swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, kama ambavyo Mhe. Jaku Hashim Ayoub, amenukuu Katiba kwamba matibabu ni haki ya msingi ya binaadamu sio tu Mzanzibari na Wizara hii ndio iliyobeba jukumu la kuwahudumia kiafya na kimatibabu Wazanzibari wote na Baraza hili Mhe. Spika, ndio ambalo hupitisha bajeti ya Wizara kwa ajili ya matumizi ya vituo vyote vya Unguja na Pemba. Ningetegemea Mhe. Naibu Waziri, atwambie sababu zipi za msingi ambazo wameshindwa kununua vifaa hivi katika hospitali hiyo badala ya kuwataka Wawakilishi wanunue kama kwamba ndio wenye jukumu la kuhudumia vifaa vya hospitali.

(a) Je, Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri, anakusudia kunambia kwamba Wizara yake imeshindwa kuhudumia wananchi wa Muyuni.

(b) Zamani kulikuwa na utaratibu wa *pushing system* na tukakubaliana kwamba sasa kuwe na *pulling system*, je, Mhe. Naibu Waziri, utaratibu ule sasa ukoje.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, napenda nirejee kusema tena wanayoyasema ni ya kweli kwamba matibabu ni haki ya kikatiba. Katika jumla ya matibabu vifaa vinahitajika kuwepo, vifaa vinakuwepo kila mwaka

vinanunuliwa katika bajeti zinazokuwepo, mwaka huu bajeti ya vifaa ipo, lakini kuna taratibu zinahitaji kufatwa. Kuna *tender process* ipite kutafuta wazabuni, mpaka ifikie kipindi cha kuweza kununua vifaa, hilo si jambo la siku moja wala si jambo la mwezi mmoja.

Kwa hivyo, itapofika wakati kama kitu kitakamilika vifaa vitanunuliwa na vitagawanywa katika vituo. Sikuwaambia Wawakilishi wanunue, mimi nimesema mfano Wawakilishi wanapoona matatizo kwenye vituo vyao wako ambao wananunua na nikasema Mhe. Mwakilishi wa Uzini ameshanunua si mara moja, mara mbili na yeye pia anajua kwamba Wizara ina jukumu hilo. Lakini kwa kuona kwamba wananchi wake wanapata shida akafanya hivyo, sasa kama wengine hawataki siwalazimishi kufanya, Wizara tutafanya maana ndio jukumu letu.

La pili, utaratibu wa *push* na utaratibu wa *pull* huo ndio utaratibu umeshakamilika ulikuwa umeanza kwa baadhi ya vituo na sasa hivi wameshafikia asilimia moja. Safari hii pesa zikikamilika vikinunuliwa vifaa na dawa zitanunuliwa kwa mujibu wa matakwa ya vituo husika.

Nam. 29

Uingizwaji wa Mafuta ya Kula Chini ya Kiwango

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Takwimu za kibiashara Tanzania Bara zimeonyesha wafanyabiashara wamekuwa wakiingiza zaidi mafuta ya kupikia aina mbali mbali yakiwemo mafuta ya chikichi sambamba na kutokea malalamiko juu ya ubora wa mafuta hayo kwa afya za wananchi.

a) Kwa Zanzibar takwimu za uingizaji zikoje.

b) Ni aina gani ya mafuta hapa Zanzibar serikali imeyagundua kuwa ni salama zaidi kwa matumizi ya chakula.

c) Je, ni kwa nini serikali haiwahamasishi wananchi kulima kilimo cha Mchikichi kwa lengo la kuongeza pato la Taifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 29 lenye kifungu (a), (b), (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, takwimu za uagiziaji wa mafuta ya kupikia nchini kuanzia Januari mpaka Septemba ilikuwa ni lita 11,824 na mafuta hayo Mhe. Spika, yanatumika Zanzibar, lakini mengine hupelekwa katika soko la Tanzania Bara.

b) Aina ya Mafuta ya Kula Mhe. Spika, yanayoingizwa Zanzibar ni kama hivi ifuatavyo:-

- Sunflower Oil
- Palm Oil
- Coconut Oil
- Corn Oil
- Cotton Oil
- Olive Oil
- Peanut Oil
- Cashewnut Oil
- Premium
- Oky Oil

Aina zote hizo Mhe. Spika, zinazoingizwa hapa Zanzibar kwanza hufanyiwa uchunguzi na Bodi ya vyakula, dawa na vipodozi iliyo chini ya Wizara ya Afya na baadae yakithibitika kwamba ni salama kwa matumizi ya binaadamu basi huruhusiwa kuingizwa madukani.

c) Mhe. Spika, kuhusu ulimaji wa Kilimo cha Michikichi, hili ni shauri zuri, lakini kwa kuwa masuala ya Kilimo yako chini ya Wizara ya Kilimo, basi nimwambie Mhe. Mwakilishi, kuwa tunalichukua suala hili na tutakaa na Wizara husika tuone kama kilimo hiki kitasaidia katika uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Jaku Hashim Ayoub mwanzo pale alisema kwamba anampongeza Mhe. Zahra Ali Hamad, lakini mimi ninampongeza Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, kwa sababu si tu kwenye kamati yangu, lakini yuko makini zaidi kuliko mimi naomba nimpongeze katika hilo nimefurahi kwa majibu yake.

Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, mwenye dhamana ya Biashara na Masoko, naomba anielimishe kidogo tu katika aina hii ya mafuta ambayo yanaingia nchini, ametaja hapa aina zaidi 8, ni aina ipi ya mafuta ya kupikia ambayo angewashauri Wazanzibari watumie zaidi kwa msingi wa kujenga afya za mama na watoto.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija, napenda nichukue nafasi hii kupokea kwa dhati kabisa pongezi alizonipa na nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba jitihada hizi zinachangiwa kwa kiasi kikubwa na maelekezo yake wanayotoa wanapokuwa katika Kamati.

Mhe. Spika, katika swali lake Mhe. Mwakilishi, anataka ushauri wa mafuta ya kutumia ambayo yako salama zaidi. Mhe. Spika, masuala ya mafuta sote tunatambua kwamba mafuta yanayotokana na mimea tunaambiwa kwamba ni salama kwa matumizi ya binadamu zaidi kuliko mafuta yanayotokana na wanyama. Kwa maana hiyo nimshauri Mheshimiwa, pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwamba *vegetable oil* ni salama zaidi kwa matumizi ya Afya ya binaadamu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Spika, nami kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Katika majibu yake alieleza Mhe. Waziri, kwamba mafuta yale yanapokuja huwa wanayapeleka katika Bodi ya Madawa na Vyakula kwa ajili ya kufanyiwa uchnguzi. Mimi nilikuwa nataka kujua ni mara ngapi wamegundua kuna baadhi ya mafuta kwamba hayafai kwa matumizi ya binaadamu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, katika jibu langu kama amesikiliza vizuri Mhe. Mwakilishi, nimesema kwamba mafuta haya yanapoingia tu nchini huwa yanakaguliwa na Bodi ya Vyakula, Dawa na Vipodozi ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya. Sasa takwimu za mafuta ambayo yamepatikana hayafai ni kiasi gani takwimu hizo nitakuwa sina Mhe. Spika, itabidi nizifatilie Wizara ya Afya, lakini kwa sababu tunafanya kazi kwa pamoja, basi nitalifatilia na jibu hilo atalipata.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kikundi cha ushirika cha Mjimbini, Kangaani na Tondooni kimeshindwa na mashine ya kusagia mafuta ya *sun flower* ambayo ni biashara kubwa hapa Zanzibar, je, Mhe. Waziri, unawaambia nini wanakijiji hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, sijalifahamu vizuri swali lake kuhusu hiyo mashine.

Mhe. Spika: Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, rudia swali.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante Mhe. Spika, ninamuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa kuwa kikundi cha ushirika cha Mjimbini, Kangaani na Tondooni kimeshindwa na mashine ya kusagia mafuta ya *sun flower* ambapo

sasa hivi wanazo mbegu nyingi tu ambazo hiyo nayo ni biashara kubwa hapa Zanzibar. Je, Mhe. Waziri, unawaambia nini wananchi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kikundi hicho Mhe. Spika, ningeomba Mhe. Mwakilishi, kupitia kwake awaambie wafike Wizara ya Biashara, kwa sababu ni kazi ya Wizara ya Biashara kuangalia ni kiasi gani wanaweza kuviwezesha vikundi vya uzalishaji na hasa mazao ya biashara ili tuweze kukaa nao na kuona jinsi gani tutaweza kuwasaidia katika tatizo lao hilo.

Nam. 53

Uchakavu wa Skuli ya Msingi ya Muyuni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza :-

Ahsante sana Mhe. Spika, nirejee tena kuhusu Mhe. Zahra Ali Hamad na Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, mimi na Mhe. Hija Hassan Hija tulikuwa katika Kamati moja kipindi kilichopita kabla hujatupa uhamisho kwenda kamati nyengine, tulikuwa nae Naibu Waziri, Mhe. Sira na uwezo wake tumeuona. Na bahati vile vile umetupanga katika kamati nyengine mimi na Mhe. Hija Hassan Hija katika Wizara ya Biashara na uwezo wa Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, tumeuona.

Mhe. Spika, kuwa na diploma, *degree*, *master*, na *PHD*,mimi ninafikiri si uwezo mkubwa. Mhe. Zahra Ali Hamad, ameonesha uwezo mkubwa katika kujibu maswali katika Baraza hili katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mhe. Zahra Ali Hamad, nikupongeze kwa dhati kabisa ndani ya nafsi yangu kwa uwezo wako na jitihada unazozionesha. Na naomba Manaibu na Mawaziri waige mfano wa Mhe. Zahra Ali Hamad hajibu swali mpaka ende *field* kwenda kuangalia, nilimuuliza swali kipindi kilichopita....

Mhe. Spika: Uliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tuendelee Mhe. Spika.

Serikali imekuwa ikichukua hatua ya kuimarisha kiwango bora cha elimu ikiwemo kuwa na skuli zenye hadhi kama ujenzi wa skuli ya sekondari za Wilaya. Skuli ya Msingi Muyuni imekuwa katika kadhia ya uchakavu inayosababisha watoto wasome katika unyonge mkubwa kinyume na malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ya 1964.

(a) Kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu, serikali imechukua hatua gani ya kuhakikisha inakaa pamoja na kamati ya skuli na kulipatia

ufumbuzi tatizo la uchakavu ambalo limesababisha wanafunzi kusoma katika mazingira magumu kutokana na mapaa yake kuvuja.

(b) Wizara imechukua hatua gani ya kutekeleza kwa vitendo,kuna msemo wa Kiswahili kuwa 'kinga ni bora kuliko tiba' kutokana na kuta za Skuli hiyo kukabiliwa na uchakavu mkubwa na kusababisha wanafunzi kusoma katika mazingira hatarishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali- Alijibu :-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 53 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Kabla ya kujibu na mimi nasema ninamshukuru na sifa hizo sitanifanya niwe na *speed* zaidi ya kufuatilia kazi ambayo nimetumwa na wananchi. Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali imekuwa ikichukuwa hatua ya kuimarisha miundo mbinu ya skuli zetu kama ujenzi wa skuli za sekondari kupitia mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya lazima.

Pia, ni kweli kuwa baadhi ya majengo ya skuli ya msingi ya Muyuni yamechakaa na yanahitaji kufanyiwa ukarabati. Majengo ya skuli yaliyochakaa ni mengi sana na kutokana na uwezo mdogo wa kifedha, Wizara haina fedha za kutosha kuyafanyia ukarabati yote kwa pamoja.

Hata hivyo, pale Wizara inapokuwa haina uwezo wa kutosha kuyafanyia ukarabati majengo ya skuli huwaomba wananchi wachangie katika ukarabati wa skuli zao. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imepanga kuyafanyia ukarabati majengo ya skuli 12 tu za msingi, Unguja na Pemba. Miongoni mwa skuli za Mkoa Kusini Unguja zitakazofanyiwa ukarabati ni skuli ya Mwera na Kitogani. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

Ukarabati wa skuli ya Muyuni haukupangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2013/2014, bali utaingizwa katika mpango wa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

a) Wizara katika kutekeleza kwa vitendo msemo wa Kiswahili kuwa "Kinga ni bora kuliko tiba" imezipa uwezo Kamati za Skuli kupanga mipango na mikakati ya ujenzi wa madarasa mapya na kuyafanyia ukarabati majengo ya skuli zao.

b) Napenda kutoa wito kwa Kamati za Skuli zote, ikiwemo Kamati ya Skuli ya Muyuni kuanza mipango ya kuyafanyia ukarabati majengo skuli zao na Wizara itaendelea kuunga mkono juhudi zao kwa kukamilisha kazi ambazo zimeanzwa na wananchi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa kuwa elimu ndio msingi wa maendeleo ya nchi, serikali inatumia vigezo gani katika kupanga vipaumbele katika bajeti kuu na kuacha skuli kuchakaa na kufika kuvunjika.

b) Mhe. Naibu Waziri, utachukua hatua gani za dharura kama hali ulivyoiona jana mwenyewe kwa macho yako ili kuwanusuru wanafunzi wale ili wapate kusoma katika kipindi hiki cha mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama ambavyo nilizungumza kwenye jibu langu mama, skuli ambazo zinatakiwa kufanyiwa ukarabati ni nyingi na bajeti yetu ni ndogo. Na Mhe. Jaku Hassan Ayoub, atakuwa ni shahidi katika hiyo kutumia kipaumbele mwaka jana tulitengeneza banda lake moja pale la skuli ya Muyuni na kama ambavyo nimeahidi katika bajeti inayokuja kwa sababu kama nilivyosema kuna Wawakilishi wengi, kuna majimbo mengi ambayo yanataka yatengezewe skuli zao na bajeti yetu Mhe. Spika, ni ndogo haitutoshelezi.

Mhe. Jaku Hassan Ayoub, naomba urudi kwenye bajeti yetu ukurasa 24-25, Uimarishaji wa skuli za msingi tuna bilioni moja pale Mhe. Spika, na bilioni moja hiyo tumepanga kutengeneza skuli 12 ambazo hizi nimezizungumza. Lakini pia, tuna majengo ambayo wameanzisha wananchi karibu majengo 480 tumepanga kuyamaliza kwa pesa hizi.

Pia, kwa pesa hizo hizo tunataka tumalizie nyumba tatu, kuna ununuzi wa madawati 1000, lakini kuna kuwawezesha walimu kuweza kujihusisha katika mradi huu wa TZ 21. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wawakilishi najua matatizo ambayo yapo katika majimbo ya skuli zenu nyingi ni mbovu na nyingi ambazo zinahitaji kutengezwa. Lakini mtizame na huu uwezo wa Wizara katika kukamilisha hayo.

Na ndio Mhe. Spika, ninasema na ninashukuru hilo wananchi wameliitikia kuwa Kamati za Skuli tumezipa uwezo wa kuanzisha majengo, lakini na kukarabati pale ambapo wanaona skuli zao zina matatizo na sisi Wizara tutathamini hizo nguvu tutahakikisha kama pale ambapo wameanza na sisi tunamaliza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Mhe. Spika, sera ya elimu na sheria ya elimu inasisitizwa kutokuachwa kwa mtoto yoyote kusoma skuli na Wizara yake imetangaza mara kadhaa kwamba imevuka lengo la uandikishaji wanafunzi kwa zaidi ya asilimia 100. Hivi ninavyomwambia skuli shehia za Muambe jimboni kwangu wanafunzi wameachwa kuandikishwa kwa sababu hakuna madarasa ya kukaa licha ya kwamba wananchi na Mwakilishi wao wamejenga mabanda hayajaezekwa.

- Je, utatoa tamko leo kwamba wanafunzi wale walioachwa wachukuliwe na mimi na wewe tuwatafutie pahala wanafunzi wale wasome ili wasikose haki ya msingi.

- Hivi karibuni serikali imetia saini *memorandum* of *understanding* na kampuni ya *Gas Ras Al Khaimah* na wameahidi kwamba watasaidia madarasa 300 kwa nini haya madarasa ambayo yamekaa muda mrefu yakiwemo ya Muyuni na Muambe kule Pemba, hutamki leo kwamba utayapa kipaumbele ili tukajenga imani kwamba utasaidia. Kwa sababu hofu iliyopo kwamba majengo yanayojengwa ni yale ambayo yana wakubwa kwenye Wizara ya Elimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nataka nikiri kama sina taarifa ya wanafunzi ambao wameachwa Skuli ya Kiwani. Na kama wapo Mhe. Spika, wanafunzi hao mimi leo ninakwenda Pemba tayari nimekuaga, nitakwenda Skuli ya Kiwani nikifika tu Pemba na kuhakikisha kama wanafunzi hawa wamepatiwa sehemu ya kusoma.

Kwa sababu ninajua uwezekano wa wanafunzi kupatiwa nafasi ya kusoma upo Mheshimiwa licha ya kuwa tuna matatizo kweli, lakini hatujafikia hapo na nataka nilisisitize ni kweli kama tumevuka malengo ya dunia, malengo ya *millennium* ya kuhakikisha kila mwanafunzi anayefikia umri wa kusoma anapata nafasi ya kusoma. Kwa hivyo, hilo Mheshimiwa ninakuahidi kama nitalifatilia na wanafunzi hao nitahakikisha wanaingia darasani na kusoma itakapofika wakati.

Hili la pili, Mheshimiwa sitaki nitoe ahadi hapa kwa sababu kama alivyosema saini ni kitu kimoja na utekelezaji ni kitu chengine. Baada ya kwisha kupata msaada huu kama Wizara tutakaa na kuona ni skuli gani ambazo ziko taabani sana tutazisaidia Mhe. Spika, kwa sababu ni wajibu wetu. Ninakushukuru sana.

Taarifa

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, taarifa yangu ziara yake ya Pemba asiende Skuli ya Kiwani ende Skuli ya Muambe ambayo ndio yenye tatizo hili. Akenda Kiwani ataambiwa Mwakilishi ameongopa, lakini ende Muambe ambako takwimu ya wanafunzi walioachwa ipo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nitakwenda Muambe.

Nam. 19

Vipindi Vinavyokiuka Maadili Kwenye T.V.

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza :-
Ahsante sana Mhe. Spika kabla Mhe. Waziri hajajibu swali langu naomba nitumie dakika moja nifanye mambo yafuatayo:-

Kwanza kabisa kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi ninachukua fursa hii kutoa mkono wa pole kwa ndugu zetu wa Afrika Kusini kutokana na kufiliwa na kiongozi wao *Chief Carter Madiba,* kwa kweli kufiwa kwao ni kufiwa kwetu. Kwa sababu huyu ni kiongozi ambaye ni kioo ambacho Ulimwengu mzima unataka wakiangalie kutokana na mambo ambayo aliyafanya katika uhai wake.

Pili, napenda vile vile kutoa pole kwa Mhe. Naibu Waziri wa Afya Dr. Sira kutokana na kufiwa na mama yake mzazi, kwa kweli kwa niaba yangu na wananchi wa Wawi tunampa pole sana na *Inshaalla* Mwenyezi Mungu ailaze mahala pema peponi maiti.

Mwisho kabisa Mheshimiwa kwa niaba yangu na kwa niaba ya familia yangu napenda nitoe shukurani za dhati kwa Ofisi yako kupitia kamati yako ya Kudumu ya Fedha na Uchumi kwa kuweza kushirikiana nami katika kipindi kile cha msiba. Kwa hivyo, kwa niaba ya familia yangu inayoongozwa na Bwana Nassor Bin Juma, tunashukuru sana Ofisi yako kwa kuweza kuwa nasi katika kipindi kile cha msiba. Kwa hivyo, nasema ahsante sana.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu sana naomba swali langu namba 19 lipate majibu hivi sasa.
Kwa kuwa Televisheni na Radio ndio Kioo cha jamii na kwa kuwa katika vipindi mbali mbali vya Burudani kupitia *ZBC-TV* wasanii wamekuwa wakivaa mavazi, sambamba na kucheza michezo inayopelekea kwenda kinyume na mila, silka na desturi za Kizanzibari.

(a) Je, serikali haikujipangia utaratibu wa kuzihakiki sanaa hizi.

(b) Kama sanaa hizi hazifanyiwi uhakiki si zitaendelea kuipotosha jamii badala ya kuielimisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo –Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 19 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa vyombo vya *TV* na Redio ndio kioo cha jamii na kwamba kuwepo kwa vipindi vya burudani kupitia *ZBC*, wapo baadhi ya wasanii wamekuwa wakivaa mavazi ambayo ni ya kunengua michezo inayopelekea kukiuka Mila, Silka na Desturi za Kizanzibari.

Mhe. Spika, Serikali kupitia vyombo vyake vya Bodi ya Sensa na Baraza la Sanaa imekuwa ikifanya utaratibu wa kupitia kwa kazi hizo kwa lengo la kupunguza ukiukwaji wa maadili ya Kizanzibari.

Mhe. Spika, kuzuiliwa kwa vikundi vya sanaa kama vile "*Off side Trick"* cha kizazi kipya na baadhi ya nyimbo zake, kama vile "nyama ya bata ni tamu" mfano hai wa hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kupunguza ukiukwaji wa maadili. Aidha, ndani ya vyombo vya habari vya *ZBC* na Shirika la Magazeti la Zanziba Leo kuna kamati maalum za uhakiki wa sanaa.

Mhe. Spika, ni wazi kuwa iwapo sanaa hazitofanyiwa uhakiki zitaendelea kupotosha jamii badala ya kuelimisha na kuburudisha, ili kuondokana na hilo, wizara yangu haitofumbia macho mwenendo huo utakapoendelea kuvunja mila na desturi za Kizanzibari.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mavazi mara nyingi huwa yana-*determine national identity*, yaani ndio yanakuwa utambuzi wa kitaifa, na kwa kuwa Wazanzibari mila na silka za Kizanzibari ni kuvaa mavazi ya heshima na taadhima ya hali ya juu, na kwa kuwa kwa sasa hakuna sheria iliyoletwa katika Baraza hili inayozungumzia mambo ya mavazi.

Je, Mhe. Spika, isingekuwa vyema kwa wizara yake Mhe. Naibu Waziri ambayo ndio inayoshughulika na mambo ya silka na tamaduni za nchi kuleta mswada hapa Barazani wa mavazi ili kuweza kulinda utamaduni wa nchi. Hilo la kwanza.

Pili, kuendelea kuwaachia hawa vijana wa *Bongo Flavor* na Rusharoho kucheza nusu uchi na nyinyi kuwaonesha katika vyombo vyenu vya habari huku si kuudhalilisha utamaduni wa Zanzibar pamoja na kupoteza maadili kwa kutumia televisheni ambayo sisi tunalipa kodi ili kuendesha televisheni ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba sheria ya mavazi ipo tangu wakati wa mwaka 1964.

Mhe. Spika, swali lake la pili kuhusu wasanii wetu, kwa kweli Mhe. Mwakilishi mavazi ni kitu kizuri sana kama tulivyoeleza katika swali mama kuwa Bodi ya Sensa inashughulikia uhakiki wa mavazi. Sasa nataka nimwambie kwamba kwa kushirikiana na yeyé, kwa sababu vikundi hivi vinatoka kwenye mikoa na wilaya zetu, basi tuweze kukaa navyo vikundi hivi ili kuvielimisha. Nataka nikuhakikishie kwamba na wizara inakaa ili kuvifahamisha vikundi hivi kuhusu mavazi na mambo mengine yanayohusiana na mila na desturi za Kizanzibari.

Utaratibu

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kwa sababu hichi ni chombo cha wananchi, na wananchi wengi wanakisikiliza nadhani na nje ya nchi hii. Mimi ninayoikumbuka ni *Presidential Decree* ya mwaka 1972 ile tuliyodhibiti mabuga na chupa hapa aliyoitoa Mzee Abeid Amani Karume. Je, Mhe. Naibu Waziri anaweza akaniambia ni sheria namba ngapi na ya mwaka gani inayodhibiti mavazi.

Mhe. Spika: Sijakufahamu Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika. Mhe. Naibu Waziri amejibu kwamba sheria inayodhibiti mambo ya mavazi ipo katika nchi hii. Mimi nasema kwamba ninayoikumbuka ni ile *Presidential Decree* ambayo ilitolewa na Mzee Karume ya kudhibiti mabuga pamoja na chupa hapa nchini, suruali zile za mabuga pamoja na suruali za chupa zile zilizokuwa zikibana sana huku chini tukawa tunadhibiti kupitia Valantia. Sasa lakini sikumbuki kama kuna sheria, hivyo kama ipo anambie ni sheria namba ngapi na ya mwaka gani ili tuweze kuliweka sawa Baraza.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi, mimi hapa nilipo nina umri wa miaka 53 na mimi nafahamu na Mzee Abeid Amani Karume, mimi namfahamu, hayo yote unayoyasema Mheshimiwa nasema kwa uhakika, kwa

sababu na mimi hayo mavazi nimeyavaa nilikuwa ni mwanafunzi nasoma Skuli ya Forodhani tulikuwa tunavaa suruali tukiwa ni wanawake na hilo Mhe. Mwakilishi nataka nikwambie lipo, sheria ipo sasa hivi tunatakiwa tufanye marekebisho tu ya sheria hiyo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, labda kwa idhini yako pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa kama alivyotangulia kusema Mhe. Saleh Nassor Juma kwamba hiki ni chombo chetu kikubwa na kumbukumbu zetu ni vizuri zikawa sahihi.

Ni kweli kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba sheria ya kudhibiti mavazi ipo ambayo ni Sheria Nam. 1 ya mwaka 1973, inaitwa ni Sheria ya Kulinda Utamaduni wa Taifa Nam.1 ya mwaka 1973. Sheria hii Mhe. Spika, haijafutwa lakini utekelezaji wake ni kweli haufuatwi kama vile ambavyo sheria yenyewe inavyosema, kama itafuatwa nadhani wengi humu tutakwenda ndani kwa masharti yake yaliyopo.

Kwa hivyo, inahitaji kufanyiwa marekebisho na nadhani wizara inachukua hatua ya kuitazama tena sheria hii ili iendane na mazingira ya sasa hivi. Ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa vijana ndio hasa wanaopotoka na kuiga mambo yanayokwenda kinyume na mila, silka na tamaduni za Kizanzibari. Na kwa kuwa bado tunahitaji vijana Wabunge na Mawaziri wa Katiba na Sheria kama waliyotutembelea leo hii.

Je, serikali inachukua hatua gani kuona kwamba inatoa elimu juu ya kuenzi na kudumisha mila, silka na desturi za Kizanzibari kwa vijana.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tuna kipindi maalum *ZBC* cha mavazi, namuomba sana aangalie ili aone mavazi yetu ya Kizanzibari yanavyovaliwa na wanavyopendeza Wazanzibari wetu wa hapa visiwani.

Nam. 13
Jengo la Shirika la Bandari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Ni muda mrefu sasa jengo la Shirika la Bandari limeikosesha serikali mapato karibu miaka 23 sasa, na hasara inakisiwa kuwa Shilingi 830, 000,000/=

kutokana na uzembe wa watendaji wa Shirika la Bandari. Hivi sasa jengo lile limejengwa na kuwekwa *frame* za mbao na kupoteza taswira nzuri ya mfano wa majengo yaliyojengwa na Mfanyabiashara Mzalendo Bw. Said Salim Bakhressa.

(a) Je, wizara haioni aibu kuliharibu jengo lile kwa kuweka *frame* za mbao tofauti na majengo mengine ya kisasa yaliyojengwa na Bw. Said Salim Bakhressa.

(b) Kwa nini wizara isiombe msaada wa kulikarabati jengo lile katika mjengo wa kisasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano-Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 13 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, jengo analolizungumza lilikusudiwa kuwa *"Duty Free Shop"* hapo bandarini na lilijengwa na Kampuni moja ya Panama iitwayo *"ZANZIBAR DUTY FREE S.A",* pamoja na Kampuni tanzu ya wakati huo iitwayo *"WORLD DUTY FREE COMPANY LTD"* katika mwaka 1993. Baada ya kutokea mzozo wa kisheria baina ya wawekezaji hao na Wizara ya Fedha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifungua kesi Mahakamani na kupeleka mradi huo kusitishwa.

Kutokana na hali hiyo, Mahakama Kuu ya Zanzibar ilizuia matumizi ya jengo hilo kwa muda mrefu ambapo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Shirika la Bandari ilifanya jitihada za kuliomba kwa idhini ili kulitumia jengo hilo lakini ruhusa hiyo haikutolewa hadi mwaka 2009 ambapo Mahkama iliruhusu matumizi ya jengo hilo.

Mhe. Spika, kutokana na kukaa kwa muda mrefu bila ya matumizi, jengo hilo liliharibika kiasi cha kutofaa kutumika. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Shirika la Bandari baada ya kupata uwezo wa kifedha limeanza kulifanyia matengenezo makubwa jengo hilo kwa mujibu wa maelekezo na masharti ya Mamlaka ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe. Matengenezo yanayofanyika yanaendelea na mahitaji halisi ya kazi za shirika pamoja na ruhusa kutoka kwa wahusika yaani Mamlaka ya Mji Mkongwe.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, hivi sasa kama maelezo yangu ya awali yanavyojieleza tayari Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Shirika la Bandari wameanza kulijenga kisasa na matarajio yetu mapema mwezi ujao (2014) jengo hilo litakuwa limekamilika na litakuwa na sura na muonekano mzuri pamoja na kukidhi haja za kiofisi kwa shirika letu.

(b) Mhe. Spika, hatukuona haja ya kuomba msaada kwa kutambua kwamba gharama za ujenzi huo zinaweza kugharamiwa na serikali yetu na ujenzi huo utakamilika kwa muda usiokuwa mrefu kutoka hivi sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya rafiki yangu naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Je, serikali ilikuwa ikifanya utafiti gani kuwachunguza wawekezaji waliokuwa wababaishaji kabla ya kuangalia mikataba yao kama inavyotokea katika maeneo mengine hasa Sekta ya Utalii.

(b) Kwa kuwa jengo lile watendaji wakuu wa bandari ndani hawana ofisi za uhakika na wadau wengine, kuna mpango gani wa kutumia ofisi ile katika kipindi hiki cha mvua.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala la serikali kufanya utafiti kwa wawekezaji mimi naamini kwamba serikali iko makini na hakuna mwekezaji mbabaishaji ambaye atakuwa anakaa, kama litatokea kosa la mwekezaji ambaye hayuko makini kupewa nafasi, tabaan taratibu na sheria husika itamzuia na atashindwa, na serikali itarudi katika utaratibu wake wa kawaida kuhakikisha kwamba kila mwekezaji anayekuja nchini anakuwa mwekezaji makini atakayeleta tija na faida kwa wananchi wetu.

Swali la pili, kuhusiana na suala la ofisi. Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba jengo lile litakapokamilika mwezi Januari, 2014 tuna hakika kwamba ofisi zote muhimu wakiwemo rafiki zake wa rada na wengineo wote wataweza kupata nafasi ya kufanya kazi kwa utulivu na eneo ambalo litakidhi haja. Madhumuni ni kwamba, jengo hili likitumika tutapata nafasi ya kutizama mabanda mengi kuyavunja ili kuongeza nafasi pale kati kwa ajili ya kupata eneo la kuweka makontena.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tulimtegemea Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto atufanyie majumuisho hivi asubuhi kama vile tulivyokubaliana jana. Lakini nimetahadharishwa hivi leo asubuhi wakati nataka kuingia ukumbini, kwamba kumbe kulikuwa na orodha ya mambo mengi ambayo Mhe. Waziri alikubaliana na Kamati akayafanyie kazi halafu arejeshe kwenye kamati kuyaweka vizuri kwa pamoja.

Kwa sababu siku ya Jumatatu ilikuwa ni siku ya *holiday*, majibu hayo ambayo Mhe. Waziri, aliyafanyia kazi aliyatuma ofisini mapema, lakini sasa kamati ikawa haikukaa pamoja na Waziri ili wakayaweka vizuri kukamilisha kazi hii ambayo majadiliano tumemaliza jana. Kwa hivyo, baada ya kutahadharishwa, hivyo nikaelekeza kidogo iko kinyume na utaratibu, ilikuwa Waziri aje hapa na Mjumbe atoe hiyo taarifa kuniomba kwamba mswada huo urejeshwe kwa kamati ili kuweka vizuri yale mambo ambayo walikubaliana yafanyiwe kazi.

Sasa ilifikiriwa kwamba kazi ingekuwa ni fupi na kipindi hiki pengine ingekuwa tayari na kuweza kutoa majumuisho yakiwa yapo pamoja na yale mambo ambayo kamati walikubaliana wayaweke pamoja ili hatimaye kumaliza kazi ya mswada huu.

Kwa hivyo, hivi tunavyozungumza Kamati wako pamoja na Mhe. Waziri, kujaribu kuyaweka pamoja yale yote ambayo wizara walikwishayafanyia kazi ili aweze kuja kuyatoa pamoja na majumuisho yale mengine ambayo Waheshimiwa Wajumbe wametoa hoja mbali mbali. Hivyo, tumeelekeza kwamba kazi hiyo ya kufanya majumuisho sasa ije ifanyike jioni wakati hivi sasa kamati inaendelea na kazi hiyo ya kuweka pamoja yale yote ambayo wanaweza kukubaliana.

Kutokana na hali hiyo, basi inabidi tuzuie kifungu kidogo na tuendelee na shughuli inayofuata baada ya hapo. Kwa hivyo, moja kwa moja nimuombe Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ili kuwasilisha Mswada wake. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano karibu sana. Faida ya kuwa na *spare part* ambayo itakuwa itafanya kazi wakati wote ambapo mambo hayako vizuri. Karibu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny. Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano): Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikimwakilisha Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kuwasilisha Rasimu ya Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Barabara ya Zanzibar ya mwaka 2013.

Mhe. Spika, madhumuni ya Mswada huu ni kufanya marekebisho ya Sheria ya Barabara Sura ya 134 pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Marekebisho ya sheria yanayopendekezwa yanatokana na ukweli kwamba baadhi ya vipengele vilivyokuwemo kwenye sheria hiyo tayari vimeonekana kupitwa na wakati na hivyo kuhitaji kufanyiwa marekebisho ili viendelee kutumika katika kazi za kusimamia ujenzi na utunzaji wa barabara hapa Zanzibar.

Miongoni mwa maeneo ambayo mswada huu umezingatia ni muongozo juu ya eneo la hifadhi ya barabara, uwezo wa Waziri wa kuzigawa barabara kulingana na mahitaji ya kitaalamu na wakati husika, kufuta baadhi ya maneno na vifungu na kuongeza maneno na vifungu vipya.

Mhe. Spika, sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho kwa mara kadhaa na kwa mara ya mwisho ilifanyiwa marekebisho mnamo mwaka 1958. Mhe. Spika, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, sheria hiyo ya mwaka 1997 imeonekana wazi kuwa haitaweza kukidhi matakwa ya wananchi kwa wakati huu na ni wazi kuwa haitakwenda sambamba na mabadiliko ya sekta ya usafiri.

Mhe. Spika, kwa sababu ya matatizo ya kiufundi naomba niwasiliane na Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Mhe. Spika, naomba kurudia, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, sheria hiyo ya mwaka 1997 imeonekana wazi haitaweza kukidhi matakwa ya wananchi wakati huu na ni wazi kuwa haitaenda sambamba na mabadiliko ya Sekta ya Usafiri wa Barabara.

Hivyo, kuhitajika kufanyiwa marekebisho. Aidha, mabadiliko ya mfumo wa usafiri idadi ya vyombo na mabadiliko ya mfumo wa utawala ni miongoni mwa sababu zilizopelekea sheria hiyo kufanyiwa marekebisho ili iendane na mabadiliko haya.

Mhe. Spika, kwa vile marekebisho yanayopendekezwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usafiri wa Zanzibar ya mwaka 2008 na

Mpango Mkuu wa Usafiri Zanzibar wa mwaka 2009, ambazo kwa pamoja zinahimiza kuwepo kwa mpango madhubuti wa usimamizi wa ujenzi na utunzaji wa miundombinu ya barabara na huduma za usafiri Zanzibar, ni wazi kwamba sheria hii itakuwa na nafasi nzuri ya kutuletea ufanisi katika kuendeleza kazi za barabara.

Mhe. Spika, lengo la kuleta mapendekezo na kuifanyia marekebisho sheria hii ni kuondoa mapungufu yaliyojitokeza na kukidhi malengo ya uimarishaji na usimamizi wa miundombinu ya barabara Zanzibar yanafikiwa.

Mhe. Spika, Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Barabara umegawika katika vifungu 26 vifuatavyo:

Vifungu vyenyewe ni kifungu 1, 2, 3, 4, 5, 6, 7, 8, 8(a), 9, 10, 11, 11(a), 15, 19, 20, 21, 23(a), 24, 25, 26. 27, 30, 30(a), 32 na 33 kama ilivyoonekana katika bango kitita inayowasilishwa hapa.

Mhe. Spika, mwisho kumewekwa jadweli la barabara za Zanzibar. Mhe. Spika, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuchangia, kutoa maoni ili kupata sheria bora ya barabara.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Sijui kama hoja imeungwa mkono! Eee, hoja imeungwa mkono na Mhe. Mjumbe mmoja na wa pili amejitokeza. Nashukuru hoja imeungwa mkono, sasa mjadala uendelee. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Panya Ali Abdalla (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumshukuru *Allah Subhana Wataala*, kwa kutujaalia afya njema na kutupa nguvu ya kuweza kufika hapa leo kwa lengo la kuendelea na shughuli zetu za kawaida za kuwawakilisha wananchi wa Zanzibar katika chombo chao cha kutunga sheria.

Mhe. Spika, vile vile, niitumie nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, kwanza kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza hili tukufu na kwa busara zako zisizokuwa na mfano za kukiongoza chombo hichi muhimu katika kufanikisha malengo yake.

Naomba pia, niwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe pamoja na Makatibu wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi, ambao kwa ushirikiano wao na nguvu yao ya kufanya kazi bila ya kuchoka, ndiyo iliyonipa mimi ujasiri wa dhati wa kusimama mbele ya hadhara hii tukufu kutoa maoni waliyoyatoa kuhusiana na mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Amri ya Barabara ya Sura 134.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema nianze kutoa muhtasari wa maoni hayo kwa kuipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kufikiria mawazo mazuri na yenye tija ya kurekebisha Amri ya Barabara; ambayo ni hakika kwa wakati huu tulionao ilikuwa haitoshelezi kukidhi mahitaji ya maendeleo ya nchi tuliyoyafikia, hususan katika sekta ya Barabara.

Nazungumza hayo kwa sababu, tulikuwa tukishuhudia ajali nyingi zikitokea katika barabara zetu siku hadi siku. Sababu za ajali hizo Mhe Spika, ni nyingi, lakini miongoni mwa hizo ni uwekaji wa matuta kiholela bila ya kufuata sheria.

Pia, uharibifu wa barabara na kushamiri kwa vitendo vya wananchi kujenga pembezoni mwa barabara hali inayoipa serikali wakati mgumu pindi inapoamua kuongeza upana wa barabara zitakazokidhi mahitaji ya nchi. Lakini kwa mswada huu, tunaamini kuwa vitendo hivi vitakomeshwa kwa kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaohusika na vitendo hivyo.

Mhe. Spika, kamati inapenda kuikumbusha Serikali kwamba kuwa sheria ni kitu kimoja na usimamizi wa sheria ni kitu chengine.Hivyo, basi tunawaomba wale wote waliopewa dhamana kuisimamia sheria hii wahakikishe kwamba wanaifanya kazi hiyo kwa uadilifu wa hali ya juu. Kwani bila ya usimamizi mzuri, sheria hii haitakuwa na maana yoyote.

Nikielekea kwa upande wa vifungu vya mswada huu, kwa ujumla ni marekebisho ambayo yamejitosheleza. Hata hivyo, Kamati ilipendekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuboresha zaidi mswada huu. Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nigusie baadhi ya vipengele muhimu kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Kamati ilipendekeza kufanyiwa marekebisho kwa maelezo ya kifungu cha 15 cha mswada, ambapo iliitaka wizara kuitaja sheria ambayo itahusika na masuala ya fidia kwa mtu ambaye hakuridhika na fidia aliyolipwa na Idara ya Barabara kutokana na kuchimbwa kifusi katika ardhi yake kwa lengo la kujengea barabara za umma. Badala ya kutaja “Sheria ya Fidia” itajwe “Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya 1992 na Sheria nyengine zinazohusika”.

Ni imani ya Kamati kwamba kuitaja sheria hiyo kutaondoa utata na itampa urahisi mwananchi wa kawaida ambaye hana uelewa mkubwa wa masuala ya sheria kujua njia rahisi ya kupata haki yake iwapo hajaridhika.

Mhe. Spika, Kamati pia ilipendekeza, katika kifungu cha 23(v) ambacho kililetwa na Wizara ikiwa ni nyongeza ya marekebisho ya Mswada, kwamba badala ya kuipa mamlaka Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara peke yake kufanya maamuzi ya kukubali maombi ya kujengwa matuta ya barabarani, basi mamlaka hayo apewe Waziri ambaye atapokea maombi yaliyotumwa katika Idara hiyo. Hili pia litafanikiwa zaidi iwapo Waziri kabla ya kufanya maamuzi hayo atashauriana na Idara.

Katika kutilia mkazo suala la matuta yanayowekwa barabarani, ni vyema wizara kuyafanyia kazi kwa wakati maombi ya wananchi wanaotaka wawekewe matuta katika barabara ili waweze kupunguza ajali na uwekaji wa matuta yasiyokuwa na viwango. Ikiwa maombi hayo hayawezi kutekelezeka, basi wananchi waelezwe pamoja na sababu za kutotekelezwa huko.

Mhe. Spika, mara nyingi wananchi hufanya mambo kinyume na sheria kwa kukosa uelewa wa athari za mambo wanayoyafanya, lakini Kamati inaamini kwamba elimu itakayotolewa na idara husika kupitia vyombo vya habari kutasaidia sana kupunguza vitendo hivi vinavyoweza kusababisha maafa kwa wananchi wenyewe.

Kifungu cha 24(ii) cha Mswada, Kamati imeona ni vyema wizara ikakaa na kukitafakari upya kwa sababu marekebisho yaliyoletwa katika Mswada huu yameonesha kwamba faini ya fedha ambayo imefanyiwa marekebisho ni moja tu, ambayo kwa mujibu wa sheria mama ilikuwa ni Shilingi mia nne na hamsini, ambapo Mswada wa Marekebisho unapendekeza iwe Shilingi milioni moja.

Hata hivyo, Kamati inaona ni vyema na faini ya pili iliyomo katika kifungu hicho hicho. Pia, ifanyiwe mapitio kwani nayo imepitwa na wakati ambapo ni shilingi “mia saba na hamsini”. Kima hichi cha fedha ni dhahiri kwamba kwa wakati huu tulionao hakistahiki kuwa ni adhabu ya mtu aliyevunja Kanuni za Sheria ya Barabara.

Mhe. Spika, kwa kuwa sipendi kutumia muda wako mwingi katika kutoa maoni ya kamati kuhusiana na Mswada huu, hasa ukizingatia kwamba marekebisho kwa urefu yanaonekana katika waraka wa marekebisho ambao nina imani kwamba Wajumbe wote pamoja na wewe Mhe. Spika mmepatiwa.

Hivyo basi, Mhe. Spika, napenda nikushukuru kwa kunivumilia kwa muda wote nilioutumia kutoa maelezo katika Baraza hili. Ni imani yangu kwamba maoni hayo yatatoa mwanga fulani kwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu, kuweza kujua kwamba Mswada huu ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Na mimi kwa upande wangu nawaomba Wajumbe wenzangu tuujadili, tuuchangie na tuukosoe kwa lengo la kuboresha mswada huu na hatimaye serikali iweze kufikia malengo yake iliyojiwekea wakati ilipoamua kuleta mswada huu hapa Barazani.

Mhe. Spika, bila ya kusahau naomba pia niwashukuru wadau walioshiriki kutoa maoni yao kuhusiana na mswada huu kwa moyo wa dhati, ninawaambia tunathamini michango yao na wakati adhimu waliotumia pamoja na kuacha kazi zao muhimu ili kuja kutusikiliza. Kwa mwenendo huu, nchi inaweza kupiga hatua kubwa zaidi ya hapa tulipofikia.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, niruhusu niwataje kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Makatibu wake kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	MakamoMwenyekiti
3. Mhe. Marina Joel Thomas	-	Mjumbe
4. Mhe. Ismail Jussa Ladhu	-	Mjumbe
5. Mhe. Mohamed Haji Khalid	-	Mjumbe
6. Mhe. Salma Mohamed Ali	-	Mjumbe
7. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	-	Mjumbe
8. Ndg. Latifa Saleh Suleiman	-	Katibu
9. Ndg. Saad Othman Saad	-	Katibu

Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Sasa Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, ninashukuru kunipatia nafasi hii ya kwanza kabisa katika kuchangia hoja hii ambayo ipo mbele yetu.

Mhe. Spika, mswada huu kwa maumbile yake ni mdogo sana na una bahati mbaya ya pili kwamba ni mswada wa marekebisho ya sheria mama na bahati mbaya nyengine hiyo sheria mama

wengine hatuna, maana yake hii ilitungwa tokea mimi sijazaliwa. Kadri nilivyoona huu mswada ilitungwa toka kabla ya mapinduzi.

Sasa tuliwahi kuagiza hapa kwamba ni vizuri mawaziri hizi sheria waziweke karibu na sisi. Sasa hicho kifungu kinachorekebishwa, mimi sikijui, sijui kina mawazo gani na haya marekebisho yanakusudia kurekebisha kitu gani ndani ya kile kifungu. Sasa inakuwa ni tabu kidogo.

Sasa kwa msingi huo Mhe. Spika, mimi nitajaribu kuchangia, lakini zaidi kwa kuangalia matumizi ya lugha tu ya Kiswahili ambayo hiyo haihitaji *reference* ninajua imo kichwani mwangu. Na kwa msingi huo nataka nianze kwenye kifungu cha 1, kuhusu jina fupi na tarehe ya kuanza kutumika.

Ukisoma kifungu 1 (1) kinaeleza hivi,"Sheria hii inaweza kuitwa kama amri ya barabara"

Kwanza nataka nipongeze marekebisho yaliyofanywa na Kamati kwamba hii amri ya barabara, hili neno "amri" linatoka na badala yake linakuwa "sheria". Kwa hivyo, na mimi nakubaliana nayo.

Lakini na hili neno "kwamba sheria hii inaweza kuitwa", mimi nadhani si lugha nzuri sana ya kutumia. Ni afadhali tungesema moja kwa moja kama sheria hii itajulikana kwa jina la Sheria ya Barabara, lakini tukisema inaweza kuitwa maana yake ni jambo ama ukitaka utafanya usipotaka basi. Sasa nadhani tungerekebisha hapa kidogo.

Sasa baada ya pendekezo hilo la marekebisho, naomba sasa niende kwenye kifungu cha 13 cha mswada huu ambacho kinarekebisha kifungu cha 11 cha sheria mama. Na hapa kidogo matumizi ya lugha Mhe. Spika, pia hayajakaa vizuri.

Kinasema hivi sheria mama inarekebishwa kwa kuingiza kifungu kipya cha 11 (a) kama ifuatavyo:-

Kifungu cha 11 (a) Waziri atasababisha mpango au ukaguzi kutayarishwa.

Sasa hili neno "atasababisha", mimi sifurahii, kwa sababu Kiswahili ni lugha yetu. Maneno kama haya yanataka aseme Mzungu aliyekuwa si Mswahili hajui mantiki ya Kiswahili, lakini kwa sisi tuliobobea katika lugha ya Kiswahili Mhe. Spika, mimi nadhani tungesema tu, "Waziri ataagiza mpango au ukaguzi", lakini ukisema, "atasababisha", mimi nadhani katika Kiswahili si lugha nzuri. Kwa hivyo, naomba nalo hilo Waziri alichukue kwa marekebisho.

Nikitoka hapo niende kwenye kifungu cha 18, kipo ukurasa wa 362, kuna hifadhi ya barabara pale. Sasa hapa nilitaka nizungumze kidogo kuhusu mamlaka ya barabara. Mhe. Spika, hizi barabara zetu zote zina mipaka yake na wataalamu wanatwambia ziliekewa mpaka *beacons* za barabara. Lakini sijui niseme kama ni muhali mwingi tulionao Wazanzibari au tuseme sijui ni uzembe, kwa sababu sheria kama ipo halafu ukaifumbia macho kwa kumuonea mtu muhali, mimi nadhani ni uzembe.

Sasa matokeo yake ni kusababisha matatizo baadae. Kwa sababu Afisa wa barabara au mtu wa mamlaka ya barabara anajua kama barabara hii mipaka yake ipo hapa, lakini anapita leo pamepigwa *foundation* ndani ya *beacon* na yeye akanyamaza kimya, au siku nyengine anaweza akauliza ya nani hii, akaambiwa hiyo ya mtu wa fulani bwana, aah! Kama ya mtu wa fulani basi, akaachiwa akajenga ndani ya barabara, na jirani ya yule aliyejenga akiona fulani kajenga na yeye kaweza na yeye atafanya juhudi na yeye atajenga.

Hatimaye barabara yote nzima Mhe. Spika, inajengwa. Ukija mpango sasa wa kupanua ile barabara, wanakimbilia mule mwenye *reserve* ambamo mushajengwa. Sasa ukitaka kumuondosha mtu ulipe fidia. Fidia ambayo kwa kweli haikuwa ya lazima kabisa kwa sababu ile ilikuwa ni eneo la barabara toka mwanzo, mara nyengine unaweza kusema ni kutumia pesa za wananchi vibaya. Kumpa mtu fidia wakati kafanya kosa makusudi yeye mwenyewe.

Sasa hizi lawama zangu, ninavika kwa Mamlaka ya Barabara kwamba wanafanya uzembe kuwaachia watu wakajenga katika maeneo ya barabara. Kwa hivyo, naomba sana watu wa mamlaka ya barabara pamoja na wizara kwa jumla katika suala la kufuata sheria, maana tukishatunga sheria ile sheria inakusudia kuondoa matatizo.

Sasa tukishatunga sheria, kwa nini tushindwe kuisimamia ile sheria ikafuatwa ambayo kama hatukusimamia matokeo yake baadae yanakuja kuwa matatizo kama haya ya kupoteza pesa za wananchi isivyo vya lazima.

Kifungu cha 19 ambacho kinarekebisha kifungu cha 24, kuna matumizi pia ya lugha nayo si mazuri, maana yake mara nyengine tunaambiwa ni hifadhi ya barabara. Lakini hapa sasa ukisoma utakuta kuna maneno "akiba ya barabara". Mimi nafikiri kutumia neno "akiba" si uzuri, bora tutumie lile neno "hifadhi ya barabara". Kwa hivyo, ninapendekeza hilo neno "akiba ya barabara" hapo bora liondolewe na badala yake iwekwe "hifadhi ya barabara".

Nikitoka hapo kifungu hicho hicho cha 19 (2) sasa, pia napo pana matumizi ya lugha ambayo si nzuri. Kinasema kile kifungu cha 19 (2) "Mtu yeyote au taasisi atakayekwenda kinyume na kifungu cha 19 (1) atakuwa na hatia ya

kutenda kosa na ikithibitika atastahili adhabu ya faini ya mia tano elfu". Naomba sana hili neno, “mia tano elfu" litoke kwa sababu kuna maneno maarufu katika lugha ya Kiswahili tunaita laki, hizi ni laki tano bwana. Kwa hivyo, badala ya "mia tano elfu" tuseme, "laki tano".

Na ukisoma kifungu cha 20 ambacho kinarekebisha kifungu cha 25 cha sheria mama. Kule mwisho nacho ni kifungu cha adhabu vile vile, lakini kule mwisho kuna, ngoja nikisome chote nacho.

Kifungu cha 25 cha sheria mama kinarekebishwa sehemu ya adhabu kwa kuongeza maneno "sio chini ya shilingi milioni moja" na kufuta maneno sio zaidi ya shilingi mia nne hamsini elfu. Na hili neno "mia nne hamsini elfu", hii maana yake ni laki nne na nusu. Huyu aliyestafsiri hii sheria, maana yake hii sheria ilikuwa ni ya Kiingereza, sasa imetafsiriwa Kiswahili, lakini inaonekana huyu aliyetafsiri hajabobea katika lugha ya Kiswahili Mhe. Spika. Kwa hivyo, nayo hii pia isomeke "laki nne na nusu" na sio mia nne na hamsini elfu".

Sasa nikiendelea baada ya neno adhabu na badala yake kuandika neno na sio zaidi ya shilingi milioni tatu na miezi mitatu itabadilishwa kuwa miezi kumi na mbili na hii neno miezi 12 Mhe. Spika, ni afadhali isemwe ni mwaka moja ndio lugha sanifu na hata lugha ya Kimahakama ndio inavyotumika hivyo.

Na ukisoma kifungu cha 21 ambacho kinarekebisha kifungu cha 26 cha sheria mama. Pia, nayo pale kati kati, yaani kuna (a) na (b). Hiyo (b) pale kati kati pana maneno, "mia tano elfu" yamejirudia. Naomba pia nayo iandikwe, "laki tano".

Nikiondoka hapo kwenye kifungu cha 24. Mhe. Spika, kifungu hichi cha 24 kinarekebisha kifungu cha 32 cha sheria mama. Hichi kifungu sina tatizo nacho, lakini ukisoma kifungu cha 25 cha mswada, sasa kinarekebisha kifungu cha 30.

Sasa utakutia hichi kifungu cha 25 kinarekebisha kifungu cha 30, lakini kifungu cha 24 kinarekebisha kifungu cha 32 kama kwamba 32 imetangulia kuliko 30, naona kama sio mpangilio mzuri wa vifungu. Ilivyo hasa ilikuwa hichi kifungu cha 24 ambacho kinarekebisha kifungu cha 32 basi kije chini na kiwe cha 25, na hichi ambacho cha 25 kinachorekebisha kifungu cha 30 kikae pale juu kiwe cha 24. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri, aangalie hilo kwa sababu hapa mpangilio umekwenda kinyume mbele.

Na mwisho kabisa ni kifungu cha 26, kifungu hichi kinasema sheria mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 33 kama ifuatavyo. Lakini

sasa hicho kifungu chenyewe hakipo hakikuandikwa. Sasa naomba Mhe. Spika, Mhe. Waziri labda afanye *reference* kwenye makabrasha yao wakiandike hichi kifungu, maana hakipo na hakionekani kabisa.

Baada ya marekebisho hayo Mhe. Spika, mimi nataka nikubaliane na Mhe. Waziri, kwamba kulikuwa na haja sana ya kuirekebisha hii sheria sura ya 134 kama alivyoeleza kwamba ilikuwa haitekelezeki kwa sababu vifungu vyake ni vya zamani sana mpaka leo vinataka wale watawala wa Kiingereza waliotawala siku hizo na Zanzibar kwenye sheria ile inaitwa koloni la Kiingereza.

Kwa hivyo, kulikuwa na haja kweli ya kuibadilisha ili maneno kama yale yatolewe kabisa tuwe na maneno yetu ya kisasa, maneno ya kimapinduzi. (*Makofi*).

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi mswada huu nauunga mkono na kwa niaba ya watu wa Jimbo la Chonga, mimi sina pingamizi nao. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea. Sijui kama inaonesha tumeridhika na michango, eeh! Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe.Spika, kwanza sina budi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kwa mara nyengine tena leo tukaweza kufika hapa na kuweza kuendelea na shughuli zetu kwa mujibu wa taratibu zetu ambazo huwa tunajiwekea.

Mhe. Spika, mimi sina mengi sana ya kuchangia leo katika mswada huu hususan ilivyokuwa kwamba ile kazi ya kuchambua pamoja na kutoa mapendekezo ndani ya mswada huu tulikwishaifanya baina yangu mimi na Wajumbe wa Kamati. Kimsingi nimesimama hapa Mhe. Spika, kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waujadili mswada huu na ikiwezekana wakubaliane na marekebisho ambayo ilikuwa sisi kama wanakamati tulikuwa tumeyatoa kwa nia na lengo la kuboresha mswada huu ili uweze kuleta mantiki na maana halisi ambayo ilikuwa imekusudiwa.

Mhe. Spika, mswada huu sisi kazi yetu kubwa ilikuwa ni kuboresha zaidi kifungu cha 134 cha sheria hii. Tulipokuwa tunapitia mswada huu Mhe. Spika, tuliona zile taratibu za malipo hasa, malipo yale ya faini ambayo yalikuwa yameekwa, malipo yale yalikuwa yamepitwa na wakati sana.

Kwa kushirikiana na Wajumbe wa Kamati tulitoa mapendekezo kwamba malipo yale kwa sasa yazingatie zaidi uhalisia wa thamani ya pesa yetu tuliyonayo kwa sasa, lakini vile vile, kuweza kutoa uzito fulani ili wale ambao watakuwa wanabainika kufanya makosa waweze kuona kwamba ile faini itakayokuja kujitokeza baadae ni faini ambayo inaweza kuwapa mazingira ya kuwasababisha kutokaribia kufanya kosa lile.

Mhe. Spika, lakini baada ya hapo vile vile, kamati yangu pamoja na kushirikiana na wadau wenzetu walitoa mapendekezo yao.Pia, kuona kwamba miswada mengine yote ambayo inakuwa inashushwa tuweze kujadiliana kwa pamoja na yale maoni yao ambayo wanakuwa wanayaleta kwetu tuyachukue na tuyajumuishe ili yaweze kwenda sambamba katika utaratibu wa kutengeneza sheria zetu mbali mbali ambazo hatimaye zitakuja kutumika katika nchi yetu.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, sasa niendelee kuwaomba tena Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa sababu kama nilivyokwishasema mwanzo kwamba kazi hii tumekwishaiangalia na kuifanya kwa uwezo wetu na kwa upana ambao tulihisi kwa upeo wetu sisi kuwa inatosheleza, niwaombe tena Waheshimiwa Wajumbe waendelee kuchangia zaidi na kutoa makosa pale ambapo wanahisi ipo haja ya kufanya hivyo, lakini na hatimaye wakubali kuupitisha mswada huu na iwe sheria iweze kutumika.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano bado yanaendelea. Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kukushukuru wewe kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia mswada.
Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa kuweza kuleta marekebisho haya. Haya marekebisho Mhe. Spika yalikuwa yaletwe zamani sana, kwa sababu suala la barabara katika nchi ni muhimu sana, sio tu katika suala la kurahisisha mawasiliano baina ya eneo na eneo, lakini suala la barabara ni jambo muhimu sana katika suala zima la uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, unapoiweka nchi katika *network* nzuri ya mawasiliano ya barabara, kwa kweli ni kusema kwa kiasi kikubwa umeufanya uchumi wa nchi hii uendelee na ndio maana mataifa mengi makubwa badala ya kushughulikia zaidi masuala ya anasa, huekeza sana katika *network* ya

barabara na hatimaye wanapata maendeleo. Hii ni kutokana na umuhimu wa mawasiliano baina ya eneo na eneo na nchi na nchi, ndio ambapo uchumi unaweza kukua.

Mimi juzi hapa Mhe. Spika, kwa sababu na mimi nilipata fursa ya kwenda kutembelea nchini China, nikaona mbona hawa Machina wameendelea sana, mbona sasa wamekuja juu sana katika masuala ya kiuchumi.

Ile siri Mhe. Spika, niliona kumbe siri moja kubwa iliyowafanya wenzetu wa China waendelee ni kutokana na kuweka vyema mtandao wao wa barabara, kiasi ambacho sio kwamba wanatumia hizi barabara hizi za chini, lakini kumbe mpaka barabara za ghorofa Mhe. Spika, zipo na zinafanya kazi, tena sio ghorofa moja tu, unaweza ukajikutia unapita katika mtandao wa barabara ghorofa ya kwanza, ya pili na ya tatu. Kwa kweli barabara ni jambo muhimu sana. Kwa kuwa sisi hatujafika huko, napenda niipongeze serikali kwa kuweza kuona kwamba kuna umuhimu sana wa kufanya marekebisho ya sheria zetu zinazohusiana na mambo ya barabara.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa kuweza kuleta mabadiliko ya sheria hii kuweza kukiingiza kifungu kipya cha 8 (a) ambapo kifungu cha 9 cha sheria hii inasema sheria mama hapa inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 8 (a) kama ifuatavyo. Kwa vile kuna mtandao wa barabara sasa umepanuliwa ikiwemo barabara kuu, barabara za vijijini, barabara mijini na barabara nyengine.

Kwa kweli hili walilolifanya serikali ni muhimu sana na kwa vyovyote vile Mhe. Spika, kuna umuhimu wa kuweza kuziingiza *feeder roads* katika mtandao mzima wa barabara zetu. Ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa nchi, lakini la kusikitisha Mhe. Spika, katika kipindi chote hiki serikali yetu ilikuwa inadharau sana hizi *feeder roads*. Kuna *feeder roads* ambazo zimekufa, kuna *feeder roads* ambazo zimesahaulika, kuna *feeder roads* hazijulikani ambazo zamani zilikuwa zikisaidia sana katika uchumi wa nchi yetu.

Kwa mfano Mhe. Spika, soko la Chake Chake pale Pemba linaunganishwa sana na barabara hii *feeder road* inayotoka Uwandani kupitia Vikunguni, Ng'ambwa kuja zake Gombani ya kati mpaka barabara kuu ya Chake Chake. Ile *feeder road* imesahaulika sana na mimi nilimwambia Mhe.Waziri, katika masuala kadhaa yaliyopita kwamba hizi barabara ni muhimu kwa uchumi, sio pale Pemba tu, lakini hata katika *network* ya uchumi wa nchi nzima hii.

Kwa mfano wale wenzetu kule Uwandani wanazalisha matofali haya ya kuchonga ambayo ni muhimu sana ambayo inabidi yasambazwe katika

sehemu kadhaa za Pemba na hata hapa Unguja nimeshaanza kuyaona yakiingia sehemu za Kaskazini, lakini barabara imekufa ambapo enzi za ukoloni ilikuwa ikifanya kazi vizuri.

Sasa mimi naamini uwepo wa sheria hii, uwepo wa marekebisho haya, basi ni matumaini yangu kwamba Mhe. Waziri, ataiangalia vizuri barabara inayotoka machimbo ya matofali Uwandani kupitia hapa Vikunguni kuja Gombani Ng'ambwa, kuingia Pima Mbili hadi kuja zake Kijitomavi pale mpaka kufikia barabara kuu, jambo ambalo tutawafanya watu Mkoani waweze kunufaika na matofali yanayotoka Uwandani, watu wa Pima Mbili na wao waweze kupata matofali vizuri pamoja na watu wa Muambe ambao kwa kweli sasa hivi nyumba zao zinakuwa si madhubuti kutokana na kukosa yale matofali kutoka Uwandani.

Ni matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri katika hili itakapopitishwa sheria hii, ataweza kuziona barabara zile ambazo sio tu kwa masuala ya ujenzi wa matofali, lakini hata viazi, ndizi nzuri na tamu zinazotoka Vikunguni, basi zinaweza zikaliwa mpaka Unguja kama barabara zile zitafufuliwa. Ni matarajio yangu kwamba Mhe. Waziri, hili ataliangalia sana.

Mhe.Spika, suala jengine katika suala zima la ujenzi wa barabara nimeona katika marekebisho kwenye kifungu cha 15 cha mswada, kifungu cha 19 cha sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kizima na kuweka badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo, naomba ninukuu hichi kifungu cha 19 (1).

Kifungu cha 19(1)

> "Mtu ambaye atakuwa hakuridhika na maamuzi ya idara ya malipo au kiwango cha fidia yanayotokana na tendo lolote au jambo lolote linalofanywa na idara kwa mujibu wa uwezo wake chini ya kifungu Nam. 13 atalazimika kupeleka ombi hilo la maandishi kwa utaratibu uliowekwa na sheria ya fidia"

Mhe. Spika, nadhani kifungu hiki kitakuwa ni mkombozi kwa sababu zifuatazo:-

Mhe. Spika, hizi barabara ili zijengwe huwa zinahitaji zipate kokoto. Kokoto hizi kwa kule Pemba zinatoka aidha jimboni kwangu Vitongoji au katika Jimbo la Micheweni la Mhe. Subeit Khamis Faki.

Mhe.Spika, kama kuna watu wanaoteketea na kudharaulika na kuumia kimaisha na kiuchumi, basi ni sisi watu wa maeneo haya, kutokana na sababu

zifuatazo, barabara ni muhimu, lakini vile vile na sisi tukiangaliwa pale ujenzi wa barabara unapofanywa. Mhe. Spika, hivi ninavyokwambia sisi watu wa Jimbo la Wawi hususan katika maeneo ya Makaani ambapo kuliko na athari hizi za kuchimba mawe.

Sisi tunategemea sana ardhi ya maweni kwa kilimo, lakini la kusikitisha leo unakuwa tayari umeshatayarisha mashamba yako ya tungule, viazi, njugu, mahindi na nyanya hizo una shamba lako ghafla unaambiwa Mawasiliano wanakuja hapa kuchimba kifusi kwa sababu watu wameshakuja wanataka kifusi, panapigwa *bulldozer*. Matokeo yake Mhe. Spika, hatulipwi fidia, matokeo yake tunadhalilika na sisi tunategemea sana kilimo hicho cha tungule ili kuweza kuwasomesha watoto wetu.

Kwa sababu kifungu hiki kilikuwa hakipo katika sheria ya barabara, ilikuwa tunadhalilika mno. Hivi ninavyokwambia Mhe. Spika, Mhe. Waziri, nilimwambia na nitakuwa mgumu sana mpaka anipe ufafanuzi katika hili ikiwa hali yangu itakuwa hairidhishi, ni kwamba Mhe. Waziri hapa aliniahidi kwamba kwa kweli wanakata miembe yetu, minazi na miti yetu, ili wanaikata kupitisha umeme wa kupeleka mashine ambayo mashine hiyo ndio inasaga hizo kokoto za kujengea barabara.

Akaniahidi kuwa mashine hizi tumeshazikodisha sisi na kupitia kodi hii, basi tutawalipa fidia wananchi wako. Mhe. Spika, wananchi wangu katika Jimbo la Wawi hususan katika maeneo kuanzia Wawi mpaka Vitongoji wamedhalilishwa sana, nadhani kwa sababu hii sheria ilikuwa haipo, kwa sababu nashukuru hiki kipengele cha 16 kifungu cha 20 kimeandikwa. Kwa mfano amesema kwamba kifungu cha 19 (2)

> "Endapo itatokezea kutokuwepo kwa sheria ya fidia mtu yeyote alazimika kufungua shauri hili Mahakamani"

Nashukuru kwamba kifungu hiki kimeeleza hivi. Hivi sasa mimi nasubiri jibu la Mhe. Waziri, kwa sababu sheria ipo na naomba Mungu ikifika tu asaini hii Rais, hii sheria mimi ninaiunga mkono na kwa vyovyote hivyo ninawaomba Waheshimiwa tuiunge mkono ipite na ikifika tu Mhe. Rais asaini, akishasaini Rais ninamsikiliza Waziri, kwa sababu kuna watu wanadai fedha zao chungu nzima ambazo walikatiwa miti yao zamani na Mhe. Waziri hapa akanidanganya kwamba tumeshaikodisha hii mashine na kwa vyovyote vile watakapolipa kodi zao watu hawa tutawalipa fidia wananchi.

Huu ni mwezi wa sita Mhe.Spika, kampuni zile zilizokodi zinafanya kazi, pesa chungu nzima zinapatikana katika mashine, watu hawa hawajalipwa fidia. Nasubiri hii sheria ipite tu na ninamuomba sana Dr. Ali Mohamed

Shein, akiiona katika meza yake hii sheria aisaini ili niweze kukimbilia Mahakamani iwapo Mheshimiwa huyu hawakuwalipa fidia watu wa Vitongoji.

Mhe. Spika, jambo jengine huu mtandao wa barabara umepanuka na kwa kweli sisi sheria zetu haziangalii sana mambo haya ya rasilimali watu, kwa bahati mbaya sana hizi sheria zetu tunazozitunga zinaangalia zaidi uchumi na sio njia kuu za uchumi. Njia kuu ya uchumi ni watu, ukiipoteza rasilimali watu katika nchi basi uchumi unakuwa mdogo.

Mhe. Spika, sisi tuna barabara inatoka Chanjamjawiri kuelekea Tundauwa, mimi kwa upande mmoja wa umamani kwangu ndio tulikuwa na matanga hapa Kiziwani na kwa bahati hapa Shungi palipokuwa na matanga ni karibu sana na barabara. Mhe. Spika, kwa kweli kila siku tulikuwa tunasalia mtume kwa kipindi kile cha msiba wa mzee wangu. Mhe. Spika, gari zinapita mbio, tumekwenda mawasiliano kuwaambia jamani hebu njooni mtuwekee matuta kuna baadhi ya watoto hawana akili na kila wakifika pale karibu na watu wanatia mbwembwe zaidi.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Spika, hii mamlaka inayohusika na kutia matuta iangalie katika maeneo ya watu. Kuna barabara inayotoka Vitongoji Makaani, kuanzia sokoni pale Udusini, tumeshapoteza watu wengi sana kwa magari kupita mbio na tukimwambia waziri anasema hapana, mambo ya matuta hapana. Tukimuendea Afisa Mdhamini, aah! mambo ya matuta haiwezekani tunaweka alama. Hawa masharobaro wanaoendesha gari hizi kwa kumuekea kwamba *50 km per hour* haoni, kwa sababu hawa wanaoendesha magari wakati mwengine sijui wana nini vichwani mwao.

Mhe. Spika, mimi naona katika maeneo nyeti, kwa mfano kwenye eneo la Vitongoji Udusini, eneo la Vitongoji Skuli, eneo la *Fidel Castro Secondary School* watuwekee matuta. Juzi pale alikosewa kijana mmoja anaitwa Meja, tena anateremka gari tu kumbe kuna gari linakuja mbio likamchukua. Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu sana, naomba sheria hii iwe makini katika kulinda rasilimali watu, kwa sababu tusiendelee kuwapoteza watu siku hadi siku kwa ajali za magari.

Mhe.Spika, nadhani sheria hii lengo lake kubwa vile vile ni kutoa urahisi wa watu katika kupita kwenye maeneo. Lakini inasikitisha kwa sasa mheshimiwa unapofanya *alternative* ni lazima uwe na kitu chengine umekiweka pembeni, kikifeli hiki nitafanya hiki.

Mhe. Spika, sitaki niingilie, kwa sababu pale napo tunazungumzia mambo ya watu na magari. Magari yalikuwa yanaegeshwa pale stendi ya daladala ya

Darajani hayasumbui watu, kwa sababu yalikuwa ni nje ya barabara. Lakini sasa hivi pale Kisiwandui katika barabara ile ya Michenzani, barabara ile ni kubwa na ina watu wengi, leo unakuja kuweka *bus stand* pale, tena karibu na ofisi ndogo ya Chama cha Mapinduzi ambapo siku nyengine pengine Rais wetu, anaweza kuwepo pale. Sasa unamkusanyia magari!

Mhe. Spika, mimi nashauri Mhe. Spika, kwamba Baraza hili ni miongoni mwa mihimili mikuu mitatu ya nchi. Kama kutakuwa na uwezekano basi itoke amri sasa hivi gari ziondoke pale, kwa sababu ya usalama wa Rais wetu.

Sababu ya pili Mhe. Spika, ni kutokana na usumbufu wa kumtoa mlipa kodi wa nchi hii, kuanzia Malindi kwa miguu anaburuta vibegi na watoto wanne au watano. Mlipa kodi huyu kaja na ile meli ya rafiki yangu Bakharesa, baada ya usumbufu mkubwa wa bahari na watoto kisha anaburura mabegi kuanzia bandarini hadi Michenzani.

Kwa hivyo, naomba sana mheshimiwa katika hili, nilikuwa nina mambo mengi, lakini kwa sababu nililazwa hospitali na afya yangu bado haijawa vizuri basi naomba nimalizie hapa na katika hili naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Saleh Nassor Juma, ujumbe umefika. Sasa tumkaribishe Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana. Leo kidogo nina mafua, hivyo sitoweza kusema kama mjumbe mwenzangu aliyeondoka kwa sauti kali sana.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Mjumbe mwenzangu amemkubali Rais wetu na kamtaja vizuri na kamtengenezea mazingira mazuri, Rais ambaye ni wa Chama cha Mapinduzi, namshukuru sana Mhe. Saleh Nassor Juma, na tena namuunga mkono Mhe. Spika, kwa kukumbuka hilo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujaalie, ama kweli hii ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kuwa leo anatusifia hivyo!

Mhe. Spika, pia, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kutufikisha leo sote tukiwa hai, waheshimiwa wako hapa wazima wa afya, pamoja na wewe kiongozi wetu *alhamdulillah* unachukua muda mwingi sana hapo kukaa ukatusikiliza na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akuzidishie afya njema, uendelee Mhe. Spika. Maana yake mimi ukiniweka hapo kwa muda mchache tu nashindwa.

Mhe. Spika, huu mswada mimi nimeufurahia sana na nimeusoma kwa muda mchache sana na nimeona kweli kulikuwa kuna mapungufu huko nyuma. Pia, Mhe. Spika naskitika kwani leo naona juu hakuna mtu hata mmoja kutoka wizara yake wakati huu tunachangia mswada huu, kwa kweli Mhe. Spika, haileti sura nzuri sana siku kama ya leo kuwa watendaji ambao watakaokuwa watekelezaji wa mswada huu hawapo.

Jambo hili siku zote tunasema Mheshimiwa, tunapoleta miswada basi wale watendaji wao wakubwa waje katika jukwaa kule juu na wao wasikilize ni nini kinachozungumzwa kutoka kwa wajumbe. Kama wana matatizo mengine tutawasamehe, lakini kama hawana tatizo basi haileti picha nzuri kwa mujibu wa utaratibu.

Mhe. Spika, nikienda kwenye mswada wenyewe, wenzangu wengi waliokwisha kuchangia wamepiga kelele sana na hasa kaka yangu pale Mhe. Saleh Nassor Juma. Kwa kweli ameyaona masuala ambayo ni lazima yarekebishwe na yaweze kutiliwa nguvu kwa utekelezaji.

Mhe. Spika, sheria tunazitunga, lakini tatizo la sheria zetu usimamizi wake unakuwa ni mdogo sana na hili ndilo ambalo linatufikisha pahala pabaya sana. Hasa kama mimi *professor* kuchangia jambo Mhe. Spika, likawa halifanyiwi kazi basi sijisikii vizuri, kwa sababu najikongooa kabisa kutoa mawazo yangu katika akili yangu yote, ili yaweze kusaidia kwa jamii na yaweze kusaidia serikali, lakini inakuwa halina usimamizi mzuri.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri katika kifungu hiki kwenye ukurasa wa mwanzo kabisa hapa, katika kifungu cha 2(iii) kushukia chini barabara za umma. Ina maana kwa barabara yoyote iliyotajwa katika jadweli moja ya sheria hii ni barabara yoyote ambayo inaweza kupewa na waziri chini ya kifungu cha 3.

Mhe. Spika, tafsiri ni tafsiri na lugha ni lugha. Mheshimiwa mimi nafahamu ukiniambia barabara za umma tayari nimeshakuwa na maswali mengine. Lakini wananchi wanaotusikiliza wanakuwa hawafahamu ukiwaambia ni zipi hizi barabara za umma.

Mhe. Spika, kwanza naomba unipe masahihisho hapa ya kunisaidia. Ni lugha gani hasa ambayo uliyoikusudia hapa, nipe lugha fasaha kabisa ya kuwa huu umma ni wale jamii ambao ndio barabara zao, leo unataka tuwahalalishie kuwaambia kweli kwamba wananchi barabara ni halali yenu kinyume na utaratibu na sheria hii au ni kitu gani hasa Mhe. Waziri ulichokiona wewe hapa. Kwa sababu barabara zimo ndani ya ardhi na ardhi tunaambiwa ni mali ya serikali, na wewe ndiye unayeweka pale barabara.

Mhe. Spika, mimi hapa huwa nazishangaa sana hizi sheria, sijui nani atakuwa ni sahihi. Barabara imo ndani ya ardhi na ardhi yenyewe ambayo inasheria tayari, lakini na yeye mwenyewe waziri anaitungia sheria ndani ya sheria. Naomba ufafanuzi Mhe. Waziri ili niweze kujua vizuri, kwa sababu kila mtu na taaluma yake alivyosoma.

Mhe. Spika, sheria zina upeo wa macho, unapojua wewe hivi na mwenzako anajua kuliko hapo. Naomba Mhe. Waziri, kidogo anisaidie hapa kwa akili yangu ndogo ili niweze kumuhalalishia vifungu vyake. Atakuwepo mjanja katika taratibu kwa makusudi ataharibu ile miundombinu, lakini kwako wewe tayari umeshatunga sheria, lakini atakwenda kutafuta kifungu ambacho kitamlinda yeye katika matumizi ya ardhi ile.

Mhe. Spika, nikiendelea na ukurasa wa 359 hapa anasema jengo maana yake ni ujenzi uliofanyika ukiwa na au bila ya kuwa na paa au ukuta, ikijumuisha msingi, nyumba, viwanda, vibanda na chochote cha maumbile kama hayo.

Mhe. Spika, sawa mimi nakubaliana nalo sina tatizo. Lakini nimuulize atakapokuwa anataka kwenda kulipa si ndio utakaponiambia mzee hapakuwa na nyumba palikuwa na msingi. Kwa hivyo, hebu tutizame maelezo hayo yako sahihi. Mhe. Spika, naomba sana tuangalie kuna mambo ambayo yatatukwaza mbele na sheria nyingi sana ukitizama Mhe. Spika, baadae zinafunga, nafikiria Mhe. Mwanasheria Mkuu yupo, nitakuja kuzifafanua wakati wa kamati teule katika ripoti ya ardhi.

Mhe. Spika, kuna sheria nimeziona katika *label* yangu nitakuja kuzieleza, ili tuone ile hali ambayo imejitokeza, leo siwezi kuzisema hapa. Naamini kwa leo utanipa muda mzuri ili tuendelee vizuri, nashukuru sana kwa hilo, naona umetikisa kichwa hapo.

Mhe. Spika, naomba sana suala hili tuliangalie kwa upeo kabisa, unamaanisha kuniambia kuwa jengo ina maana ujenzi, nimekubaliana nayo, msingi ni ujenzi, kibanda ni ujenzi, hilo sina tatizo nalo nataka uje unifahamishe vizuri.

Mhe. Spika, nikiendelea chini yake hapo kuna kitu kinaitwa machimbo, maana yake ni pahala ambapo kwa kawaida ni tundu. Mhe. Spika, hii maana yake sijui ikoje. Hii tafsiri tundu au shimo ardhini ambamo hutolewa mawe, mchanga, udongo, fusi na nyenzo nyengine inayoweza kuhitajika kwa madhumuni ya kufungua, kutengeneza au kukarabati barabara zozote za umma.

Mhe. Spika, sasa hii niulize ni mali ya nani, kwa sababu mheshimiwa barabara inatakiwa kifusi. Zamani ilikuwa yakipangwa mawe, lakini sasa hivi

ni kifusi na kokoto. Lakini vitu hivi kwa utaratibu wetu vyote vitakuwa vimo katika miliki ya wananchi wenyewe.

Sasa wizara au idara iniambie inapokuwa inataka kufanya shughuli kama hizi, kuna kitu kinaitwa malipo, analipwa nani, au ndio kwa kuwa serikali ikitaka jambo lake, basi iruhusu tu serikali ichukuwe tu, kwa kuwa inataka kufanya jambo la umma na wakati tayari mwananchi yule ameshakubalika kupewa ardhi ile kwa kufanya shughuli zake.

Naomba sana Mhe. Waziri, unisaidie hapa, kwa sababu tayari watu wengi wanalalamika hawalipwi na pengine wanalipwa, lakini tathmini ya kulipwa ile inakuwa ni ndogo sana imepitwa na wakati. Naomba sana Mhe. Waziri, kifungu hicho ukiangalie vizuri, uje unipe jibu zuri ambalo litaweza kuwafanya hawa watu wajielewe sasa hivi kwamba hii haki itakwenda kwa watu wa Idara ya Barabara au watakuwa wanakubaliana. Je watalipwa malipo kwa kupitia mfuko huo kutoka serikalini kwa kuendesha shughuli za umma.

Mhe. Spika, nikishuka chini hapo hapo kifungu kimoja unakiruka. Barabara maana yake ni eneo la wazi au linatumiwa na umma na linaendelezwa kwa ajili ya, au hutumika zaidi kwa kuendesha vyombo vya moto. Mhe. Spika, kwa hapa nimsifu sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri wake wamepata mtaalamu mzuri sana aliyewatengenezea sheria hii.

Kwasababu vitu kama hivi kweli kama vilikuwepo enzi za ukoloni, basi tulikuwa hatuvijui. Mimi nilikuwa sijui kama barabara ni jambo la wazi, kwa sababu nilijua unapotafuta barabara ni lazima ukafyeke, ndivyo ninavyofahamu, kumbe ina maana popote penye uwazi ni barabara tu, si ndio hivyo. Mimi nafikiria Mhe. Spika, labda ufahamu wangu ni mdogo, lakini kutokana na kifungu hiki nimeelewa hivyo.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nitafahamu hivyo, lakini wananchi hawafahamu hivyo. Huu uwazi wenyewe uje kufahamishwa Mhe. Waziri ni wa aina gani, wa sehemu gani ambao unastahiki kwa mujibu wa sheria kutengeneza barabara. Ningeomba sana nisaidiwe fikra hizo, ili tufike pahali twende vizuri.

Mhe. Spika, kuna kitu kimenichanganya akili, lakini inawezekana kuwa huko nyuma sheria ilikuwa ikitumika, neno la balozi mkaazi au wa Uingereza. Mhe. Spika, lilinichanganya sana hili suala. Naomba sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri kama huko nyuma kulikuwa na neno kama hilo, lilikuwa linaelimisha kwa mantiki gani na kwa kuwa sasa hivi hulitaki umegundua kuna sababu gani. Naomba Mhe. Mwanasheria hili suala hebu kidogo tufahamishwe.

Mhe. Spika, sheria sio kitu cha mchezo, ninasema siku zote, sheria tuiangalie kwa upeo kabisa. Naomba suala hilo Mhe. Waziri tuelezwe, leo unasema hulitaki tuweke neno Zanzibar, sawa mimi sina tatizo nalo.

Mhe. Spika, kama nilivyokuambia leo nitakuwa mtaratibu, kwa sababu leo nimegeuza mfumo wa kuchangia, inategemea na miswada yenyewe Mheshimiwa, kila unapokuja mswada inategemea na ile *model*, siku hizi nakwenda na *model* Mhe. Spika. Yote hii ni yako wewe Mhe. Spika, ni *UNDP* hiyo uliyotuletea ikatuelimisha, japo tunapata posho kidogo lakini tunapata mambo mazuri, si haba *Alhamdulillah*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nikiingia katika ukurasa wa 360, Mheshimiwa hapa kinasema kufuta maneno mgawanyo na barabara za umma ziliopo katika maelezo ya pembeni na badala yake kuandika maneno, Waziri anaweza kuzigawa na kuzigawa tena barabara za umma.

Mmh! Mhe. Spika, kinasema kufuta maneno mgawanyo wa barabara za umma, lakini Waziri anaweza kuzigawa na kuzigawa tena barabara za umma. Mhe. Spika, bado ninapata shida na nina wasi wasi sana kama nikasema ipite Mhe. Spika, kumbe ikawa na tafsiri nyengine au nampa Waziri *power* hapa, anaweza hata akasema hapa nyumbani kwa Makame Mshimba inafaa barabara kuu vunja peleka huko, keshaniathiri Mheshimiwa.

Sasa barabara hizo kuu ni za kuamua tu, *feeder roads* tukazibadilisha kuwa ni barabara kuu ni maamuzi tu na zipo, *feeder roads* nyengine ni sawa sawa na barabara kuu. Sasa barabara kuu hizo sijui zimeainishwa kwenye sheria za aina gani humu, Mhe. Spika.

Mhe. Spika, bado mimi nina wasi wasi, mswada mdogo, lakini naona mantiki yake hasa kwenye kichwa changu leo naona haujaingia. Ukiweza Mhe. Spika, niwachie mpaka nimalizie saa 7:00 hapa, kwa sababu kuna vitu ambavyo vinatakiwa kuchanganuliwa kwa taratibu ili wajumbe waweze kupata mawazo mengine ya kuweza kusaidia sheria hii. Nina wasi wasi na tusikurupuke tu kwa kutunga sheria za hapo kwa hapo, tuangalie na ile mantiki ya lugha. Mhe. Spika, lugha nazo ni sheria. Nimepata mashaka makubwa ndani ya mswada huu.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ni mwalimu wangu sana na Naibu Waziri ni mwanasiasa wangu sana, lakini leo hapa mmeniziba macho bado sijaona ndani. Kuja kusema kwamba nitaukubali kwa asilimia mia kwa mia itakuwa ni kitu kigumu.

Tunaendelea Mhe. Spika, na kifungu cha 8(a) kuhusu barabara kuu.

> "Barabara kuu: Barabara ambazo kimsingi huunganisha mikoa miwili au zaidi"

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ukizingatia na muda wako unamalizika baada ya dakika kama tatu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Dakika tatu. *Thank you* Spika. Mhe. Spika, namalizia hapa ndio kabisa sioni kitu. Ananiambia barabara kuu, barabara ambazo kimsingi huunganisha mikoa miwili au zaidi, hizo barabara kuu zenyewe Mheshimiwa, mimi katika Jimbo la Kitope nina barabara moja *feeder road*, lakini kubwa sana, inaweza ikaunganisha barabara hii kuu na barabara nyengine kuu kwa upande mwengine. Je, na hiyo niite barabara kuu kwa kuwa imeunganishwa ndio maana yake Kiswahili kiliopo, imo ndani ya mkoa nayo ile, kwa sababu ni Mkoa wa Kaskazini.

Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Spika, kwa kuwa muda mdogo sana umenipa wa dakika tatu, nimalizie kwenye ukurasa 361 kifungu cha 19(1) kinasema;

Kifungu cha 19(1)

> "Mtu ambaye atakuwa hakuridhika na maamuzi ya idara ya malipo au ya kiwango cha fidia inayotokana na tendo lolote au jambo lolote lililofanywa na idara kwa mujibu wa uwezo wake chini ya kifungu cha 13, atalazimika kupeleka ombi la maandishi kwa taratibu uliowekwa na sheria ya fidia"

Mhe. Spika, suala hili kweli na hao watu wapo huwajafika kwenye nyumba zao. Mhe. Spika, utaratibu huu sijui umeuwekaje kwa mujibu wa sheria. Mimi naamini sasa hivi tuwe na utaratibu wa sheria, usijenge barabara mpaka uwalipe wananchi, naomba sana tuwe na utamaduni huo na tuweke sheria hiyo, kwa sababu tunapofika kujenga barabara, basi wananchi tunakuwa tunawadhalilisha hatuwapi fedha zao na ile barabara sio kwamba hawataki. Lakini sasa na wao wafikiriwe wanalala nje, barabara nyingi kule Bumbwini, Kiombamvua, Kilombero na sehemu nyingi sana hawajalipwa.

Kwa hivyo, naomba hizo nazo tuzitengenezee sheria. Serikali kwanza iwaelimishe wananchi wafahamu halafu wapatiwe fidia za nyumba zao au miti yao baadae ndio barabara zijengwe, vyenginevyo vyovyote tunapoteza muda mpaka leo hii. Hebu Mhe. Waziri, njoo unijibu umewalipa wangapi hasa katika upande wa Kaskazini.

Mhe. Spika, nimalizie. Samahani sana kwa dakika ya mwisho naondoka.

Mhe. Spika, kuna hii vurugumechi ya daladala hazina sehemu maalum katika utumiaji wa barabara, zipo tu zinakaa bila ya utaratibu na kuhatarisha maisha ya watu. Kwa hivyo, ningeomba sana suala hili liangaliwe. Wenzetu nchi za nje Mhe. Spika, nimekwenda katika nchi ya Australia wana sehemu maalum ya eneo la kituo limo ndani ya mji na wanaegesha magari vizuri kwa mujibu wa taratibu. Kama tunaamua hivyo Mhe. Spika, sasa tuwajengee vituo vikuu vya kufikia zile gari na kuweza kubadilisha gari, naomba sana ili tuweze kuwatimizia wananchi na kuondokana na usumbufu huo.

Mhe. Spika, la mwisho, wengi mmetembea nchi za nje huko kina Mhe. Mohammed Aboud Mohammed na kina Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame. Kule wenzetu wana vile vibanda wanakuwa wanalipa ada ya kutumia ile barabara na sisi tujiandae hakuna ubaya si ndio maana ya kutembea nje. Tizama zile barabara zake Mhe. Spika, na wewe mwenyewe umetembea, huwezi kupita katika kile kibanda kama hujalipa ada. Kwa hivyo, na sisi tuwe na taratibu hizo ili kuzifanya barabara zetu ziwe *standard* kabisa.

Lakini leo barabara zetu ziko nusu ya *standard,* nasema *standard,* lakini ziko nusu ya *standard*. Kwa kuwa tunashindwa kupatia mfuko wa kuchangia, sijui kama ipo. Naambiwa sijui *road license,* lakini sioni, ile sio kuchangia, kwa sababu wewe hupati mfuko ule Mhe. Waziri, ungekuwa unaupata mfuko ule Mhe. Waziri, basi naamini barabara zako zingekuwa nzuri.

Mhe. Spika, nakushukuru sana na nasema natamka wazi nina asilimia 50 ya kuukubali mswada huu, vyenginevyo nije kupewa maneno mazuri na Mhe. Waziri, maana yake leo nimekwenda kifungu hadi kifungu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa tukiwa katika hali ya afya njema kwa mustakabali wa kuisaidia serikali yetu.

Mhe. Spika, mimi nimejawa na wasi wasi, kwa sababu haya ni marekebisho na marekebisho haya tumeona mapungufu mengi katika huu mswada. Sasa wasi wasi wangu umenijia kwamba sijui ule mswada wa zamani ukoje. Kama marekebisho ni haya yenye matatizo, basi ninaimani hata huo mswada tungeupata basi tusingelipata mafanikio makubwa sana.

Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Spika. Sasa hivi ni lazima tuwe na *vision* kwa sababu tunakwenda kwa wakati wa sayansi na teknolojia. Kama hatuna *vision*

ya kuangalia huko mbele, basi kwa kweli mambo mengi tutafeli katika shughuli zetu za kitaifa.

Mhe. Spika, wenzangu wamechangia hapa na pale na mimi nitachangia hapa na pale kwa jumla. Lakini nasema kwa nini nikasema tuwe na *vision.* Mhe. Spika, sasa hivi madaladala yetu haya lazima tuyajenge kwa mujibu wa wakati tulionao. Lakini nashangaa saa nyengine utakikuta kidaladala ambacho kupishana na gari nyengine ni shida.

Naiyomba sana serikali, wakati tunapofanya mambo yetu, basi tuangalie na mbele ili kuepuka hasara nyengine kama tuna matumaini ya kuhakikisha kwamba hapa tunataka kuongeza barabara nyengine. Tunapoanza hivi sasa basi tutizame na mbele.

Mhe. Spika, upana wa barabara ambazo zinajengwa sasa hivi nyengine sio za kuridhisha. Lakini pia, niseme tu kwamba na magari yanayopita katika barabara ile, uzito iliyonayo kwa kweli hairidhishi. Naiomba serikali na wizara husika tuwe wakali, tusiseme tu kwenye redio, lakini tuchukue hatua zinazofaa kwamba barabara hii haiwezi kuchukua gari ya tani 20 basi isipite, uchukue kwa mujibu wa tani ya barabara iliyojengwa, hili moja.

Lakini jengine nije kwenye fidia, kwa sababu maendeleo katika nchi ni lazima, lakini maendeleo yale tutizame na wakati. Mimi nitatoa mfano wangu mwenyewe. Kwanza niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kunipelekea barabara Mtambwe, nitoe pongezi za dhati kabisa.

Lakini mimi mwenyewe nimevunjiwa nyumba yangu au sijui kwa sababu ndio nimeonekana kwamba ndio Mheshimiwa nikapewa fidia ya milioni 7. Mhe. Spika, fidia ya milioni 7 nitajenga nyumba kweli niimalize kwa milioni 7 pamoja na kwamba ni kijijini, lakini vifaa tunanunua wapi, mjini. Lakini kwa sababu mimi ni kiongozi nikaichukulia fidia ile ya milioni 7.

Hivi ninavyokwambia Mhe. Spika, nyumba haijamalizika, kwa sababu ni nyumba ya kifemilia, lakini ni nyumba ambayo nimeijenga kwa imani yangu kwa kuwajengea wazee wangu. Mimi mwenyewe hivi sasa imenipata kazi mpya, milioni 7 hufiki popote, pamoja na kwamba nyumba nimeijenga japo niseme milioni 3 au milioni 4, lakini kwa kipindi hiki sasa hivi kwa huko mbele tunavyokwenda na kwa mambo yanavyokuwa, huwezi milioni 7 ukajenga nyumba kijijini.

Niseme hayo tu kwamba tunapotoa fidia tuangalie na wakati ule wa fidia unapotolewa ili mwananchi yule aliyekuwa mwengine ni masikini ya Mungu

kajenga kibanda chake ahakikishe anapigiwa hodi. Asihakikishe kwa pesa ile aliyopewa kwamba mlango uwe wa gunia, tumeshatoka huko Mhe. Spika.

Mhe. Spika, suala la matuta, sijui kama mnaita matuta au mnaita sijui nini. Kwa kweli kuna mtindo wa vijiji vyengine kujijengea matuta si ya kiwango yanayotakiwa. Naiomba wizara iliangalie suala hili mwisho ndio nitakuja kutoa ushauri wangu.

Lakini jengine niseme Mhe. Spika, na mimi nitilie mkazo Wizara ya Mawasiliano ishirikiane na Baraza la Mji, kuhakikisha kwamba vurugu ambalo lipo hivi sasa katika mambo ya maegesho ya gari kwa kweli walitatue haraka. Wakae pamoja, wakubaliane kwani tunawapa shida kubwa sana wananchi wetu.

Ukipita humo njiani wewe mwenyewe utaona huruma jinsi wananchi wanavyopata shida. Mtu akitoka masafa ambayo anatarajia akiteremka hapa atapanda hapa afike kwake, lakini haiwezekani na Wazanzibari asili yetu ni twike kama nilivyosema asubuhi hapa. Twike nikaulizwa nini. Twike ni mizigo, akitoka Makunduchi mtu anatwike, huyo Mpemba ndiyo mama yangu weee! haisemeki twike alizonazo.

Hizo ndizo mila zetu tokea huko nyuma tulizonazo, unatoka unakwenda, mie leo nakwenda kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nichukue masheli sheli japo mawili na nazi zangu tano, nampelekea mwanangu Ismail Jussa Ladhu. Huwezi ukamkuta Mzanzibari anapunga mkono kama anakwenda kucheza bomu. Safari yoyote lazima awe na kitu.

Kwa hivyo, naiomba Wizara husika pamoja na Manispaa warudie tena vikao vyao wahakikishe wanapanga ruti ambazo wanaona wananchi wetu hawatosumbuka. Wananchi wetu kwa kweli wanasumbuka. Na mimi niunge mkono takriban humu sisi sote tumetembea kwenda nje, tunaona jinsi wenzetu wanavyopanga mipango yao.

Wewe kabla hujamuondolea mtu kile ambacho amekizoea, basi mtafutie pengine ili akiondoka pale apate pengine ambapo na hapo hapatotoa usumbufu. Naomba hilo Mhe. Spika, bado mjini nafasi tunazo za kuweka maegesho yetu na wananchi wetu wakaridhika kuhakikisha kwamba hawatopata shida ambazo wanazipata sasa hivi.

Mhe. Spika, nilisema kwamba mwisho nitoe ushauri. Natoa ushauri kwa wizara husika ni vizuri tukatathmini, tukazunguka, tukaacha tuliyonayo, tukaangalia ni Mkoa gani na Wilaya gani kunatakiwa nini, kunatakiwa barabara ya kilomita ngapi, kunatakiwa barabara ya kiasi gani na wananchi

hawapati shida ili kuondoa usumbufu ambao unawaletea shida wananchi pamoja na ajali zinazotokea mara kwa mara.

Mhe. Spika, ukitoka hii njia ya Mwanakwerekwe kwa kweli ni hatari tupu. Kama serikali inataka kuijenga njia ile basi ifanye tathmini kwanza na upana wake kwanza. Kwa sababu tusijidanganye Mhe. Spika, tunakotoka kweli tulikuwa hatuna njia, Muingereza alituwekea njia zake kwa kutuhesabia kwamba nikiondoka mimi nikikaa miaka miwili mitatu njia zimekufa na kweli.

Lakini tuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada kubwa ambayo imefanya kwa kutujengea barabara kwa wingi, hilo tunalishukuru. Lakini sasa, je, tufanye utafiti mwengine ili kuhakikisha zile barabara tunazozijenga tutizame na mbele tunakokwenda.

Pia, naiomba sana serikali, kwa sababu sasa hivi ajali za baskeli na ajali za vespa ni nyingi mno. Na watoto wetu hawa wadogo kuanzia miaka 7, 8 ,10 na 12 tumewapa raha na wao waendeshe baskeli, lakini matokeo yake ajali ni kubwa. Kwa nini hatuendi na *vision* tukaweka magari upande huu na baskeli pamoja na vespa upande mwengine ili tukaepukana na ajali hizi, Mwenyezi Mungu atuepushie mbali, ikawa wakigongana kwenye magari tena itakuwa wametaka wao wenyewe.

Mhe. Spika, la mwisho, naiomba wizara hii kwamba kuna mambo mengine madogo madogo tunayaona, lakini ni makubwa kwa kusimama gari inapotaka wenyewe. Gari ikiona hapa isimame baada ya kumuona abiria anamgongea mara gari inasimama. Ikenda mbele kidogo gari inagongwa tena na utingo gari inasimama.

Na saa nyengine maana sijui niseme daladala zimelaaniwa ulimwengu mzima, mtindo wao huo hata ukenda nchi za nje daladala ndivyo zilivyo. Daladala lazima zitafanya yale mambo yake ya kidaladala. Unaweza ukashtukia gari inakufuata wewe mwenyewe huna habari na saa nyengine si tumetia kugawa hizi daladala mstari mweupe, basi anaweza akakupitia hata upande ambao sio, unashtukia tu daladala vuuu wanafukuzana.

Mimi nadhani tathmini moja wapo niliyoisoma kwamba vituo tuvijenge upya vya usimamiaji wa magari. Na wenzetu hawa askari wa *trafic* tukishakuwa wakali maana udongo upatize ungali maji, lakini hiyo rushwa imekithiri Mhe. Spika. Mtu anaweza akasimama hapo wakati gari kaliona, sisi kule Pemba kulikuwa kuna gari tukiliita mbirimbi, maana ilikuwa haijai hiyo. Maana m-birimbi ukizaa unaujua hauna kiwango, unazaa tu. Basi na hiyo gari ilikuwa

inaitwa mbirimbi, ikitoka Wete imejaa watu tele mpaka wengine wananing'inia na wengine wanapandishwa juu.

Sasa mimi nazungumza kwanza tukemee rushwa. Pili, tuwaombe wenzetu askari wa *trafic* waangalie vizuri ili kulinda mustakbali wa wananchi wetu. Kwa sababu unapomruhusu mtu kupakia si kiwango cha gari inavyotakiwa ni kuhatarisha maisha ya wananchi.

Baada ya kusema hayo kwa sababu nimesema tufanye utafiti na turekebishe baadhi ya mambo yetu, sasa kama sikuunga mkono huu Mswada nitakuwa sijafanya lolote. Kwa sababu mimi kuna mambo nataka yarekebishwe tena nikisema mimi siungi mkono, sitoeleweka. Kwa hivyo, niseme tu naunga mkono Mswada huu mia juu ya mia ili tuweze kurekebisha yale matakwa kwa wananchi wetu.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Mawasiliano na Uchukuzi. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kutufikisha hapa tukiwa salama kwa pamoja sote na kuweza kuchangia Miswada iliyokuwepo mbele yetu kwa wakati na ufafanuzi mzuri.

Mhe. Spika, kwa kweli na mimi naungana na wenzangu kuweza kuchangia Mswada huu hasa kifungu cha 1 kuhusu matatizo ambayo yanakabili barabara zetu pamoja na usafiri wa nchi kavu. Kwa kweli tuna matatizo mengi sana ambayo hivi sasa ipo haja kuyatanzua hasa kwa vile tunahisabu nusu karne imeshafika. Ni vyema turekebishe matatizo yetu ili tuweze kuanza tena awamu nyengine ya kuweza kufatilia masuala muhimu.

Mhe. Spika, ikiwa muda mrefu tunalalamikia barabara kwamba mpaka leo kuna barabara ambazo hasijajengwa na hata kuanzwa. Hili jambo linasikitisha sana. Iko haja ya kuyapitisha yote yaliyoombwa yapitishwe, lakini kwanza mengine ni lazima yatanzuliwe ili tuendelee kuweza kuhakikisha kwamba tunakwenda na wakati.

Tukitizama hivi sasa tuna barabara nyingi ambazo zinajengwa. Lakini utakuta wananchi wengi wanalalamika kuhusu mazao yao hayashughulikiwi ili kupata fedha za fidia kutokana na mazao yao.

Pia, kuhusu vibanda vyetu ambavyo tumejenga maeneo ya zamani ambayo yalikuwa sio maeneo ya barabara, lakini sasa hivi barabara inataka kupitishwa. Ni vyema wananchi wafikiriwe kwamba wanahitaji kupatiwa fidia za mashamba yao na vibanda

vyao ambavyo walivipatia tabu sana kuyahuisha na kuweza kuhamishwa sehemu ile na kuanza kwengine maisha mapya sehemu nyengine.

Kama mimi katika jimbo langu la Koani nina mategemeo ya kupata barabara nzuri ambayo ya kutokea Pongwe hadi Jumbi ambayo inaanzishwa hivi sasa. Lakini vilio vya wananchi wetu ni vikubwa sana na huwa wanatuletea malalamiko ili kuweza kuyafikisha kwa Waziri. Lakini utakuta hadi hivi sasa hatua zilizochukuliwa kutokana na malalamiko hayo. Utakuta hivi sasa barabara zimekwama na wananchi wamekubali bora wafe, lakini nawaondoki katika sehemu ambazo hawajalipiwa fidia zao.

Hilo linakuwa sisi Wawakilishi wa majimbo linatupa mzigo mkubwa ili wananchi wetu kuweza kutukubali kwamba tunayafuatilia masuala yao. Tunamuomba Waziri aje ahakikishe kwamba anatoa fidia kama alivyokubali mwenyewe na akaweza kuweka msururu wa watu kwamba huyu nitamlipa hichi na huyu nitamlipa hichi, ingawa ni kidogo, lakini watu walikubali. Lakini leo utakuta hata hicho kidogo wananchi imeshindikana kulipwa.

Mhe. Spika, kwa kweli utakuta mwananchi mwengine ana nyumba yake, lakini si kubwa kiasi hicho, lakini ana watoto 12. Watoto kama hao anapata shilingi milioni moja au laki tano, ndio anaambiwa akaanze maisha mapya kwa kuwa kibanda chako kilikuwa si kizuri ni kibanda cha *full suit*, lakini mwenyewe kwa wakati ule kilikuwa kinamridhisha na wakati ule alikuwa na uwezo wa kukaa na watoto wake 12, alikuwa anakata *partition* humo humo ndani kwa ndani ingawa za makuti.

Lakini leo kweli unamuhamisha akaanze kujenga nyumba popote atakapokwenda kununua kiwanja tu inaanzia milioni 5 na kuendelea. Yeye unampa laki 5 sijui unamsaidia nini mwananchi yule. Kwa kweli naomba Mhe. Waziri, hilo aliangalie sana kwamba anatupa majukumu wakubwa, makubwa sana sisi Wawakilishi wa Majimbo huko majimboni kwetu.

Mhe. Spika, utakuta hivi sasa Mwera/Pongwe wananchi wengi hawajalipwa fidia. Na nimeshaonana na Waziri na Naibu Waziri, lakini anakujibu nyumba yake ile hata Pongwe hakai. Ndiyo lakini ni yake, ni lazima apewe fidia zake ili anapokwenda mwenyewe kama pesa ile atakwenda kulewea pombe au atajenga, lakini alipwe kutokana na uwezo wa majenzi yale.

Vile vile, ningelipendekeza kwa serikali inapoanza kuvunja nyumba za wananchi itushirikishe na sisi Wawakilishi wa majimbo ili mwananchi anapokuja kutoa lalamiko iwe mimi ni shahidi tosha kwamba nilikuwepo wakati unaambiwa kwamba faini hapa na fidia utalipwa. Ili niwe shahidi kwa upande wa serikali na wananchi pamoja. Lakini utakuta wananchi wetu

ametilishwa saini kwamba waondoke na yeye ameambiwa tu tia saini kabla hawajatiliwa idadi ya pesa ambazo atalipwa.

Jambo hili kwa kweli limeleta matatizo makubwa sana kwa wananchi wetu, kwamba fidia iliotolewa ni ndogo na sio aliyokubali mwenyewe na ukitizama sasa hivi unaona saini yake, lakini pesa zimetiwa baada ya yeye ameshasaini. Wananchi wengi hivi sasa wanatoa malalamiko na sisi tukioneshwa ile karatasi tunamwambia mwananchi saini yako nimefatilia, nimeikuta na kweli pana shilingi laki tano.

Mwananchi anasema mimi nimetia saini lakini palikuwa hapajaandikwa hata shilingi moja. Niliambiwa utaondoka hapa na nimekubali, kwamba nitaondoka, lakini pesa walizozifanyia makisio serikali bila ya hata kujua mwananchi yule kwamba atalipwa kiasi gani. Lakini kama tutashirikishwa wawakilishi wa majimbo itakuwa ni ushahidi tosha kwa wananchi na kwa upande wa serikali.

Mhe. Spika, nije upande wa usafiri juu ya wananchi wetu. Kwa kweli kuna matatizo makubwa sana kutokana na upande wa usafiri wa nchi kavu. Kuna vijiji vyangu hivi sasa vina miaka hamsini utakuta kijiji hicho hata Waziri mwenyewe hajui kama kuna kijiji na hata ukimfahamisha anakwambia kijiji kile si tumeshatengeneza, lakini ukimwambia nenda Mkorogo, hapajui Mkorogo ni wapi. Hakuna namba ya gari hata moja, sijui wananchi wale wanafika fikaje, wanatumia magari ya ng'ombe na magari ya punda hata wanapoumwa kwenda hospitali, gari hazifiki.

Mvua kama hivi sasa ukienda Mkorogo kama utaondoka asubuhi mjini utafika saa 10 hujafika unapokwenda. Kwa kweli kama unatoa mgonjwa Mkorogo kumpeleka hospitali, wengi wao wanafia njiani kwa sababu hakuna usafiri. Ukimkuta mwenye daladala anakwenda Tunguu au anakwenda Chuo Kikuu ukimwambia naomba ukanichukulie mgonjwa wangu Mkorogo anakwambia Mkorogo hakwendeki, hata ile gari ya namba ya Mkorogo hamna.

Hili ni tatizo kubwa sana kwa Waziri kutokujali ama kutumia mbinu ya kuweza kutembea katika vijiji akajua vijiji vyake ni vingapi vyenye matatizo au ni vijiji vingapi vinahitaji vipate barabara hata ya fusi.Utakuwa wananchi wengi wanamlalamikia Mwakilishi au Mbunge au Diwani, kwamba hawatii kifusi, lakini kumbe serikali ipo inayohusika zaidi.

Barabara ya Mkorogo ni barabara kubwa kwa sababu kuna kijiji, lakini Waziri hapajui ni wapi. Utakuta kuna mji mwengine unaitwa Mjonga iko Unguja, lakini mwambie Waziri nipeleke Mjonga hata umpe dola mia tano,

hapajui Mjonga ni wapi. Wakati Mjonga ndipo panapotoka mazao mengi hasa machungwa na mapapai ambayo yanastahiki kufika katika soko, lakini yanashindikana kufika katika soko kwa sababu hakuna barabara ambayo inapitika kwa gari, hata namba ya gari ya kufika huko hakuna.

Huko kote kunamngoja Mwakilishi, Mbunge aweke barabara ya fusi. Utakuta pesa anayopata mwakilishi huyo hata kunawa uso kwa hapo Mjonga haisaidii kitu.

Namsisitiza Mhe. Waziri, katika Mswada wake huu tunaupitisha, lakini ajali sana kwamba wananchi wetu hivi sasa wanahitimisha miaka 50 ya Uhuru, kwa kweli isiwe kama ndio wanapigania uhuru hivi sasa. Kupigania uhuru ni mahali ambapo hakuna usafiri, hakuna hospitali na utakuta Mkorogo hakuna Skuli, hakuna hospitali, utakuja Mjonga hakuna hospitali hakuna skuli, kwa kweli wananchi wa huko wanadhalilika sana.

Tukienda tunahamasisha sana wananchi wetu kwamba tutafanikisha, lakini maneno matupu. Watu wanasema "Mkono mtupu haurambwi" Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, napenda sana kumsaidia Waziri wangu kuhakikisha kwamba Mswada wake tunauunga mkono na unapita, lakini ajali sana kwamba afanye mwenyewe miundombinu kama lilivyo jina la kazi yake, miundombinu ya kuweza kutembelea shehia ambazo kuna haja kwamba azijue kwamba hakuna barabara na hakuna usafiri na hivyo ni vitu vikubwa sana barabara na usafiri.

Hiyo ni tosha kwamba kujitawala nchi yoyote kuwa na vitu hivi. Unamsikia Rais wetu sasa hivi Mhe. Kikwete, ametangaza kwamba wakati wanaondoka Waingereza nchi hii ina barabara saba tu, lakini sasa hivi Tanzania nzima unaweza ukaitembea kwa siku moja. Hiyo ni tosha kwamba wenzetu wamepiga hatua kwamba wanajali sana muundo wa barabara.

Hivi sasa tuna miaka 50 tunajenga mambo makubwa sana ya historia, tunaweka mnara wa historia wa miaka 50 ni jambo ambalo tulitegemea haitowezekana. Iweje tushindwe kuweka daraja la Uzi Ng'ambwa tukahakikisha kwamba linafanana na daraja la Mkapa la kule Mtwara. Utakuta daraja letu halichukui maili nyingi kama lilivyokuwa daraja lile la Mtwara. Lakini wananchi wa kule wenzetu wa Tanzania hii hii wanafaidika, leo mwananchi wa Uzi Ng'ambwa anapoumwa kwa kweli utasema majanga.

Maana hujui umfikishe vipi hospitalini ama umsaidie vipi. Daraja la kutoka Unguja Ukuu pale ambapo kufika Uzi halichukui hata maili mbili, lakini iweje serikali ishindwe miaka 50 kuhakikisha wananchi wanapatiwa daraja la kileo na wakafaidika na uhuru wao na wao wakajijua kama wamegomboka.

Maana nchi yetu tangu mkoloni Uzi Ng'ambwa hakuna barabara, lakini kuja Chama cha Mapinduzi kimeweza kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika na wanasherehekea miaka 50.

Mhe. Waziri, naomba alichukue hilo kwamba tukimaliza bajeti hii tuhakikishe kwamba ananichukua mimi tunafuatana kwenda Uzi Ng'ambwa kumuonesha kutoka Makime ambako ni sehemu ya Ungujaukuu hadi Uzi kama ulivyopita umeme na tukaweza kufikisha Uzi Ng'ambwa umeme na nikaweza kumuonesha kwamba gharama ndogo linaweza likaingia daraja kutoka Makime hadi Uzi Ng'ambwa wananchi wakafaidika na wakatembeleana kila wakati.

Lakini leo Mwananchi wa Uzi siku ya maji anaambiwa bwana kumetokea sherehe Unguja Ukuu au imetokea sherehe mjini anakwambia nnaitaka nikaiyone sherehe, lakini leo maji hakupitiki. Zanzibar hii hii kweli kuna mahala ambako kusipitike kwenda kuona mwananchi sherehe ya miaka 50. Lakini anashindwa wakati wa kurudi atashindwa kuingia katika kijiji chake maana maji yatakuwa yameshajua na atakuwa mgeni wa nani pale Ungujaukuu.

Namsisitiza sana Mhe. Waziri, ahakikishe miaka 50 analipanda daraja na Uzi Ng'ambwa, kikao chengine tukija hapa 2015 tuhakikishe kwamba tunasema kwamba 2010 - 2015 tumefanya makubwa.

Mhe. Spika, kwa kweli barabara zetu zina matatizo, Mhe. Hayati Mzee Karume alihakikisha kwamba kujenga kambi za wanajeshi katika Zanzibar na kambi ya kwanza kujengwa Zanzibar ilikuwa Ubago. Kwa kweli Mheshimiwa barabara ya Ubago imejengwa tangu 1964 barabara hiyo mpaka leo haijafanyiwa matengenezo. Na kwa kweli jeshi linahitaji kuondoka katika sehemu iliyopo kwenda sehemu nyengine isichukuwe dakika tano.

Lakini kutoka Ubago hata ujiunge na barabara kuu ya mjini kutoka ndani ya kambi ufike barabara kuu ya Chwaka au Uroa, barabara hiyo inachukua masaa mawili kama kweli gari za kijeshi zimebeba vyombo vya hatari au vimebeba mirupuko inaenda hata iko sehemu wanashuka gari ipige moto isukumwe na wanajeshi ili miripuko isije kuripuka. Kwa sababu kuna mashimo matupu na utawaonea huruma mpaka wananchi wenyewe wanashiriki kuzibeba gari za wanajeshi ili zifike salama katika maeneo ambayo yaliyopangiwa.

Kwa kweli nilikwenda na mwenyewe Waziri kwenda kuhakikisha na Mkuu wa Jeshi wa kambi ya Ubago akachukua hatua kwamba hatochukua hata miezi mitatu barabara hii ataitengeneza, sasa hivi ina miezi 6 barabara ile

haijafanywa chochote. Ninamshauri Waziri kwamba ahadi zake ziwe za kweli tuweze kumchagua 2015.

Kwa kweli Mhe. Spika, utaona hali ya barabara ni mbaya na zote nimesisitiza kwamba zifanyiwe matengenezo na nyengine ziwepo barabara Mkorogo, Mjonga na sehemu nyengine zisaidiwe ili nao wananchi wajikute wako huru.

Vile vile, Mhe. Spika, naungana na wenzangu kuhusu tatizo la daladala, kwa kweli wengi sana Waheshimiwa wanapozungumza kuzungumzia mambo ya nje huona kama wanatu-*joke* sisi wengine tunaokwenda Pemba na tunaokwenda Dar es Salaam, wasitujejee, lakini na sisi wengine tumeshafika nje hata kwa njia nyengine zozote zile, lakini tumefika. Mimi mwenyewe nimefika Swizerland, Swizerland kwa kweli hamna daladala, Swizerland wanatumia sana *train*, lakini *train* inakwenda kwa wakati ni kama daladala hapa kwetu, pale ikifika inachukua dakika tano, kengele inalia kisha *train* inaondoka inakwenda kituo chengine.

Nimetembea Dar es Salaam ambao Tanzania Bara mahala kusiko hasara nilikuta Kariakoo zamani palikuwa kuna zogo sana za daladala na pana uchafu mwigi sana. Lakini juzi nilikwenda pale Kariakoo nilishangaa nilisema niko Ulaya au niko Tanzania. Kwa kweli sijaona daladala hata moja, sikuona pale pana zogo la uchafu, nikasema labda hapa Kariakoo nikazunguka Msimbazi nilikuta daladala ziko njiani kama zilivyokuwa Zanzibar zinapita na zinaondoka kwa *time*, hakuna msongomano wa watu pale.

Na sisi Zanzibar tusifikiri tulipofika kwamba tuwe sijui nchi ya mwisho, sisi sasa tunakwenda na wakati, kwa kweli tunaondoka tulipo tunasonga mbele tunafukuzia waliko wenzetu, tusiwe kama hatutembei tukaona kwamba tutaona Darajani tu, tutaona barabara za Mnazimmoja zinapokaa daladala.

Kwa kweli ulimwengu mzima sasa hakuna *park* ya daladala, *park* zinaficha daladala zinaweka na kuondoka, isipokuwa tusisitize kwamba daladala zisiweke msongomano zikifika zinachukua abiria zinaondoka, kapata njiani ndio hakupata sawa. Tukisema zikae Darajani wenye daladala si kweli kwamba *park* zote tukikaa sisi tunalipa, kwa kweli Darajani akishalipa daladala mara moja anajiona kama ndio kalipa kwa siku, ikiingia mara kumi daladala hana uwezo wa kulipa mara kumi.

Na ukiingia pale unatakiwa ulipe, lakini sasa wamesaidiwa kwamba zinapita daladala katika njia za kawaida kama nchi zilizoendelea ni kama hiyo nchi niliyoiona mimi huko Switzerland, Tanzania Bara na pengine Uganda ambako nimefika tumeona mote hamna daladala ambazo zinaweka *park*. Daladala

kazi yake ni kupita kama zinavyopita *train* pana abiria inachukua, hakuna zinakwenda kwengine kuelekea mjini na kutoka mjini kwenda katikati ya mji.

Si kweli kwamba tuhakikishe tunaweka *park* ya daladala tutakuwa hatufiki tunakokwenda, tutakuwa siku zote Zanzibar haina maendeleo. Sasa tunakwenda na wakati ndio tukaona tunajenga mnara wa kisasa kama tunavyokwenda na nchi hizi.

Kwa kweli mimi naunga mkono Mhe. Waziri pamoja na Ofisi ya Baraza la Mji kuhakikisha kwamba daladala hakuna *park,* daladala zipite na zichukuwe watu na kuondoka sio ku-*park* daladala kuweka zogo na uchafu. Leo ukenda Darajani yale mazoea kwamba pananuka, watalii hawendi, ajabu sana hukuti harufu, mimi mwenyewe napita mule kwenye majaa ninawauliza mmetumia nini, akili gani wanasema akili kubwa tuliotumia ni kuondosha msongomano wa daladala. Kwa sababu ilikuwa taka zinanuka, watu wengine wanakuja wanatoka shambani hawakogi wananuka.

Kwa hivyo, ilikuwa wazi kwamba msongomano Darajani ukenda samaki wote wananuka, ikawa Darajani hapana sifa ya kileo. Lakini kwa kweli sasa Darajani ni mahala sawa sawa na Ulaya yoyote ambayo inayofanana na Darajani. Hiyo ndio kukua kwa nchi na kusema sasa Zanzibar tumepiga hatua na tukaweza kuwa na mnara wa miaka 50.

Kwa kweli naomba wenzangu wakubaliane na hilo kwamba tusirudi tulikotoka, twende mbele kama walivyopanga marais wetu na sio kwamba wapange marais tu, lakini na sisi Waheshimiwa ambao tumo kwenye nyumba hii sasa ya Baraza ina maana tuisaidie serikali, sio serikali inapanga mambo yake mazuri kwenda mbele sisi tunairejesha nyuma, tukijihesabu tunakwenda wapi. Sisi tunasema kwamba serikali ikisema suala, sisi tuikazanie na tuijengee hoja kwamba ilivyofanya ndio.

Mimi mwenyewe nimeshakaa Darajani kupitisha daladala, daladala zilikuwa zinasimama katika mzunguko pale Makao Makuu ya Chama Kisiwandui, zinasimama. Mimi nilisaidiana na *traffic* kuzipitisha pale, sema tu *traffic* wetu wapunguze rushwa, wapunguze kuzungumza na watu wa daladala. Pale wamekwenda kazini kwa muda ambao yupo pale hatakiwi kuwa rafiki na mtu wa daladala, apite mwenye daladala aende sehemu inayotakiwa. Sio yeye anazungumza kwamba jana hukunilipa. Sehemu ya daladala haitakiwi mazungumzo. Hata mimi nikimkuta *traffic* anazungumza na mtu wa daladala katika eneo lile nitamchukulia hatua.

Kwa kweli Mhe. Spika, kwa leo nimechangia sana mswada huu kwa kumtaka Mhe. Waziri aendelee na mswada wake mimi na wananchi wangu wa Koani tunaunga mkono mswada huu upite mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwanza sina budi awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehma na mwingi wa utukufu aliyenijaalia adhuhuri hii na hidaya yake ya uzima na afya njema na akanipa uwezo wa kusimama hapa katika kuendeleza majukumu yetu ya kitaifa.

Mheshimiwa na wewe ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kwa kuweza kutoa mchango mdogo sana katika marekebisho ya sheria hii. Mhe. Spika, kwanza naomba nitoe masikitiko yangu makubwa kuhusiana na marekebisho haya tunayoletewa hapa, kitu ambacho kinyume na makubaliano tuliokubaliana. Tuliomba kuwa tutakapoletewa marekebisho ya sheria basi angalau isitolewe sheria nzima, lakini tuletewe vile vifungu ambavyo havikuwepo, madhumuni yake na sababu ya kuondoshwa kile kifungu ili na sisi tuliokuwa hatuna uzoefu huu basi tupate angalau la kusema.

Na Mhe. Waziri, huyu ninakumbuka aliwahi kuleta marekebisho yake ya sheria hapa, hakutuletea hivi, atuletee hivyo tulivyotaka. Lakini sasa leo ninasikitika kuona kuwa badala ya kuanza yale mazuri sasa hivi karudi kwenye mpango ule ule uliokuwepo wa zamani.

Mhe. Spika, Waziri wa Katiba na Sheria alituletea marekebisho tena mswada mkubwa mno uliokuwa tangu koloni za Kiingereza na marekebisho yake yalikuwa madogo tu, lakini alijaribu kuutoa mswada huo Wajumbe wote wakapatiwa mswada mzima tangu nyuma ulivyokua. Lakini sasa wengine kila kitu ni uzito, usilete huo mzima basi hata haya marekebisho vile tulivyokubaliana hatuletewi.

Mhe. Spika, badala ya masikitiko yangu hayo tunawaomba mawaziri wengine watufanyie vile tunavyotaka. Mimi nilikwenda katika Tume hii ya marekebisho ya sheria nikawauliza na wakasema mpango wanauweka wa kuleta marekebisho ya sheria ndani ya Baraza hili hili, lakini Mhe. Spika, haufuatwi. Kwa hivyo, tunaomba tufanyiwe vile ambavyo kuwa na wengine watatupa uwezo wa kuweza kuchangia miswada hiyo.

Mhe. Spika, nianze kwenye madhumuni na sababu ya Idara ya Wizara hii ya kuleta marekebisho haya, wanasema hapa kuwa Idara ya Barabara imeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kuondokana na kuwa vifungu vingi vya sheria ya barabara ya sura ya 134 vimepitwa na wakati na haviendani na hali halisi ya sasa ya mabadiliko ya ufanyaji wa kazi. Kwanza

niwashukuru kwa kuliona hili nadhani badala ya marekebisho haya shughuli zao labda zitakwenda kwa ufanisi au vile wanavyokusudia.

Mhe. Spika, mimi kwa kuchangia nina mambo yangu mawili, kuna kifungu kimoja ambacho kuwa kimeongezwa hicho, kifungu cha 25, nyongeza kifungu kipya cha 30(a) uhifadhi wa mazingira. Naomba nikinukuu Mhe. Spika, amesema "mamlaka ya barabara inayokabidhiwa uendelezaji uongozi wa utengenezaji barabara za umma chini ya dhamana yake itafuata miongozo, taratibu au sheria zilizowekwa kuhusiana na uhifadhi wa mazingira na utupaji taka" Mheshimiwa hili ni jambo zuri, kifungu hiki kuongezwa na mimi nakiunga mkono, lakini huo uhifadhi wa mazingira unaonekana hapa ni utupaji wa taka.

Mhe. Spika, tuna matatizo kidogo hapa tunaloliona ni lakutupa taka lakini, je, ndio mazingira ambayo kuwa yanatukabili haya tu. Kwa upande wa binaadamu hakuna mazingira yanayotukabili ya kiafya ya kibinaadam, Mhe. Spika, naomba nimueleze Mhe. Waziri kama kwanza kuna Kampuni ambazo kuwa zinajenga njia kwa muda mrefu, ule nao pia ni uchafuzi wa mazingira halafu pia afya za binaadamu zinakosekana katika mazingira yale.

Mheshimiwa siku zote tunapiga kelele hapa kuhusu barabara ya Wete-Konde na Wete-Gando ni barabara zinazojengwa kwa muda mrefu wala hawazungumziwi binaadamu wale wanavyoathirika kule, hawazungumziwi hata kidogo, wala wananchi wale hawawajali wanavyoathirika, Mhe. Spika, wewe kuingia ile gari Konde siku moja muda tu wa masaa ukaingia pale mpaka ukafika pale Wete, basi zile nguo unazovaa hazitamaniki. Hebu je, mfikirie yule kondakta anayefanya kazi katika mazingira yale haujawa uharibifu wa mazingira ya binaadamu hayo.

Sasa Mhe. Spika, atwambie Mhe. Waziri kuwa katika uharibifu huu wanaoutaja wao wa taka hawa binaadamu watachukua hatua gani. Maana ninahakikisha madereva wale na makondakta wanaofanya kazi katika njia ile si wazima, hawana uzima na wala hawajaliwi na serikali wala chochote wao wamo ndani ya kutafuta riziki, lakini serikali bado haiwajali.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri anieleze hii sheria katika mazingira hayo kampuni zinazotengeneza barabara katika miaka 10 hii, sheria inasemaje kwa sababu hatuijui maana hiyo kongwe hatuijuwi, sasa marekebisho haya mimi sijaiona hebu anieleze inasemaje, ni utaratibu gani ambao mnauweka kwa kampuni zile kuchukua tenda zile za kutengeneza barabara badala yake wakakaa muda mrefu na hatimaye kutuingizia wananchi wetu maradhi au sote kwa jumla, hasa sisi watu wa vijijini. Hilo ni moja Mhe. Spika.

Lakini jengine ambalo nataka nilizungumze ni Kampuni hizo hizo zinazopewa ujengaji wa barabara anieleze na wao anawapangia utaratibu gani, kupitisha magari ya tani kubwa ndani ya barabara, halafu barabara zile zikaanza kuchimbuka kwa muda mchache tu. Mhe. Spika, hili ni tatizo kwani zile Kampuni hadi zije na magari yao namna ile ambayo barabara zetu hazina uwezo wa kuchukua tani zile za magari.

Mhe. Waziri, atueleze sheria inasemaje na hatua zitakuaje dhidi ya magari yale yanayochukua vifusi yakipita kwenye barabara mbovu, barabara zinazojengwa kwa gharama halafu hatimae siku mbili tatu barabara zile zikachafuka. Mhe. hili utueleze sheria inasemaje, lakini kuna utaratibu gani, lakini na nyinyi kama serikali juu ya hili mnachukua hatua gani.

Barabara zote Mhe. Spika, sasa hivi ni mbovu kwa kupitishwa magari *Mecco*, kwani gari zenye uwezo wa kupitisha hazipo kule Pemba, wao ni kuja watengeneze njia wapelekewe hilo fusi, hamuwezi kutafuta magari mengine mkawaajiri watu wakafanya kazi. Sasa kuna mambo ambayo kuwa serikali hayazingatii kuwa huku wanatengeneza, lakini huku wanabomoa. Sasa hii sheria ituambie kuwa sheria hii inasemaje kuhusu matatizo hayo yanayojitokeza ndani ya ujengaji wa barabara hii.

Mhe. Spika, mimi sina mchango mkubwa isipokuwa yangu ni hayo, lakini ninamuomba Mhe. Waziri, masuala haya yangu mawili anieleze ili niweze kuunga mkono marekebisho haya ya sheria. Kwanza ujenzi wa barabara hizi mbili hatua itakuaje, siku zishakuwa nyingi, mimi ninahakikisha wananchi wetu pale wameshaathirika kutokana na hali ile ya mavumbi migomba inakuja iweje binaadamu.

Mhe. Spika, baada ya hayo siungi mkono mpaka nitakapopatiwa maelekezo ya maelezo yangu niliyoyatoa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mswada huu naomba nitoe mawazo yangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani, kumsaidia Mhe. Waziri katika kuweka vyema sheria hii, Mhe. Spika, nia ya sheria ni nzuri, lakini natangulia kusema kwamba nina wasiwasi kwamba sheria hii haitekelezeki. Imeshindwa hiyo kongwe ya ukoloni, lakini na hii mpya ya awamu ya saba ya Mapinduzi Zanzibar nina hakika haitotekelezeka.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu nione mna vifungu ambavyo serikali wamesahau kwa sababu walijisahau zamani sana na leo wanakusudia kwenda na wakati jambo ambalo haliwezekani.

Mhe. Spika, serikali imetuletea sheria hii wakiwa wamesahau kwamba kuna *Zanzibar Transport Master Plan* ambayo ilipitishwa tangu 2006/2007, lakini hawajawahi kuichukulia hatua kuitekeleza. Mpangilio ule wa usafiri Zanzibar upo, lakini nina hakika kwamba hawajawahi kufikiria kwamba huu ni mpango kwa ajili ya kuchukuliwa hatua. Sasa nina wasiwasi kwamba sheria hii imekuja kama sheria nyengine, lakini sioni utekelezaji wake.

Sasa Mhe. Spika, nianze kwenye tafsiri kuna neno machimbo maana yake ni pahala ambapo kwa kawaida ni tundu au shimo ardhini ambalo hutolewa mawe, mchanga, udongo, fusi au nyenzo nyengine inayoweza kutajika kwa madhumuni ya kufungua, kutengeneza au kukarabati barabara zote za umma. Mhe. Spika, machimbo sio lazima iwe tundu inaweza ikawa ni ardhi halisi ambayo baadae hufanya tundu. Kwa hivyo, ni ardhi ambayo imetandikwa na Mungu baadae wanaadamu huichimbua na unaweza ukaita shimo, tundu au vyenginevyo.

Mhe. Spika, nasema hayo kwa sababu Muambe kuna machimbo, lakini sio asili yake kwamba ilikuwa ni matundu, asili yake ilikuwa ni ardhi ambayo ni ya kilimo wananchi wanalima, lakini Wizara hii ndio wameifanya iwe tundu, sasa wanadhani kwamba ndio asili yake. Ile ni ardhi ambayo imetandikwa vizuri ina mawe, miti na kila hali, lakini Wizara hii chini ya Idara ya Ardhi basi wamekubali kuwa iwe tundu. Sasa sidhani kwamba ile ni ardhi ilikuwa ni tundu, iwe shimo asili yake ni ardhi kama ardhi nyengine.

Mhe. Spika, sasa machimbo kwenye mswada huu sijaona matumizi yake katika hivi vipengele vingi. Kwanza tafsiri ya machimbo, lakini sijaona vipi machimbo haya yametumika. Lakini nianzie hapo Mhe. Spika, kusema kwamba kifungu cha 11, 12, 13 kimechuku *reference* ya fidia kwenye sheria ya ardhi ambayo tumerekebisha Baraza lililopita, kwamba fidia yoyote ambayo itahusika na matumizi ya ardhi, serikali ikihitaji kuchukua ardhi basi itatumia fidia kulingana na soko la wakati husika.

Mhe. Spika, mimi nipongeze kwamba serikali imeona haja hiyo, tumekuwa tukiwapa wananchi wetu fidia ambazo ni udhalilishaji wa wazi, sasa serikali itaona umuhimu wa sheria ya ardhi nadhani ni jambo zuri na niwaombe wananchi wa Zanzibar wajue tu kwamba kuanzia sasa sheria ipo kwamba fidia yoyote ile ilingane na soko halisi la muda mfupi.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Bakari Makame, amesema hapa kwamba amepewa nyumba yake milioni saba, lakini wengine wanapewa fidia ya nyumba na mashamba sambamba na miti husika chini ya kiwango cha bei cha soko husika. Sasa Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri hili lisiwe tu ndani ya maneno ndani ya sheria, lakini litekelezwe kwa vitendo.

Mhe. Spika, Wizara hii imekuwa ikilipa fidia kwa ujenzi wa barabara, ni kweli Mhe. Mussa amesema pale, kuna wananchi wengi wanaingizwa katika mikataba bila hata kujua watalipwa nini, saini inatiwa mwanzo na ushahidi huo upo hatimae Wizara inakwenda kutia *figure* ambayo itamlipa yule mtu, akipewa fidia Mhe. Spika, hatimaye inakwenda kinyume na thamani ya jengo au shamba halisi.

Mhe. Spika, huu ni udhalilishaji na ninaweza kusema huu ni utapeli wa sirisiri, kwamba unamtilia mtu saini bila ya kujua atalipwa nini, hatimaye mwisho wa siku kunakuwa na mgogoro, lakini mwananchi wa kawaida afanye nini wakati tayari ametia saini yake.

Kwa hivyo, mimi nichukuwe nafasi hii kuwaelimisha wazanzibari kwamba hakuna ruhusa ya kutia saini pahala popote bila ya kujua utalipwa kiwango gani na kwa thamani gani. Ni muda mrefu Wizara hii imekuwa ikitumia hadaa na wananchi muda mrefu wamekosa fursa zao kwa sababu walikuwa hawashirikishwi ipasavyo kujua fidia hii ni kwa thamani gani. Mhe. Spika, sambamba na hilo fidia hii iendane na uwazi.

Tumekuwa tukipokea malalamiko kwamba hivi karibuni barabara ya Aman, Mkapa *road* kuna mwananchi amepewa fidia, lakini fidia ile Mhe. Spika, mwanzo aliambiwa tu kwamba fidia yako itaongezwa milioni tano, lakini tano hizi basi uje tugawane. Siku ya malipo jamaa alikataa kutoa ile fidia ile ziada hatimaye siri ikavuja kwamba kumbe kile ambacho alilipwa sicho thamani halisi, ilikuwa kuna asilimia fulani ya wahusika irejeshwe kwenye mfuko wa nyuma.

Mhe. Spika, tusende hivyo, tusitumie mwanya wa fidia kuhujumu mali na fedha za umma, lazima kuwe na uwazi na Mhe. Mussa amesema Wawakilishi, Madiwani na Masheha washirikishwe ili uwazi upatikane kwamba ile fedha inayotumika ni fedha ya wananchi wa Zanzibar, isiwe kuna mgongo wa fidia Mhe. Spika, kumbe kuna watu wanafaidika kwa ajili ya kupata maslahi yao.

Kwa hivyo, niombe wazanzibari tena kwa mara nyengine kwamba wasikae tu kimya wakiona jambo linahusu fidia basi wawaarifu Masheha, Madiwani, Wawakilishi na hata vyombo vyengine kwa ajili ya kuweka wazi katika masuala mazima ya fidia.

Mhe. Spika, kifungu cha 23(1) kimerekebishwa mimi ninasema hakitekelezeki, kwamba isipokuwa pale ambapo mali binafsi imehifadhiwa kwa matumizi ya Idara masafa ya hifadhi ya barabara kutoka katikati ya barabara kwa aina ya barabara na pande zote mbili za barabara itakuwa,

kwanza barabara kuu mita 15 Mhe. Spika, mimi ninatoa *challenge* hakuna barabara Zanzibar yoyote kutoka katikati ya barabara ya mita 15 kushoto na mita 15 kulia, usiharibu majumba nusu na robo ya wakaazi wa Zanzibar na hii ni kwa nini.

Kwa sababu Zanzibar serikali yenyewe imekataa kufuata Zanzibar *Transport Master Plan,* wamewaachiwa watu wanajenga wanavyotaka, mwenye nguvu mpe leo unatwambia mita 15 kushoto, mita 15 kulia labda iwe futi. Lakini hakuna barabara yoyote Zanzibar ambayo ukitoka katikati ya barabara utakwenda mita 15 kushoto na mita 15 kulia.

Maana Mhe. Spika, mita 15 nina hakika ni kutoka hapa nilipo sijakupita wewe huko uliko. Sasa niambie barabara gani ya Zanzibar ambayo inaweza kuruhusu hivyo. Na hivyo hivyo Mhe. Spika, hakuna barabara yoyote ambayo inaunganisha barabara kuu mita 12, barabara za mita 10 na barabara nyengine mita ambazo zitaamuliwa na Idara.

Mimi ninatoa *challenge,* Waziri anambie barabara gani Zanzibar ina uwezo wa kupima mita 15 kushoto na kulia kwa ajili ya kufanya *extension* ya barabara kama ni hifadhi ya barabara. Mhe. Spika, kifungu hiki naomba kiondoshwe au vyenginevyo tuambiwe ni futi badala ya mita, vyenginevyo Mhe. Spika, tunatafuta namna ya kuwavunjia wazanzibari majumba yao kwa makosa ambayo serikali wameyafanya wenyewe.

Mipango miji haikuzingatiwa watu wameachiwa kiholela, leo watu wemewekeza majumba ya kisasa unasema kwamba upime barabara kuu mita 15 kushoto na kulia, Mhe. Spika, mimi nina hofu sana kwamba kifungu hiki lengo lake nikukusudia kuwadhalisha wazanzibari wanyonge waliojenga, hakuna barabara ambayo tunaweza kupima mita 15 au 12 au mita 10 labda tuambiwe ni futi au sentimita, vyenginevyo Mhe. Spika, hii ni dhahiri kwamba Wazanzibari watafutiwe namna ya kuvunjwa nyumba kama zilivyovunjwa nyumba pale Mtoni mwaka 1996 kwa kisingizio kwamba kuna hifadhi ya umeme.

Leo pale pale palipovunjwa umeme Mtoni, leo tayari majumba yamejengwa. Serikali hii hii walivunja nyumba kwa gharama kubwa kwamba kuna hifadhi ya umeme, ndio serikali hii hii leo watu wameruhusiwa wanajenga majumba ya kisasa hii ndio dalili yetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba kifungu hiki kifutwe hakitekelezeki hata miaka 100 inayokuja.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka niseme ni kifungu cha 15 ambacho wenzangu wamezungumza kuhusu suala la fidia. Mhe. Spika, mimi nadhani serikali haiwezi kutekeleza, ikiwa fidia itakwenda kwa soko halisi basi kwa

utaratibu wa kujenga barabara bila ya mipango nadhani serikali itashindwa kulipa fidia. Mimi nimeingia hofu kwamba sasa serikali imesema kuwa kifungu kipya cha 19(1) na 19(2) kilichotokana na marekebisho ya kifungu cha 19 cha sheria mama kwamba mtu kama hakuridhika na fidia basi aende Mahakamani.

Mhe. Spika, Mahakamani ni zuio la haki, Wazanzibari watakwenda Mahakamani kudai fidia yao, nina hakika zitapita awamu nyingi za utawala hakuna fidia itakayopatikana. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi nina hakika kwamba serikali imeweka kifungu hiki wakijua kwamba Mahakamani hakuna kinachofanyika, wananchi watadhulumiwa haki zao, watakwenda Mahakamani badala ya kupata fursa basi watapata maudhi ambayo kwa kweli wengine watatiwa kaburini hawapati haki yao.

Kwa hivyo, mimi nadhani serikali itwambie sasa je, kutakuwa na fungu maalum la kila mradi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ambalo litatengwa kwa ajili ya kutoa fidia pale ambapo serikali itachukua ardhi au vipando vya wananchi, badala ya kuwasukuma Mahakamani ambako tuna hakika sote humu kwamba ni sehemu ambayo wananchi haki yao huchelewa sana kwa utaratibu wetu wa utawala hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, suala la uharibifu wa mazingira kifungu cha 20 kimezungumza, mimi naomba nitoe ombi Mhe. Spika, kwamba katika maeneo ambayo yamekuwa ni machimbo hapa Unguja na Pemba, basi sheria hii iseme wazi kuwa lazima kuwe na fidia ya uharibifu wa mazingira.

Mhe. Spika, Wazanzibari hawakatai miradi ya maendeleo, lakini mradi unapokwenda kuchimba fusi, mchanga au mawe hatimaye ukiacha mashimo ambayo maji yanatuama na kunakuwa na mazalio ya mbu athari inakwenda kwa wananchi husika. Kwa hivyo, sheria hii Mhe. Spika, tuongeze kifungu ambacho kitahakikisha kwamba serikali ikitumia eneo fulani kwa machimbo basi lazima eneo lile kuwe na fidia kwa ajili ya athari za kimazingira.

Mimi nimetishika kwamba sasa machimbo yalioko kule Mwambe, Vitongoji na hata Shakani basi wananchi wataendelea kuteseka na hakuna faida inayopatikana. Zaidi nimetishika kuwa eti Afisa wa Serikali akiwa amepewa agizo na mtu akipinga basi adhabu yake ni kifungo na faini, lakini serikali ikiharibu mazingira wananchi wakifa hakuna adhabu yoyote. Mhe. Spika, mimi kifungu hiki sikikubali *unless* kuwe na kifungu ambacho kinahakikisha kutoa fidia kwa wananchi pale watapoathirika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu haya, niseme kwamba siungi mkono mswada huu kwa sababu athari ya mazingira mimi naijua kule kwetu

Mwambe, bila ya kupewa maelezo ya kina kisheria kwamba nini fidia ya athari ya mazingira pale ambapo serikali itatumia maeneo haya kwa maslahi ya umma, lakini vile vile ni kulinda maslahi ya umma wengine kwa kuepusha mazingira ambayo yameathiriwa vibaya. Mhe. Spika, vyenginevyo serikali itaendelea kuharibu mazingira na wananchi watapata athari kubwa na hakuna fidia ambayo itapatikana.

Mhe. Spika, naomba maelezo hayo nije niridhike, Mhe. Waziri, akiniridhisha basi nitaunga mkono hoja na kama hakuniridhisha mimi sitakuwa miongoni mwa kupitisha mswada huu. Nakushukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi kwanza kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kuweza kunipa nafasi angalau na mimi nikatoa maoni yangu mawili matatu katika haya marekebisho ya Sheria ya Mswada ya Kurekebisha Amri ya Barabara Sura ya 134. Mhe. Spika, mimi kwa kuanzia nataka nipate ufafanuzi wa hii sheria, kwa sababu hapa tumeambiwa Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Amri ya Barabara Sura ya 134.

Sasa tumezoea kuambiwa kwamba sheria inayorekebishwa sheria nambari ngapi ya mwaka gani, lakini hapa moja kwa moja tumeambiwa sura ya 134. Sasa naomba nipate ufafanuzi labda Mwanasheria Mkuu atatusaidia zaidi imekusudiwa nini. Kwa sababu nilikuwa najaribu kutafuta hii sura katika sheria ya mwaka gani kwa vile tunaambiwa ya kikoloni au zamani hii sheria ndio ilikuwa inaitwa sura au vipi, nafikiri hapo nitapata ufafanuzi.

Lakini nashukuru jitihada ya serikali kwa kuendelea kukokotoa zile sheria za zamani ambazo bado mpaka leo tunaendelea kuzitumia tangu enzi za ukoloni, sheria hizo wakati mwengine hata yanapotokea matatizo Mahakimu wetu kwa kweli wanashindwa hata pengine kutoza hizo faini.

Kwa sababu unaweza ukamtoza faini mtu ikawa ile faini ina hasara kwa serikali. Kwa mfano unaambiwa shilingi saba au shilingi tano, sasa hivi nafikiri sheria hizo zimepitwa na wakati. Tunaishukuru serikali kwa kuliona hili kwamba tunaweka sheria za kwetu wenyewe, hili kwa kweli nilikuwa najaribu kulipongeza.

La pili, Mhe. Spika, nilipoangalia kifungu cha 9 cha sheria mama ambapo kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 8(a) kama ifuatavyo; Na hapa chini zimeelezwa aina za barabara.

Mhe. Spika, kwa bahati mbaya hiyo sheria yenyewe *original* sijawahi kuiona nikaisoma, lakini angalau nashukuru kwamba tumeweza kutolewa ufafanuzi

wa hizi barabara. Vile vile, Mheshimiwa, sijajua baada ya kuainishwa hizi sheria sasa mmiliki hatujajua labda Mhe. Waziri, akija aje atuelezee mmiliki wa barabara hizi atakuwa nani. Kwa sababu hapa pana barabara kuu, barabara za vijijini, barabara za mijini, barabara za kulishiza na barabara nyenginezo. Mhe. Spika, tunataka tuje tupate ufafanuzi hizi barabara zote atakayekuwa anazimiliki ni nani.

Kwa sababu leo tunapokuwa na matatizo yetu kwenye barabara zetu, wenzangu wamezungumza barabara zao za vijijini na wapi, lakini hata na sisi ambao majimbo yetu yapo mjini kuna barabara ambazo tunakuwa siku zote tunazipigia kelele hasa hizi tunazoziita *feeder road.* Mhe. Spika, tumewahi kuona mawaziri wanapokuja kupapatua tunapotaka hizi barabara zetu zifanyiwe ukarabati hasa kupitia Mfuko wa Barabara. Tunaambiwa barabara hizo ni *feeder road* haziko chini ya Idara ya Utunzaji na Ujenzi wa Barabara, lakini ziko kwenye Manispaa au Halmashauri.

Wakati kama tunavyojua kwamba Manispaa na hizo Halmashauri hazikusanyi *road toll*, *road toll* tunayoikusanya inakusanywa moja kwa moja na Mfuko wa Barabara ambao uko Wizara ya Fedha ambapo fedha zile wanapewa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara kwa ajili ya ukarabati.

Sasa katika hizi *categories* tano tulizoletewa tunataka tuje tupate ufafanuzi ni zipi zitakazokuwa chini ya Serikali Kuu na zipi zitakazokuwa katika Halmashauri na Manispaa, hizo ambazo zitakuwa katika Halmashauri na Manispaa *funds* zake za kukarabati barabara hizi zitatoka wapi. Sasa hili nadhani katika sheria hii ni lazima tuje tupate ufafanuzi ili tujue hizi barabara mwenyewe ni nani.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu mimi nataka nishauri baadhi ya mambo, unajua hizi sheria Mhe. Spika, tumeshaunda nyingi sana, lakini bado ukija ukiangalia kwenye barabara zetu kwa kweli kuna uzembe mwingi sana ambao unafanywa na madereva wa aina mbali mbali. Mimi sitaki kusema madereva wa daladala tu, kwa sababu wao wamefurutu ada, lakini na madereva wengine.

Mhe. Spika, pamoja na sheria zote tunazozitunga, lakini kama hakuna zile saini za barabara, hatujafanya jambo. Kwa sababu unapokwenda kuchukua leseni ya udereva Mhe. Spika, unaoneshwa zile saini, saini hii unatakiwa *parking* hapa usi-*park*, hapa unatakiwa umpite mwenzako, hapa ukiona alama hii usimpite, lakini leo unakwenda kusomeshwa saini za kutumia barabarani ukija ukenda humo barabarani mwenyewe huzikuti, sasa tutegemee nini. Mimi Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri, barabara zetu zote za Unguja na Pemba, Mijni na Vijijini tutiliwe alama.

Mhe. Spika, sisi tunatembea nchi za wenzetu, nashukuru Mhe. Mussa Ali Hassan, yeye kenda Swaziland ameona mambo mengi, lakini na sisi tumebahatika kwenda sehemu nyingi. Mhe. Spika, nchi nyingi unazokwenda wenzetu hata ukenda nje ya mji kabisa ndio hizi barabara tunazoambiwa za kulisha zote unakuta kuna alama za barabarani na hizi alama za barabarani Mhe. Spika, zinawasaidia madereva hata wale wageni.

Tunajua tuna utaratibu wageni wengine wanakuja na leseni zao, akija mtu anakodi gari, leo barabara haina alama hata moja, hajui hapa kuna mpindo, hajui hapa umpite mwenzako, hapa usimpite mwenzako tunakwenda wapi, hizi sheria tunazitunga za nini. Sasa mimi naomba hii sheria ni nzuri tunaitengeneza vizuri, lakini sasa hebu tufuate na yale matakwa ya hizo barabara zenyewe.

Mhe. Spika, wenzangu wanazungumza gari zinakwenda kwa kasi wakati mwengine, hili bado tuna tatizo jengine, hatuna utaratibu wa kuwadhibiti madereva. Mhe. Spika, ukienda Uingereza hata Marekani sheria hizi wanazo wanatengeneza sheria nzuri tu, dereva wala askari hapati tabu. Wale wenzetu wana utaratibu dereva anakuwa ana *marks* zake, kila ukifanya kosa unapunguziwa *marks*, ukifanya tena kosa unapunguziwa *marks* mpaka mwisho unafika pahala unazuiliwa leseni si chini ya miezi sita, sasa hebu tuekeni hizi.

Leo haya mashaka yanayotokezea unaambiwa sijui askari *traffic* wanakula rushwa, wanafanya nini, ndio. Kwa sababu *traffic* akishamkamata dereva atampeleka Mahakamani kenda kule kapigwa faini shilingi elfu tatu anarudi, anafanya tena akienda kule faini shilingi elfu tatu tena. Kwa hivyo, ina maana yule dereva anakuwa anazoea mpaka Mahakama haiogopi tena, lakini leo tukitengeneza sheria nzuri ambayo itakuwa inawadhibiti madereva kumpunguzia *marks* katika leseni yake Mhe. Spika, nadhani tutakuwa tumetengeneza sheria nzuri na hizi ajali nyengine zitapungua.
Mimi bado nashangaa sana, Waheshimiwa sisi tunatembea sana duniani na tunapotembea tunatembea mpaka vichochoroni, hatuoni matuta. Mhe. Spika, kwa wenzetu matuta hatuyaoni, madereva wanapowekewa matuta ina maana wana matatizo kwenye akili zao kwa nini tuwe na matuta, basi mtu apunguze kasi kwa matuta tu hakuna sheria, hakuna alama za barabarani, hakuna *penalty* zinazomfanya yule mtu lazima afuate sheria za barabara.

Sasa mimi naomba sana Waheshimiwa, kwa sababu sisi tunakwenda kwa wenzetu na wenzetu wanakuja huku, leo kila pahala matuta, mimi nadhani hakuna haja ya matuta, matuta ni sheria ambazo zinatekelezeka, sheria

ambazo mtu zitamfanya mtu aogope kutenda lile kosa. Sasa kama tunaogopa kutumikia sheria, hilo litakuwa ni tatizo letu.

Mhe. Spika, nazungumzia na suala la *parking* mwenzangu kalizungumza Mhe. Hija Hassan Hija. Mhe. Spika, mwaka 2006 miaka hiyo tulifanyiwa semina mbali mbali ya *Transport Master Plan* ya Mji wa Zanzibar na wakaweza ku-*allocate* maeneo kwamba haya ni maeneo ambayo zitapita barabara na wameweka mtandao mzuri. Walituita pale Bwawani wakatupa semina nzuri kwamba ili kuondoa msongamano gari zinazotoka mjini zitapita hapa, zinazotoka Kaskazini zitapita hapa, zinazotoka Kusini zitapita hapa, lakini vile vile tukajaribu kuwa-*alert* jamani hii *Transport Master Plan* lazima muanze kutoa maangalizo kwa ujenzi mpya.

Tuliwaambia kuwa sasa hivi kuna utamaduni umejengeka katika kila karibu na barabara kuu watu wanaanza kuporomosha magorofa, kuna maeneo mengine tulijaribu kutoa ushauri, haya maeneo ambayo barabara za kuingilia mjini zitakuja kupita magorofa yanajengwa kwa wingi, serikali itakuja kupata hasara kubwa kwa ajili ya ulipaji wa fidia.

Katika hii sheria humu leo kwa bahati nzuri Mhe. Waziri, kuna kifungu hapa ameeleza vizuri tu, fidia sasa hivi itaendana na soko. Leo angalia magorofa mangapi kama tutatekeleza ile *Transport Master Plan*. Je, magorofa mangapi tutaweza kuyavunja na serikali uwezo huo wataupata wapi.

Sasa ndio kama tunavyosema kuna mipango mizuri tunaipanga au labda kila Waziri anayekuja anakuja na mipango yake akishaondoka yeye na ile mipango imekufa, anakuja mwengine anakuja na mipango yake, mipango hii Mheshimiwa itakuwa haifiki mwisho, tunaomba mipango ibakie ya wataalamu sisi wanasiasa tuje tuweke sera na mikakati ya kutekeleza hizo sheria zenyewe. Sasa katika sheria hii labda Mhe. Waziri akija aje atwambie ile *Transport Master Plan* imefikia vipi na itatekelezeka.

Lakini pamoja na hayo Mhe. Spika, baada ya semina zile tuliona kuna alama zimeanza kutolewa. Ukiangalia kama utapita hii barabara inayotoka kwa Bi Ziredi inayoelekea mitaa ya juu kupitia Magomeni na hii barabara inayoendea Tunguu, kuna baadhi ya nyumba mle pembeni zimetiwa alama tena alama zenyewe ni nyekundu na alama nyekundu inakuwa ni hatari.

Sasa hatujui alama zile kama je wale wanatakiwa waondoke au wanatakiwa wafanye nini. Kwa sababu kama hivyo ninavyosema kuna alama na watu bado vigorofa vinaanza kuporomoshwa, sasa haya angalau wananchi waweze kujua na kama hivyo sheria hii ndio inakuja, ishampa mamlaka Waziri ya

kusema kwenye barabara kuu mita 15, sasa sijui katika hizo barabara zetu kuu sasa hivi kama angalau hizo mita kumi zinatimia.

Sasa leo hapa tukimpa mamlaka Mhe. Waziri katika barabara kuu kama mita 15 katika zile barabara nyengine mita 12, sijui hizi mita katika sheria hii walikwenda wakazipima. Kwa sababu mimi katika miongoni mwa semina ambazo niliwahi kuzipata naambiwa maisha yote nyinyi ndio Waheshimiwa mnaotunga sheria, mkitunga sheria aidha mtawasaidia wananchi au mtakwenda kuwaangamiza wananchi. Sasa nilikuwa nataka niulize kuna utafiti uliofanywa katika hiki kifungu cha 18.

Halafu hapa chini hifadhi ya barabara kifungu cha 23(a) kimeeleza kuna barabara kuu mita 15, barabara zinazoungana na barabara kuu mita 12, barabara za wilaya mita 10 na barabara nyengine kama itakavyowekwa na idara. Sasa leo tukishaweka mita hizi na katika sheria hii tumeshaweka kwamba watu walipwe fidia kwa mujibu wa soko. Je, hizi mita kweli zitatekelezeka. Mimi naomba sana, suala la hifadhi ya barabara ni muhimu sana, lakini ni muhimu sana inakuja katika zile nchi ambazo moja kwa moja zinafuata zile sheria wanazozitunga.

Mhe. Spika, mimi kuna safari moja niliwahi kwenda Botswana, Botswana wenzetu ni nchi ndogo sana, lakini katika nchi ambayo ina hifadhi ya barabara ni Botswana, maana ukiacha ile barabara kuu yaani barabara kuu unakuta lile la Michenzani kuna barabara huku na huku, lakini ile hifadhi yake ya barabara upana wake ni sawa sawa na ile barabara uliyopita. Sasa utakuta unaona hasa kwamba pale hata kama kuna mipango ya maendeleo ya baadae serikali haina haja ya kulipa fidia wala haina haja ya kupata tabu kusokotana na watu.

Lakini sisi leo kwa kweli tumeshajiachia sana na serikali kwa kuwa imejiachia na wananchi wamejiachia wamejenga kweli kweli. Sasa mimi nataka niulize. Je, hizi mita tulizozitaja katika hiki kifungu cha 18 na 23(a).(1) tumefanya utafiti tukapima hizi barabara kuu mita 15 kwa sasa hivi zinapatikana na hizo nyengine zinapatikana, *otherwise* tuzipunguze hizi mita. Kwa sababu ikiwa hazitimii tunaweza tukasema badala ya mita 15 kwa hizi barabara kuu tuweke mita 10 na hizi barabara zinazoungana na barabara kuu badala ya mita 12, tuweke angalau mita 8, barabara za wilaya naamini mita 10 zinapatikana kwa sababu bado ni maeneo ambayo yako open kabisa hayajavamiwa sana katika masuala ya ujenzi.

Lakini jengine Mhe. Spika, katika suala la *parking*. Suala hili Waheshimiwa wamelizungumza sana na kwa kweli sasa hivi ukiangalia wananchi wetu wanapata tabu sana. Ukienda pale hata mimi mwanamapinduzi, mimi

nashukuru kwamba chama chetu bado nakipenda na naendelea kukipenda hivyo hivyo na ikiwezekana harudi tena, harudi kwao sasa hivi.

Mhe. Spika, pale Ofisi Kuu ya *CCM* sasa hivi wenyewe hatuna raha, zogo, magari huku na huku na pale pembeni sisi tuna eneo letu tunataka kuweka mradi mkubwa pale, leo magari pale zogo tafrani, mimi nafikiri ile adha ya pale watuondolee, bado mimi nataka kusema serikali itafute maeneo na kama sasa hivi serikali tunaishukuru sana kwa jitihada zenu mnahangaika dunia nzima tayari kuna hawa wawekezaji wa *real estate* ambao watakuja kutujengea majumba makubwa katika nchi yetu, basi tafuteni wekeni kwanza hiyo *master plan* ya mji tuone mji utakuwa uko vipi halafu *parking* iwekwe pahala, bomoweni nyumba mtengeneze *parking* ili wananchi wetu waweze kupata nafuu.

Leo Mhe. Spika, mtu anatoka na mgonjwa anakuja pale gari ina usumbufu mtu atoke Hospitali ya Mnazi Mmoja anakuja mpaka Ofisi Kuu ya *CCM* ni tatizo. Sasa mimi nafikiri katika utaratibu huu, mimi naomba vyombo vyetu hivi vina utaratibu na siku hizi jambo lolote linakwenda kwa maridhiano, hata hizi *parking* zilipokuwa zinapangwa mimi nadhani walikuwa wakae watu wa Manispaa, watu wa Ushirika wa Daladala pamoja na Madiwani.

Kwa sababu madiwani ndio wenye watu, mimi siamini kama madiwani wataweza kuruhusu utaratibu ambao wananchi wataweza kupata tabu. Mimi nafikiri bado kuna tatizo kwa sababu wenye daladala wanapiga kelele, wananchi wanapiga kelele siku hizi kuna vyombo vya habari vya *private* kila siku wanazungumzia suala hilo bado ni adha kubwa kwa wananchi.

Sasa mimi naomba Mhe. Spika, suala hili kama bado ni tatizo basi niwaombe sana wenzetu wa Manispa kwa sababu hili sio la Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hili ni suala la Manispaa, wakae watu wa Manispaa, madereva wa daladala na madiwani wajaribu kuangalia wanaweza wakafanya utaratibu gani ili kuweza kuweka hali nzuri.

Kwa sababu hata pale kwenye Baraza letu la Wawakilishi la zamani kwenda kuwekewa zogo la magari pale hata huu mji sasa hivi hatujui tunakwenda vipi, zogo pale magari yanakaa tafrani. Lile eneo ambalo linaonekana ni mjini lina utulivu leo tafrani imekuja pale. Mimi nadhani Mhe. Spika, maeneo kama haya ni vizuri tukaweza kuyazungumza kwa vizuri ili wananchi wasipate tabu.

Mhe. Spika, mimi najaribu kuulizia, je, sheria hii itakapotiwa saini kwa sababu mpaka sasa hivi kuna barabara zimeshajengwa na wananchi mpaka leo hawajalipwa fidia zao. Je, baada ya kutiwa saini sheria hii na wale wataweza

kuangaliwa kwa mujibu wa sheria hii. Ingawa wamebomolewa zamani lakini mpaka leo hawajalipwa. Je, hii fidia ambayo inaendana na soko na wao itaweza kuwa-*accommodate*. Sasa hili kidogo nataka nipate ufafanuzi.

Jengine katika suala la fidia hapa kumekuwa na malalamiko sana katika fidia hakuna uwazi. Mimi naomba sana, sasa hivi tuko katika utandawazi na sasa hivi serikali yetu imeanzisha *system* ya *E-Government*. Mimi nafikiri masuala ya fidia kile kitengo kiwe wazi kabisa kiwekwe katika *Website* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba katika barabara hii kuna watu hawa watalipwa kila kitu ukifungua tu unaangalia, je, wananchi wangapi wanatakiwa kulipwa fidia katika barabara hii, *amount* inaonekana pale.

Hapo itakuwa hakuna fitina wala kitu chochote, sasa hivi wakati wa uwazi kila kitu kinatakiwa kiwekwe katika mtandao. Hilo mimi najua litachukua muda, lakini naomba watafute hiyo *system* ili mambo yote yawe hadharani. Sasa la mwisho kabisa kwa sababu ya muda Mhe. Spika, nilikuwa nataka na mimi nizungumzie suala la mazingira.

Mheshimiwa katika kitu ambacho ninapata tabu, Mwenyekiti wako kamati yangu inasimamia masuala ya mazingira katika eneo lenye uharibifu mkubwa wa mazingira ni eneo la ujenzi wa barabara, tatizo hawa wajenzi wa barabara hatuwapangii yale masharti ya mazingira, leo wanakuja wanachimba mashimo ukienda kama kule Matemwe Mhe. Spika, kama utaweza kuchupa basi ukitoka juu katika ile sehemu waliyochimba ukifika chini kiuno huna miguu yote itaingia ndani, leo barabara imemaliza wameondoka shimo halikufukiwa mpaka leo ukiuliza na katika sheria ya mazingira ipo unaambiwa kuna fidia pale ya *conversation* ya *environment* ni 10%, lakini 10% hiyo hailipwi *cash* wala hailipwi kwa vitendo.

Sasa mimi nilikuwa napendekeza kwa Idara ya Mazingira kwamba ile 10% bora ilipwe moja kwa moja Idara ya Mazingira, walipwe hasa *in cash*. Kwa sababu Idara ya Mazingira wao ndio kazi yao kuhifadhi mazingira, lakini ukimwambia mjenzi wa barabara kwamba hii 10% utafukia mashimo, mtu akishachukua chake keshamaliza barabara anaondoka hakuna fidia. Kwa mfano barabara ya Bumbwini sisi tumekwenda kuna shimo pale tukawaambia walifukie wakalifukia robo mpaka leo limeachwa.

Sasa Mhe. Spika, tunaomba sana bado suala la uhifadhi wa mazingira na tunajua sasa hivi miradi yote mikubwa inavyotakiwa lazima kabla ya uanzishwaji wake aidha ikiwa ya binafsi au ya serikali kwanza ufanyiwe utafiti wa mazingira na

baada ya kupata kibali cha mazingira ndio miradi ile iweze kutekelezeka. Lakini hayo hayafanyiki Mhe. Spika, miradi inafanyika na barabara zinajengwa bila ya kibali cha mazingira.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, kabla hujanipigia kengele mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura hatuna tatizo la mswada huu isipokuwa zaidi ya yale maeneo ya mita za barabara nitamuomba Mhe. Waziri, aje anipe ufafanuzi. Lakini vile vile, na ile fidia ambayo wale wananchi ambao barabara zimeshajengwa mpaka leo hawajalipwa baada ya kutiwa saini sheria hii, je, vipi na wao watakuja kuwa *accommodated* au vipi.

Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii.

(Saa 6:57mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kauli tuliyoitoa asubuhi ilikuwa jioni hii tuendelee na mswada ule wa kwanza wa kuundwa kwa Baraza la Vijana, ila napata mashaka tu ya kuja kufikia pahala ikawa hatujaweza kufikia maamuzi, *quorum* ipo chini. Nafikiri kwa idadi ya Wajumbe wenyewe waliomo ndani haipendezi machoni kwa wananchi. Hivyo, ningeomba tuakhirishe kwa muda ili baada ya hapo tuweze kuendelea na shughuli zetu. Naakhirisha kikao hiki kwa muda wa dakika 15 ili kuwaita Waheshimiwa Wajumbe waliokuwa hawajafika.

(Saa 11.01 jioni Baraza liliakhirishwa kwa muda wa dakika 15 kutokana na kutotimia quorum)

(Saa 11:16 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tulikubaliana kwamba jioni hii tuje kufanya majumuisho kwa mswada ule wa kuanzishwa kwa Baraza la Vijana. Lakini kabla ya kuanza kwa shughuli hiyo, naomba nichukue nafasi hii kutoa masikitiko yangu kwa mahudhurio yasiyopendeza, mahudhurio hayaridhishi, tunachelewa sana na wakati mwengine ndani ya ukumbi kama ilivyotokea hivi punde jioni hii Wajumbe waliokuwemo walikuwa hata kumi hawafiki, mbele ya macho ya wananchi ambao ndio tunaowawakilisha katika chombo hiki.

Kwa kweli haileti sura nzuri, haiwaridhishi wananchi na si jambo jema kwa chombo kikubwa kama hichi cha kufanya maamuzi makubwa kwa ajili ya wananchi wetu kufika pahala wenyewe wakaona kwamba hali ndio ile ambayo tunayo, hali ambayo kwa kawaida na kwa mujibu wa taratibu zetu hatuwezi tukafanya maamuzi yoyote, wakati mwengine kama michango inaendelea huwa tunafumbia macho tu, lakini pia nayo haipendezi, kwa sababu idadi inakuwa ni ndogo mno.

Jambo kama hili liliwahi kutokea pale Bungeni na mpaka wananchi wakawa wanalalamika kwamba Waheshimiwa hawahudhurii vikao kwa wakati, na ikawa inaeleweka katika maredio na televisheni wananchi wakitoa masikitiko yao. Kwa hivyo, nilikuwa nataka niombe kwamba kabla ya wananchi wetu hapa Zanzibar nao hawajatoa masikitiko yao, basi tujirekebishe ili wananchi waone kwamba ni kweli kweli hasa tumezingatia mambo ambayo tunajipangia, kuyafanya kwa wakati na kwa muda kama tulivyopanga katika Kanuni zetu.

Muda wa kawaida asubuhi tunauelewa sote saa tatu asubuhi barabara, na jioni tukiingia saa kumi na moja. Labda kama hoja ilitolewa mapema na kuamuliwa katika nyakati nyengine zisizokuwa hizo.

Sasa nilitaka nichukue nafasi hii kuwaomba sana wananchi, nawaomba radhi kwa kuona Wawakilishi wao hawafanyi kazi ipasavyo kwa kufuata taratibu tulizojiwekea ili tukafanya kazi zetu kama vile inavyotakiwa tufanye. Ilikuwa tunatafakari nini cha kufanya ili kuona kwamba shughuli zetu zinakwenda vizuri kwa mujibu wa taratibu zetu, na kimsingi jambo kubwa na muhimu ni kujirekebisha ili tukaona tunafanya kazi zetu kwa ufanisi na kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea.

Hali hii haipendezi, haifurahishi mbele ya wananchi, kwa kweli inashusha hadhi yetu katika kuwashughulikia wananchi wetu.

Waheshimiwa Wajumbe niombe sana kwamba jambo hili lisiendelee kutokea na likatupa sura mbaya katika utekelezaji wa shughuli zetu kwa mujibu wa Katiba na Kanuni zetu. Naomba sana Waheshimiwa Wajumbe tufuate taratibu tulizojiwekea kwa mahudhurio na kutekeleza wajibu wetu kama ipasavyo.
Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe, narudia tena kuwaomba radhi wananchi wetu juu ya tukio hili ambalo lililojitokeza ambalo kwa kweli halipendezi. Basi baada ya hayo sasa nadhani tuendelee na shughuli zetu, na kama tulivyokubaliana kwamba jioni hii tuje kufanya majumuisho katika mswada ule ambaoMhe. Waziri alikuwa anakutana na Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Kabla ya kumuita Waziri basi labda nipate taarifa tu kama Kamati wamefanikiwa kufanya hivyo ili hatimaye nimuite Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti karibu.

TAARIFA

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Ahsante sana.

Mhe. Spika, naomba nitoe taarifa ya kuwa Kamati pamoja na wizara zimekaa na kufanya marekebisho ya mswada. Naomba kutoa hoja.

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Sio hoja ya kuamuliwa isipokuwa umetoa taarifa kwamba shughuli sasa zipo tayari.Basi baada ya hapo nimuombe sasa na kumkaribisha Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, karibu.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru *Allah Subuhana Wataallah* kwa kutujaalia afya njema na kuendelea na kazi za Baraza.

Pili, nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii ya kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali. Tatu ninatumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa wote kwa michango yao ya maneno na kimaandishi yenye nia ya kuimarisha mswada huu na kulifanya Baraza liwe makini na linalotekelezeka.

Mhe. Spika, michango na mapendekezo yote iliyotolewa na Waheshimiwa yamepokelewa na kuzingatiwa kama inavyoonesha katika orodha ya marekebisho niliyowasilisha kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba sasa kuwatambua Wajumbe wote waliochangia mswada huu:

1. Mhe. Farida Amour Mohamed; kwa niaba ya Kamati
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mohamed Haji Khalid
4. Mhe. Salma Mohamed Ali
5. Mhe. Ashura Sharif Ali
6. Mhe. Hija Hassan Hija
7. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

8. Mhe. Hassan Hamad Omar
9. Mhe. Asha Bakari Makame
10. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
11. Mhe. Panya Ali Abdalla
12. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
13. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
14. Mhe. Rufai Said Rufai
15. Mhe. Mussa Ali Hassan
16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Abdi Mossi Kombo
18. Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Na waliochangia kwa maandishi ni:-
1. Mhe. Fatma Said Mbarouk
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
3. Mhe. Suleiman Hemed Khamis

Mhe. Spika, nikianza naomba kutoa ufafanuzi zaidi kwa michango ya Waheshimiwa Wajumbe waliochangia kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, nikianza na Mhe. Farida Amour Mohamed kwa niaba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii. Nashukuru maoni yake yote. Maoni yote ya Kamati yamezingatiwa kama ilivyoshauri kabla. Lakini pia, Mhe. Farida Amour Mohamed alikuwa na maoni yake mwenyewe binafsi. Alisema kwamba suala la elimu kwa vijana.

Napenda nimuhakikishie Mhe. Farida Amour Mohamed na Waheshimiwa wote waliosisitiza umuhimu wa vijana kupatiwa elimu, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto imejiandaa vya kutosha kutoa elimu kabla ya kuanzishwa Baraza la Vijana na hata baada ya kuanzishwa Baraza.

Suala la elimu kwa walengwa litapewa kipaumbele. Aidha napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wajumbe kuwa suala la udhibiti wa ushabiki wa kisiasa ndani ya Baraza limewekwa wazi ndani ya sheria hii na litashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria hiyo.

Mhe. Spika, Makame Mshimba Mbarouk na yeye amesisitiza maafisa kuweka utaratibu mzuri wa kuwafikia vijana hadi ngazi ya Shehia. Wizara imejiandaa kusimamia utekelezaji wa sheria na kutoa mafunzo. Uundwaji wa Baraza utasimamiwa na maafisa husika kwa kufuata sheria hii.

Kuhusu suala la uajiri sio wizara itakayohusika na uajiri bali Baraza litaajiri wenyewe kwa mujibu wa uwezo na kwa kuzingatia mahitaji yao. Tunalowasisitiza ni kwamba uajiri utafuata Kanuni na sheria za Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, nikiendelea Mhe. Mohamed Haji Khalid, alitaka ufafanuzi wa umri wa kijana. Sheria hii imemtambua kijana kama ilivyotafsiriwa na Sera ya Maendeleo ya Vijana Zanzibar ya mwaka 2005 ambayo imeelezea umri wa kijana ni kuanzia miaka 15 hadi 35. Sera ambayo ilipitishwa na Baraza la Wawakilishi hili hili au lililopita.

Kuhusu muundo wa Baraza utaanzia ngazi ya Shehia, wilaya na taifa. Hili limejadiliwa sana katika vikao mbali mbali vilivyojadili mswada huo kabla ya kuwasilishwa Barazani. Kuhusu ngazi ya Mkoa, napenda kuwajuulisha Waheshimiwa Wajumbe kuwa haimo kabisa katika sheria hii. Hii imeingia kwa makosa ya kimaandishi.

Hoja ya kuanza ngazi ya shehia, wilaya na taifa imezingatia uchanga wa Baraza na gharama za uendeshaji. Kuhusu muundo kwa mujibu wa uandishi wa sheria utaanzia katika ngazi ya taifa, wilaya hadi shehia. Hata hivyo, kiutendaji Baraza la Vijana litafanya kazi zake kuanzia ngazi ya shehia, wilaya na itamalizia kwenye taifa. Tumeshakubali kwamba tuanze na shehia, twende kwenye wilaya na tumalizie kwenye taifa kama walivyopendekeza Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Spika.

Kuhusu mtandao wa Jumuiya za Vijana, wizara inatambua kuwepo kwa mtandao wa vijana uitwao *Zanzibar Youth Organization Network*; ni mtandao wa Jumuiya za Vijana zisizo za kiserikali ambao hauhusiani na siasa, uliosajiliwa na Mrajis wa Serikali kwa mujibu wa sheria za nchi unaounganisha taasisi zote zisizo za serikali za vijana Zanzibar.

Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe Kifungu cha 6 (h). Ushauri umepokelewa na kifungu hiki sasa kinasomeka:-
Kifungu cha 6 (h)

> "Kuanzisha, kuendesha na kusimamia miradi yenye faida ya kiuchumi na ya kijamii"

Mhe. Spika, kwa vile Waheshimiwa wote waliuliza suali la miradi yenye faida na isiyokuwa na faida na tayari tumeshafanya marekebisho na kwa bahati nzuri marekebisho nadhani Wajumbe wote wameshapatiwa.

Mhe. Salma Mohamed Ali, nakubaliana na ushauri wake wa kubadilisha kifungu kinachosema mgeni mualikwa na kwamba waalikwa waweze kutoka hata kwa jumuiya zisizo za kiserikali. Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi Mheshimiwa.

Pamoja na madhumuni niliyoyataja wakati nilipowasilisha mswada huu, pia wizara inatekeleza ahadi ya Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliyoitoa wakati alipozindua Baraza hili tukufu kwamba serikali yake itaanzisha Baraza la Vijana Zanzibar. (*Makofi*).

Mjadala wa mswada huu unakwenda sambamba na maandalizi ya Kanuni ya uendeshaji wa Baraza, ambazo zitazingatia maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wajumbe ikiwemo utaratibu wa kutoa fomu za uchaguzi. Idara za Baraza zitaanzishwa na Baraza lenyewe kwa mujibu wa mahitaji na uwezo wa Baraza, sio Waziri au mtu mwengine yeyote.

Sifa za Katibu Mtendaji wa Taifa zimewekwa kama ilivyoshauriwa na Kamati ambazo awe Mzanzibari, awe angalau na shahada ya sayansi ya jamii au sheria, uzoefu wa masuala ya vijana na uongozi na awe muadilifu. Na katika ngazi ya shehia na wilaya angalau awe na elimu ya kidato cha nne pamoja na sifa nyengine zilizotajwa.

Mhe. Spika, nikiendelea na Mhe. Ashura Sharif Ali alizungumzia juu ya zawadi zinazokusudiwa katika sheria hii ni zawadi gani. Zawadi zenye nia ya kusaidia kuendeleza utekelezaji wa kazi za Baraza kwa mujibu wa sheria kama vile kompyuta, gari, baiskeli na kadhalika, sio mapesa wala mapato ya kificho. (*Makofi*).

Uwakilishi wa wanafunzi uliokusudiwa hapa ni wanafunzi wa vyuo vikuu. Wizara haina nia ya kuingilia uamuzi wa Baraza. Wizara itakuwa mshauri tu wa Baraza hilo wala sio muamuzi wa vijana. Wizara kazi yake ni kutoa ushauri na ushauri Waheshimiwa Wajumbe si jambo baya. Ushauri unatoka kwenye misikiti, majumbani, kwenye hadhara na kadhalika.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwa Mhe. Hija Hassan Hija. Ushauri wake tumeupokea na tutaufanyia kazi. Wizara inakubali

kuongeza kifungu cha 3(g), kuongeza maneno:

"iliyoidhinishwa na Baraza kwa madhumuni ya Baraza"

Mtandao wa elimu ni mtandao wa elimu wa vyuo vikuu kifungu cha 21 (2), Katibu Mtendaji limeondoshwa na kuwekwa Baraza la Utendaji litakaloidhinisha fedha. Kwa vile Baraza halitokuwa na uwezo mkubwa wa kuajiri, kwanza wataanza maafisa wa vijana wa wilaya kuwa makatibu wa Baraza la Wilaya. Kadri Baraza litakavyopata uwezo na nguvu litaajiri kwa ajili ya mahitaji yake. Wizara itasimamia maofisa hao kutoingilia Baraza. Ushauri wa kupeleka majina matatu kwa Mhe. Rais kwa mujibu wa sifa zilizotajwa umekubaliwa tena sana.

Ushauri wa kuwaalika wataalamu serikalini na taasisi binafsi kama ilivyoshauriwa umekubaliwa. Tunakubaliana na ushauri wake wa kuachana kabisa na kuweka rehani, hakuna mambo ya rehani na ushauri wake wa kuondoa fedha zisizohitajika umezingatiwa.

Mhe. Spika, naomba sasa nimjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Nakubaliana na ushauri alioutoa kwa mujibu wa sheria kijana yeyote awe mwanachana au kiongozi wa Baraza. Atakayedhihirisha siasa ya chama chake ndani ya Baraza atachukuliwa hatua kama ilivyoainishwa.

Katibu wa Shehia anachaguliwa na mkutano mkuu wa Shehia na Katibu Mtendaji wa Taifa anateuliwa na Mhe. Rais na sio msimamizi wala msemaji wa Baraza. Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza ambao wanachaguliwa na vijana wenyewe ndio wasimamizi. Katibu Mtendaji ni mtendaji tu ambaye atafuata maelekezo ya Mwenyekiti na makamo wake.

Mhe. Spika, nikiendelea naomba sasa nimjibu Mhe. Hassan Hamad Omar. Yeye aliuliza *ZYC* maana yake nini. Ni *Zanzibar Youth Council*, kwa Kiswahili ni Baraza la Vijana la Zanzibar.

Kwa mujibu wa sheria hii yeyote atakayevunja sheria hii atachukuliwa hatua za kinidhamu kama kamati ya nidhamu itakavyoona inafaa. Taarifa ya siri iliyokusudiwa hapa ni zile taarifa ambazo muda wake wa kutolewa bado mjumbe anaanza kuzisema mabarabarani. Kwa kweli hilo halitokubalika na wakati wake ikiwa bado haujafika kutolewa nje. Haina maana viongozi au wanachama kufichwa lolote katika Baraza lao isipokuwa utaratibu wa vikao tu kuheshimiwa.

Tabia mbaya Mhe. Spika, ni zile tabia zilizo kinyume na mila na silka na utamaduni wa Zanzibar kama itakavyothibitishwa na Kamati ya Nidhamu ya Baraza ambayo wataiunda wenyewe vijana. Kifungu cha 31 (1) ni kifungu kinachozungumzia kuanzishwa kamati ya nidhamu ya Baraza.

Suala la uwiano limezingatiwa na mswada huu kwa kila eneo linalohusu uwakilishi. Kwa mfano Mwenyekiti akiwa mwanamme, makamo awe mwanamke. Aidha, kwenye Baraza la Watendaji kati ya wajumbe saba angalau watatu wawe wanawake, na sisi tuingie tuonekane.

Mhe. Spika, nikiendelea na Mhe. Asha Bakari Makame. Mhe. Asha tunamshukuru kwa ushauri wake tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir, naomba nikuthibitishie kwamba mara sheria itakapopitishwa tu Kanuni zitaandaliwa haraka haraka na hatua za kuundwa Baraza zitafuata.

Aidha nikubaliane na ushauri na maoni aliyoyatoa yatafanyiwa kazi ikiwa kualikwa Waheshimiwa Wawakilishi wanaowawakilishi vijana waliomo ndani ya Baraza hili.

Kifungu cha 22 (2) kimefanyiwa mabadiliko kwa mujibu wa sheria na utaratibu utakaotumika ni ule ule wa ukaguzi wa fedha za serikali. Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu atafanya ukaguzi katika ngazi yoyote atakayoona inastahiki, kama wilaya, taifa au kama shehia.

Suala la mgao wa fedha ngazi ya shehia na wilaya asilimia itawekwa katika Kanuni zitakazoandaliwa za kusimamia mwenendo wa fedha. Waziri atashauriana tu na vijana wenyewe, au vipi, pia nalo hilo halitakiwi.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwa Mhe. Panya Ali Abdalla. Mhe. Spika, ninamshukuru Mhe. Panya Ali Abdalla, kwa ushauri wake alioutoa na pia utafanyiwa kazi.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali, ninamshukuru sana kwa maoni yake. Jumuiya za Vijana ziliopo hazikushindwa kufanya kazi zake lakini sisi hatuundi jumuiya, tuna mswada hapa, isipokuwa kila jumuiya ziliopo sasa zina lengo mahususi za kuundwa kwake. Baraza litawaunganisha wote na litakuwa na kauli moja ya vijana na ndilo litakalokuwa msemaji wa vijana wote, hatutegemei kuwa tutaharibu fedha za serikali kwa kuunda Baraza la Vijana.

Lengo la mswada ni kumzuia kijana yeyote kuingiza itikadi ya chama chake ndani ya Baraza, sio kuwazuia vijana na siasa. Nje ya Baraza hawazuiwi, lakini wanapokuwa kwenye Baraza lenyewe siasa isiletwe, nje ya Baraza kila mmoja aendelee na itikadi yake.

Mhe. Spika, naomba sasa nimjibu Mhe. Amina Iddi Mabrouk. Shukurani kwa maoni yake aliyoyatoa tumeyapokea Baraza la Vijana, uongozi wake ni miaka

mitatu. Lengo la kumzuia kijana mwenye umri wa 35 kutogombea ni kuhakikisha kuwa kijana anakuwa kiongozi ndani ya miaka mitatu bila ya kupita umri wa miaka 35. Na mimi ninamshukuru Mhe. Amina Iddi Mabrouk, alivyosema kwamba mara nyingi nilikuwa ninadaiwa Baraza la Vijana hapa, lakini ninalileta Baraza la Vijana sasa inakuwa goe goe kidogo kidogo.

Mhe. Spika, sasa ninakuja kwa Mhe. Rufai Said Rufai. Mhe. Spika, nakubaliana naye kwamba katika utekelezaji wa sheria hii ni lazima tuanze na ngazi ya sheria ili kupata wajumbe wa Wilaya na kitaifa. Umri huo umezingatia sera ya maendeleo ya vijana na miongozo mbali mbali ya kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania.

Nakubaliana na ushauri wake alioutoa, taasisi binafsi zitaalikwa. Mzanzibari na tafsiri ya sheria ya Mzanzibari Mkaazi ya Zanzibar Nam. 5 ya 1985, Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa vijana ni wasimamizi wa sera na sheria zinazohusu vijana. Sheria itafuatwa, wao ni washauri tu. Vijana wenye ulemavu kifungu hicho kimerekebishwa na sasa hivi kimekuwa na Umoja wa Watu Wenye Ulemavu watateua wawakilishi wao na sio Waziri, wenyewe watateua vijana wenye ulemavu.

Kifungu cha 10 (5) kimerekebishwa na wajumbe wa mkutano mkuu sio wanachama wote. Kifungu cha 30 cha mswada huu kinazungumzia akidi ya mkutano. Kwa vile Baraza halijaanzishwa kazi ya utaratibu itaanza Idara ya Vijana. Suala la kuajiri ni Baraza na sio wizara, sheria itasimamiwa kikamilifu.

Mhe. Spika, sasa ninakuja kwa Mhe. Mussa Ali Hassan. Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mussa Ali Hassan, kwamba wakati ndugu yangu unakubadilisha, na tusipokwenda na mabadiliko hayo tutaachwa nyuma. Tupo kwenye karne ya sayansi na teknolojia. Suala la kutathmini mchango wa elimu ni muhimu. La msingi ni kuandaa vijana waadilifu na wazalendo. Ushauri wake Mheshimiwa umezingatiwa.

Mhe. Spika, sasa naomba nimjibu Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii. Ninamshukuru sana kwa ufafanuzi alioutoa na ushauri wake ninauzingatia. Na jengine zuri zaidi ninalotaka kulisema kwamba; tangu Kamati hii ipate Mhe. Mgeni Hassan Juma kuwa ni Mwenyekiti, tunashauriana na tunakwenda vizuri, na ninamshukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Abdi Mossi Kombo, ushauri wake tumeupokea kuhusu uwezo wa kuliendesha Baraza. Litakuwa huru kutafuta nyenzo na vitendea kazi ndani na nje ya Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub, ninampa pongezi za pekee kwa namna alivyoupokea mswada huu na ushauri wake alioutoa, lakini naomba nimwambie Makao Makuu ya Baraza kwa kila ngazi husika yatawekwa na Baraza litakapoanzishwa. Aidha, vikao vya Baraza ngazi husika pia vitaamuliwa na Baraza husika wapi watafanya vikao vyao, kama wilayani, taifani, kama kwenye shehia na kadhalika.

Mwisho Mhe. Spika, kulikuwa na Waheshimiwa Wajumbe ambao wamenileta kwa maandishi, lakini kwa bahati nzuri wameunga mkono hoja hawana wasi wasi wowote, ambao ni Mhe. Suleiman Hemed Khamis na wengineo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii, na pia naomba niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yao waliyoitoa, wale waliochangia na waliokuwa hawakupata nafasi ya kuchangia, najua nia yao yote ni moja; ni kuuweka mswada huu wa kuanzishwa kwa Baraza la Vijana.

Mwisho Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri kwa majumuisho hayo. Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaoafiki hoja ya mswada huu wanyanyue mikono. Wasioafiki. Walioafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu. Ahsante.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1 Jina Fupi na Tarehe ya Kuanza Kutumika

Kifungu 2 Ufafanuzi pamoja na Marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Baraza la Vijana la Zanzibar

Kifungu 3 Kuanzishwa kwa Baraza la Vijana

Kifungu 4 Uanachama wa Baraza pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tatu

Malengo na Uwezo wa Baraza

Kifungu 5 Malengo ya Baraza pamoja na marekebisho yake

Kifungu 6 Kazi za Baraza pamoja na marekebisho yake

Kifungu 7 Uwezo wa Baraza pamoja na marekebisho yake

Kifungu 8 Uwezo wa Waziri

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na kwa sababu nasimama mtu wa kwanza naomba nimpongeze na kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa uungwana wake kama kawaida yake, amefanya majumuisho vizuri na ameturidhisha katika hoja nyingi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo machache ambayo ningeomba ufafanuzi na nimeanzia katika kifungu hiki.

Pia, Mhe. Mwenyekiti, tunaomba tupate muongozo wako, kwa sababu katika majumuisho kuna waraka wa mapendekezo ya marekebisho ambayo tumepewa, lakini una saini ya Mwenyekiti wa Kamati. Kwa hivyo, haya ni

mapendekezo ya marekebisho ambayo yamependekezwa na Mwenyekiti wa Kamati.

Lakini yako baadhi ya maeneo ambayo kidogo naona hayamo katika jaduweli la marekebisho lakini Mhe. Waziri katika majumuisho yake kayakubali. Kiutaratibu najua kwamba tutachukua yale ya Waziri ya mwisho, tutaweka katika kumbukumbu kwanza kwamba tunapokea yale maelezo ambayo kayatoa Mhe. Waziri.

Sasa katika hayo Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 8 nilipokuwa nikichangia nilipendekeza kwamba lile neno "maelekezo" lililokuwepo pale, kwamba Waziri anaweza kutoa maelekezo na ushauri, nilipendekeza lile neno "maelekezo" liondoke, badala yake ibakie Waziri anaweza kutoa ushauri.

Mhe. Mwenyekiti, katika majumuisho yake Mhe. Waziri kasema kwamba Waziri kazi yake itakuwa ni kushauri tu, lakini hakuwa wazi zaidi kwamba amekubali mapendekezo niliyokuwa nimeyatoa kwamba na hili liondoke. Kwa hivyo, nilikuwa nataka nipate maelekezo yake, halafu niweze kuridhika kuwa tuendelee au tusiendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye kwamba neno "maelekezo" litoke.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Namshukuru Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti. Naomba tuendelee.

Kifungu 8 Uwezo wa Waziri pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Nne

Muundo na Vyombo Vinavyounda Baraza

Kifungu 9 Baraza la Vijana Taifa pamoja na marekebisho yake

Kifungu 10 Mkutano wa…

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 10 nilipokuwa nikichangia nilitoa mapendekezo kadhaa ya marekebisho, mengi yamezingatiwa katika maelezo ya Mhe. Waziri, lakini nilikuwa naomba kidogo tuwekewe sawa ili turidhike kwamba katika ku-*record* mswada huu tunaupitishaje tuwe tumekaa vizuri.

Kifungu cha 10(3) Mhe. Mwenyekiti. Kifungu hiki kinazungumzia,

"Mkutano mkuu taifa utakuwa na wanachama wafuatao waalikwa ambao hawatokuwa na haki ya kupiga kura:

(a) Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana ya masuala ya vijana Zanzibar,

(b) Mkurugenzi wa Idara inayohusika na masuala ya vijana Zanzibar, na

(c) Watendaji wawili wa serikali ambao wataalikwa kutokana na utaalamu wao ili kuunga mkono Mkutano Mkuu Taifa".

Sasa marekebisho ya Kamati tuliyopewa hapa yamesema, kuongeza maneno na taasisi zisizo za kiserikali na watu mashuhuri kulingana na maudhui ya mkutano husika. Mhe. Waziri, katika majumuisho yake kalizungumza sana kukubali ushauri wa kuwaalika wengine. Lakini mchango wangu na Wajumbe wengine Mhe. Mwenyekiti, ulikuwa una malengo mawili.

1. Kwamba kualikwa kuwe wazi kama ilivyotajwa hapa.

2. Tulisema kwamba hili la kushurutisha hawa waliotajwa hapa kuwa ni lazima waalikwe, hili lirekebishwe.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hivi ilivyokaa ni sawa sawa hawa ni waalikwa wa kudumu na hata kwenye lugha ya Kiingereza katika mswada neno lililotumika limesema,

"*The National General Assembly shall have the following invited members...*"

Sasa nilipokuwa nikimsikiliza Mhe. Waziri, kaniridhisha upande mmoja kasema hawa jukumu lao ni kusimamia sera na jukumu lao litakuwa ni kushauri. Lakini ukikisoma hiki kifungu ambacho kimeandikwa kimewanyima haki ya kupiga kura tu, lakini kwa ile kufanywa kuwa ni waalikwa wa kudumu inanipa mashaka.

Sasa nilikuwa nataka tuelewane Mhe. Mwenyekiti. Ama kwa upande mmoja tuliongezee neno kwamba mkutano mkuu utakuwa na wanachama, au kwa lugha iliyorekebishwa, wajumbe wafuatao waalikwa ambao watakuwa ni washauri wa Baraza na hawatakuwa na haki ya kupiga kura, pamoja na yale maelezo mengine kwamba wanaweza kualikwa taasisi nyengine.

Au wasitajwe, liachiwe Baraza wenyewe kama tulivyopendekeza baadhi yetu kwamba mkutano mkuu wa taifa unaweza kumualika mtu yeyote kutoka serikalini, taasisi za serikali na watu mashuhuri kulingana na maudhui ya mkutano husika ili kulisaidia Baraza. Sasa moja wapo kati ya haya mawili Mhe. Mwenyekiti, litaweza kuakisi yale ambayo tulikuwa tumeyapendekeza.

Kama Mhe. Waziri, anataka kibakie sio vibaya, lakini lile neno liongezwe kwamba Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao waalikwa ambao watakuwa ni washauri kwa Baraza na hawatokuwa na haki ya kupiga kura, ili ieleweke kuwa wako pale kwa ajili ya kushauri tu.

Naogopa Mhe. Mwenyekiti, kuja kuiacha kama hivi ilivyo ikawa kama inawanyima haki ya kupiga kura tu, lakini kwa kutumia ushawishi wao na nguvu yao kutoka katika wizara ambayo ndio inabeba bajeti ya wizara hii, ikawa inatumia ushawishi wao pengine kulisukuma Baraza kufanya maamuzi sivyo ambavyo wenyewe lingependa. Kwa hivyo, nilikuwa nataka nimsikie Waziri katika hilo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu wowote ule, kwa vikao vyovyote vile waalikwa wanayo nafasi ya kutoa ushauri na inakuwa hakuna tatizo. Tatizo ni kupiga kura tu, ikifika wakati wa kupiga kura kwa sababu wao hawahusiki sio wajumbe, wanakuwa hawaruhusiwi kupiga kura, lakini kwa kutoa ushauri wanaalikwa makusudi kwa ajili ya kusaidia kutoa ushauri. Kama nimemuelewea vizuri Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, kimsingi unakubaliana na lile wazo la kwanza, kwamba waalikwa hawa wawe wanahudhuria pale kwa ajili ya kutoa ushauri na hawana haki ya kupiga kura.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Sawa Mhe. Mwenyekiti, nadhani hilo na likiingizwa na yale maneno ambayo yalikuwa yametajwa katika marekebisho yaliyokuwa yametolewa na Kamati, itakuwa sasa nimeafiki kile ambacho tulikuwa tumekitolea maoni Wajumbe. Sasa ikiwa tumeelewana hivyo basi tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tunaendelea.

Kifungu 10 Mkutano Mkuu wa Taifa pamoja na marekebisho yake
Kifungu 11 Baraza la Watendaji pamoja na marekebisho yake

Kifungu 12 Sekretarieti

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 naomba Mhe. Waziri kikae vizuri katika kumbukumbu zetu hapa, atuthibitishie kwamba yale maelezo aliyokuwa kayasema pale yanaingia ndani ya kifungu hiki, kwa sababu kama nilivyosema tunapata tabu kidogo katika waraka huu wa marekebisho ambao katuambia ndio unaotuongoza, lakini hili alilisema pale katika majumuisho yake, lakini humu halimo. Ni lipi Mhe. Mwenyekiti, ni lile linalosema;

Kifungu cha 12(1) kilichokuwa kinasema:

> "Kutakuwa na Sekretarieti ya Baraza ambayo itaongozwa na Katibu Mtendaji ambaye atateuliwa na Rais"

Wajumbe kadhaa nikiwemo na mimi tulipendekeza kwamba itolewe nafasi ya Baraza kupendekeza kwa Rais. Nashukuru Mhe. Waziri kalikubali. Kwa hivyo, kupelekwe majina angalau matatu, mwenyewe Mhe. Waziri kasema kwamba wawe na zile sifa zitakazokuwa zimetajwa ndani ya sheria. Nadhani ni sahihi.

Kwa hivyo, nadhani atueleze tu turidhike kwamba tofauti na hivi ilivyoelezwa humu ndani ya jaduweli la marekebisho kuwa tunachukua yale maelezo yake ya ufungaji, kwamba patarekebishwa hapa ili kuingiza lile neno kuwa kutokana na mapendekezo ya majina yasiyopungua matatu kutoka katika Baraza lenyewe, tukielewana hivyo tutafika pazuri.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nakubali kwamba yale maneno niliyoyatamka pale ndio yachukuliwe kwamba ndio sahihi kuwa vijana wataachiwa watoe mapendekezo yasiyopungua matatu ili kupelekwa kwa Mhe. Rais mwenyewe, ahsante.

Kifungu 12 Sekretarieti ya Baraza pamoja na marekebisho yake

Kifungu 13 Baraza la Vijana Wilaya

Kifungu 14 Mkutano Mkuu Wilaya pamoja na marekebisho yake

Kifungu 15 Kamati Tendaji Wilaya pamoja na marekebisho yake

Kifungu 16 Baraza la Vijana Shehia pamoja na marekebisho yake

Kifungu 17 Mkutano Mkuu Shehia

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, haya nitakayoeleza yanahusu vifungu vyote viwili kifungu cha 17 na cha 18. Nilipokuwa nachangia nilizungumzia kwamba katika vifungu hivi hasa kifungu cha 18, pametajwa Katibu wa Baraza la Vijana la Shehia, lakini nikasema kwamba hakutajwa anapatikana vipi, ni tofauti na wale wengine. Sasa katika majumuisho yake Mhe. Waziri alijibu kwamba huyu atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Vijana wa Shehia.

Sasa nilikuwa naomba tu kama ni hivyo ndio maana nimesimama katika kifungu cha 17, kwa sababu tukikipitisha hiki nitakuwa sina nafasi tena, kwamba pale kwenye kifungu cha 17(2)(c) niongeze basi ili ichukue yale maneno ambayo alikuwa kayatoa Mhe. Waziri, (c) ilivyo ilikuwa imemtoa katibu, imesema kuchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Shehia.

Sasa kama alivyosema yeye kuwa na katibu pia atachaguliwa na Mkutano Mkuu basi itajwe hapa, kwamba 'kuchagua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na tuongeze na Katibu wa Baraza la Vijana Shehia', nadhani tukiweka hivyo itakuwa sasa imechukua yale ambayo katujibu katika maelezo yake ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea kwamba kwenye (c) pale inaingia pamoja na Katibu wa Baraza.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimekubali tu, lakini tumeshafanya marekebisho.

Kifungu 17 Mkutano Mkuu Shehia pamoja na marekebisho yake

Kifungu 18 Kamati Tendaji Shehia pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Tano

Vifungu Vinavyohusiana na Fedha

Kifungu 19 Fedha za Baraza

Kifungu 20 Mwaka wa Fedha

Kifungu 21 Makadirio pamoja na marekebisho yake

Kifungu 22 Hesabu na Ukaguzi pamoja na marekebisho yake

Kifungu 23 Ada ya Uanachama pamoja na marekebisho yake

Kifungu 24 Kuwekeza Mfuko

Sehemu ya Sita

Mengineyo:

Kifungu 25 Nembo na Muhuri wa Baraza

Kifungu 26 Kanuni pamoja na marekebisho yake

Kifungu 27 Muda wa Uanachama pamoja na marekebisho yake

Kifungu 28 Utaratibu wa Mkutano

Kifungu 29 Uchaguzi na Taratibu za Kupiga Kura

Kifungu 30 Akidi

Kifungu 31 Taratibu za Nidhamu pamoja na marekebisho yake

Kifungu 32 Maazimio ya Baraza

Kifungu 33 Usawa wa Kijinsia

Kifungu 34 Uongozi wa Baraza

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, ilivyokua Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huo pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji basi Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na mswada huo katika kusomwa kwa mara ya tatu wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa kwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Spika: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa kazi nzuri mliyoifanya na sasa tunaendelea.

Mswada wa Sheria ya Amri ya Barabara (Marekebisho) ya 2013

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na katika orodha yangu nina jina la Mhe. Salma Mohamed Ali, karibu kwa mchango.

Mhe. Salma Mohammed Ali, hayupo. Majadiliano yanaendelea.

Sijui Mhe. Subeit Khamis Faki ndio anahangaika, inaonekana anatafuta dondoo ili achangie. *(Makofi/Vicheko)*

Mhe. Subeit Khamis Faki, karibu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa jioni hii ya leo na mimi kupata fursa ya kuchangia mswada huu wa sheria ya barabara.

Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi napenda niungane na wenzangu waliotangulia kuchangia kuwapa pole wenzetu wa Afrika ya Kusini kwa kufiliwa na Rais Nelson Mandela ambaye alikuwa ni mkombozi wa Afrika, na kumbukumbu yake itakuwa haisahauliki, nafikiri ulimwengu wote tutapata kujifunza kutokana na Rais wa Afrika ya Kusini Mhe. Mandela.

Mhe. Spika, tunajadili masuala ya barabara, ili kuweka sawa mambo yetu. Lakini Mhe. Spika, mimi kila siku huwa nazungumza suala hili na nitaendelea kulizungumza kama sisi ni wazuri wa kutunga sheria, lakini kuzisimamia sheria ndio tunakuwa na uzito. Mhe. Spika, kwa kweli wenzangu waliotangulia walizungumza na mimi nazungumza, kwamba sasa hivi ni ulimwengu wa utandawazi, sio ulimwengu wa kukaa tu ukakurupuka na kufanya mambo ambayo bila ya kukaa na kuyafanyia utafiti na kuyafanyia mipango ili kuona mipango imekaa sawa.

Mhe. Spika, kitendo kilichofanywa cha kuwatesa wananchi wa Zanzibar kutokana na usafiri wa magari ya daladala, kwa kweli sio kizuri. Kwa sababu ni vizuri sana kuweka mji wetu vizuri na kupanga mipango yetu vizuri ili kila mmoja akaona kuwa mji wetu umekaa vizuri. Lakini Mhe. Spika, watu wanatakiwa kwanza wakae ili wafikirie, wazingatie na waone kuwa mambo yamekaa sawa halafu ndio sasa muanze kutenda.

Mhe. Spika, kile kitendo cha kukurupuka tu tukaenda kuwahamisha wananchi pale Darajani kwenye sehemu ya magari, halafu tukawapeleka sehemu ambazo hazieleweki, kwa kweli sio kitendo kizuri.

Mhe. Spika, bahati nzuri kuanzia tangu juzi Mwenyezi Mungu katupa kidogo ahuweni ya jua, tuna nafuu kidogo, mvua inanyesha na watu kidogo wana nafuu. Lakini Mhe. Spika, utaona imani, leo anateremka mtu kwenye meli mgonjwa, anatokea Pemba ni mgonjwa na tusione kama sote tunaweza tukapata magari ya kupanda, wengine hawana magari wanatumia miguu yao. Wanakuja watu pale wanachukua mkokoteni na mizigo yao mpaka wanafika Darajani.

Leo mtu anashuka gari mgonjwa, anakwenda kupanda gari Michenzani, kusema kweli hatukupanga vizuri, na halafu hizo gari zenyewe huko zinakowekwa, zimewekwa kwa msongamano hazikuwekwa sehemu ambazo kuwa ni nzuri.

Mhe. Spika, leo ukienda Baraza la Wawakilishi kongwe pale, utaona msongamano wa magari, magari mpaka mengine yamefika Maisara, magari mengine matope matupu. Ukija pale Kisiwandui kwenye Makao Makuu ya CCM pale ndio kabisa vurugu tupu. Kwa kweli hatukupanga, tulikaa tu tukakurupuka na kuwafanyia watu mambo kama yale, sio vizuri kusema kweli. Tunatakiwa tujipange kwanza halafu ndio tuamue.

Kwa hivyo, mambo kama yale tunaitia aibu serikali, maana wanatukanwa viongozi wa serikali, tunatukanwa sisi Wawakilishi, unatukanwa wewe Mhe. Spika, kwa sababu maamuzi yale yanaonekana kama ni maamuzi tumeamua Baraza la Wawakilishi. Hiyo ilikuwa ni dibaji Mhe. Spika.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nilitaka kulizungumza, nimeona hapa katika kifungu cha 13 kuna maneno yameandikwa katika hii sheria kwamba Waziri atasababisha mpango wa ukaguzi utayarishaji kuhusiana na barabara zote za umma. Sasa Mhe. Spika, haya maneno mimi naona hayakukaa vizuri kama Waziri atasababisha. Labda ingekuwa waziri atatayarisha ukaguzi au mpango wa ukaguzi, lakini waziri atasababisha utayarishwaji wa ukaguzi. Naona hayakukaa vizuri.

Kwa hivyo, ningeomba kidogo haya maneno yawekwe vizuri ili hizi sentensi zisomeke vizuri na hii sheria yetu iwe nzuri zaidi.

Mhe. Spika, pia ningetaka ufafanuzi katika kifungu cha 18 ambacho ni 23(a),

Kifungu cha 23(a). (1)

"Kutokana na maombi ya mamlaka ya barabara, waziri anaweza kuweka masafa fulani kutoka katikati ya barabara maalum kuwa ni hifadhi ya barabara hiyo"

Mhe. Spika, hapa ningeomba nisaidiwe ufafanuzi, maana sikufahamu mimi kama waziri kutokana na maombi ya mamlaka ya barabara kuwa waziri anaweza kutenga nafasi katikati ya barabara. Kusema kweli sikufahamu naomba nifafanuliwe kama katikati ya barabara atatenga vipi iwe ni masafa fulani kutoka katikati hiyo kuwa ni barabara maalum kuwa ni hifadhi. Hiyo hifadhi itakuwa pale katikati ya barabara vipi.

Kwa hiyo, na huku chini zimebaguliwa, lakini sasa nilikuwa nataka nielewe, kwa sababu miye labda nimesema kutokana na ujenzi wa barabara labda tunataka kufuata wenzetu.

Kwa sababu wenzetu kule Bara wanakuwa wanaweka *road reserves* kwenye barabara, sasa zilikusudiwa hivi kuweka *road reserves* au ni ile sehemu ya kugawa barabara kati kati. Kama ni ugavi wa barabara katikati basi tusingeambiwa kwamba ni hifadhi ingekuwa ni ugawaji wa barabara, anaweza akatenga sehemu ya kuigawa barabara. Lakini ilivyowekwa hivi mimi sikufahamu.

Ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja anifafanulie zaidi hapa ili nielewe kama pamekusudiwa kitu gani, kama ni *road reserve* au ni ugawaji wa barabara. Kwa mfano kama Darajabovu sasa hivi kunajengwa barabara, lakini pale katikati inagaiwa kutokana na barabara hii na hii. Lakini pale haiwi hifadhi inakuwa ni ugavi wa barabara kutokana na barabara hii na hii, lakini imewekwa kama ni hifadhi ya barabara. Kwa hivyo, naomba hapa anipe ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nifafanuliwe kwenye kifungu cha 19 (2) kuna sentensi ambayo kuwa inasema hivi:

Kifungu cha 19(2) "Mtu yeyote au taasisi atakayekwenda kinyume na kijifungu (1) cha kifungu hiki atakuwa na hatia ya kutenda kosa na akithibitika atastahili adhabu ya faini ya shilingi mia tano elfu na sio zaidi ya shilingi milioni moja au kifungo ...."

Sasa nilikuwa nataka ufafanuzi maana wengine si Waarabu, wengine wanafahamu ni waarabu lakini wengine si Waarabu. Hizi mia tano elfu zinaandikwa hivi mia tano elfu, nawasikia kiti cha sheria hapa. Kwa hivyo,

nilikuwa nataka iwekwe sawa hii, walikusudia mia tano elfu au vipi au shilingi elfu milioni tano. Naomba na hapa nifafanuliwe nipate kufahamu zaidi.

Mhe. Spika, suala jengine ninalotaka kupata ufafanuzi kuna maneno hapa yamejirudia rudia. Hili neno, naona kama ni neno moja kwa miye ninavyolielewa. Sasa naomba ningepata ufafanuzi zaidi. Maneno yenyewe yanasema kwamba

Kifungu cha 16

> "20. Mtu yeyote anayepinga, anayeizuia, anayekwamisha, anayesumbua au kusababisha kuzuiwa ..."

Mhe. Spika, na haya mimi naona kidogo hayakunikalia sawa, maana kupinga na kuzuia ni jambo moja, kwa miye ninavyoelewa Kiswahili cha kwetu Micheweni. Sasa ningeomba kidogo na hapa haya maneno ningepata ufafanuzi, maana maneno karibu yote matatu yana maana moja. Kwa hivyo, na hapa je, ningeomba Mhe. Waziri aje atufafanulie atuwekee sawa zaidi ili tuweze kupata neno moja lililokuwa zuri. Maana mimi nampinga huyu asifanye au namzuia asifanye si neno lile lile moja. Naomba ufafanuzi zaidi.

Mhe. Spika, huu Mswada kwa kweli si mbaya ni mzuri isipokuwa kuna mambo fulani fulani yanatakiwa yawekwe sawa. Lakini wakati huo huo Mhe. Spika, ningetaka kupata ufafanuzi kama sisi tunarekebisha sheria hii. Sheria tukisharekebisha tutachukua muda hatujarekebisha tena, ningetaka Waziri anipe ufafanuzi kama sisi tunapotoa *tender* kwa makampuni yanapokuja yakapewa ujenzi wa barabara.

Kwa sababu kama alivyosema Mhe. Hija Hassan Hija, kwamba Micheweni na Vitongoji ni waathirika wakubwa wa ardhi yetu kuchimbuliwa kwa ajili ya kupata kifusi kwa ajili ya kufanyiwa barabara zetu. Hilo sio vibaya, lakini ningetaka nipate ufafanuzi hivi kutokana na hali hiyo ilivyo hivi haya makampuni kuna sheria gani kuwa leo tunarekebisha hatukuwawekea, kwa sababu makampuni haya yakishatuharibia zile ardhi zetu ndio yameshakwisha, wao wanakwenda zao hawarudi tena na wala hakuna sheria yoyote inayotungwa juu ya hili.

Halafu isitoshe hilo mbali, lakini wakati huo huo kuna barabara ambazo zitakuwa zimeshajengwa ni nzuri na tunazitumia. Leo makampuni yanakuja kutengeneza barabara nyengine, lakini barabara nyengine wanazokuja kutengeneza zile barabara zilizokuwa zimeshakuwa nzuri zinaharibiwa zote hazifai.

Kwa mfano, sasa hivi barabara yetu ya Micheweni haifai kabisa kwa kupita magari makubwa ya *H. Young* na *MECCO* na sasa hivi wameshaharibu, wameshakwisha sasa hivi wanafunga virago vyao, serikali inapata tena hasara ya kujenga tena mwanzo ujenzi wa barabara ile.

Sasa je, tunapitisha hizi sheria na katika hizi sheria tunazopitisha za barabara, tusiweke masharti ya kuwa atakayeharibu barabara aijenge barabara. Leo tunapitisha sheria hii tunaacha wazi hapa kesho tunataka kumshika mtu hatuna pa kumshikia, wakati sheria ndio tunaipitisha.

Mhe. Spika, naomba wakati tunaipitisha hii sheria Waziri akija atueleze kwamba kuna masharti gani kwa yule anayeharibu barabara. Ili iwe kuna sheria inayoweza kumbana akishaharibu barabara aweze kuitengeneza ili irudi, sio kwamba yeye anakuja anaikuta barabara imeshajengwa pamoja na kuwa anatujengea nyengine sio tena kwamba atuharibie na zile zilizopo. Kwa hiyo, akiharibu ile aweze kuirudisha ili iwe barabara ipo katika hadhi yake. Kwa hivyo, kifungu cha sheria mimi naomba kiwekwe ili tuweze kumbana mtu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nakushukuru sana.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze mchango wangu katika ukurasa wa 358 kifungu cha 2(3) kwenye tafsiri ya barabara za umma, mstari wa sita. Kuna maneno ambayo yametaja mifereji yote. Hapa namuomba Mhe. Waziri anifahamishe amekusudia nini. Kwa sababu wale wenzetu wa Bara mifereji ni misingi ama mitaro. Lakini yeye katika kifungu hicho kataja neno mitaro, lakini pana na mifereji.

Naomba Mhe. Waziri anifahamishe kwa sababu sisi Wazanzibari tukisema mifereji tunakusudia mifereji ya maji safi na salama. Sasa kwa sababu hii Shekhe, Alhaji pengine kakusudia katika barabara kuweka mifereji ili wananchi wakiona kiu wapate maji wanywe au kakusudia ikifika kipindi cha sala watu watilie udhu waende wakasali.

Hapa naomba kidogo Mhe. Waziri, anifahamishe. Mhe. Spika, ingelikuwa hakutaja mifereji halafu akataja na mitaro ningelisema labda kafuata ile lugha ya wenzetu, lakini kataja mitaro halafu kataja na mifereji. Kwa hivyo, namuomba anifahamishe hapa kakusudia nini.

Mhe. Spika, pia katika Mswada huu kumetajwa vifungu vingi vinavyorekebisha kiwango cha adhabu ya malipo ya fedha, ambayo ni marekebisho ya sheria kongwe na ni sheria ya zamani na adhabu hizi zilikuwa

zikifanya kazi. Lakini kutokana na kuporomoka kwa sarafu yetu adhabu hizi zilikuwa hazina nguvu tena na ndio maana leo hii panawekwa adhabu nyengine tena zile zile za fedha.

Sasa Mhe. Spika, sasa hivi hizi adhabu zilizowekwa tunaziona ni kubwa lakini itafika kipindi pia zitakuwa ndogo. Sasa hapa ninaushauri kidogo Mhe. Spika, naomba viwango hivi vya adhabu viwekwe kwenye kanuni kwamba Mhe. Waziri, aweze kubadilisha viwango hivi vya adhabu kulingana na wakati tuliona na wakati uliopo. Kwa sababu ikiwa pesa imeshashuka thamani aweze kurekebisha. Lakini vifungu hivyo visitumike mpaka pale vitakapopitishwa kwenye Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayohusika na masuala hayo kama ya barabara kupata baraka zake.

Mhe. Spika, vile vile mswada huu hauoneshi kuleta marekebisho ya mambo mawili, ambayo kwa siku ya hivi karibuni yamekuwa ni jambo la kawaida, uzururaji wa wanyama barabarani. Hili limekuwa ni tatizo kubwa na limekuwa ni kero. Hata viongozi wetu wa juu wamelisemea sana suala hili, akiwemo Mhe. Rais wa Zanzibar, lakini bado suala hili linaendelea. Mimi nilifikiria huu Mswada utakuwa ni suluhisho wa tatizo hilo, lakini haukuonesha kifungu chochote kinachorekebisha masuala hayo.

Jambo jengine ambalo halipendezi ni tabia ya wananchi kujiwekea wenyewe matuta yanayoudhi sana. Hili pia hatuoni kuelezwa katika Mswada huu. Ushauri wangu kwanza Wizara itoe elimu kwa wananchi wafuate utaratibu na vile vile iweke mikakati ya kuzuia tabia hii isiyopendeza. Pia katika ukurasa wa 361 kifungu cha 19(1) na (2) hapa kidogo mimi nataka Mhe. Waziri, anifahamishe. Naomba nivinukuu kama hivi:

> "19. (1) Mtu ambaye atakuwa hakuridhika na maamuzi ya Idara ya malipo au ya kiwango cha fidia yanayotokana na tendo lolote au jambo lolote lililofanywa na Idara kwa mujibu wa uwezo wake chini ya kifungu cha 13, atalazimika kupeleka ombi la maandishi kwa utaratibu uliowekwa na Sheria ya Fidia.
>
> (2) Endapo itatokezea kutokuwepo kwa Sheria ya Fidia mtu huyo atalazimika kufungua shauri Mahakamani."

Mhe. Spika, hapa mimi kidogo pananichanganya kwa sababu hapa tumeshaambiwa sheria ya fidia, lakini kifungu cha chini kinasema kwamba endapo kama itatokezea kutokuwapo kwa sheria ya fidia, ina maana ilikuwa imeshajulikana kama haipo. Sasa ilikuwa kuna haja gani ya kuweka hichi, bila shaka wakati Mswada huu umeletwa na Mhe. Waziri, ndiye aliyeelezea kwamba endapo itatokezea kutokuwepo, alikuwa keshajua kwamba hakipo.

Halafu vile vile, napenda nifahamishwe kwamba hii sheria imepitishwa leo au ndiyo inatarajiwa kupitishwa leo, lakini kuna watu tayari wameshajenga majumba yao. Sasa katika yale maeneo ambayo tayari wananchi wameshajenga majumba yao pia sheria hii itawaandama.

Kwa sababu wametangulia kujenga wao kabla ya barabara. Wale ambao barabara itapita baadaye bila shaka watakuwa wameshajua kama kuna sheria fulani, lakini wapo waliokuwa wameshajenga na barabara ndio zinajengwa mle ambamo kuna majumba yao. Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi sheria hii kwao wao itakuwa vipi.

Mhe. Spika, nakushukuru, Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nikushukuru wewe kwa jinsi unavyoliendesha Baraza hili kwa umakini wa hali ya juu pamoja na watendaji wako wa Baraza hili.

Mhe. Spika, naomba kuuchangia Mswada huu wa Kurekebisha Amri za Barabara Sura 134. Mimi kwanza nataka kufahamu Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake wakuu wametembelea lini vituo vipya vilivyofunguliwa hivi majuzi vya daladala.

Hapa Mhe. Spika, nitakuwa mkaidi, tupo hapa kwa niaba ya wananchi. Asubuhi nilisema kwamba hichi chombo ni cha wananchi, wananchi wanapata shida, mgonjwa anatoka Bububu anafikia kwa Bakhressa atafikaje Hospitali pale, hana haki mwananchi yule. Anatoka Bububu hospitali yenyewe pengine akienda dawa yenyewe haipo, na pengine mgonjwa wa macho akienda pale anaambiwa kituo kimehamishwa kipo KMKM. Kweli ndio tunawafanyia haki wananchi namna kama hii.

Mhe. Spika, Waziri na Naibu Waziri watakapokuja watueleze, vituo vipya hivi vilivyofunguliwa majuzi mmevitembelea lini na watendaji wako. Leo vituo gari zinasimama kiholela kabisa hujui mwanzo wala mwisho, leo Ofisi yetu ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndio chama kikubwa kuliko vyote Tanzania imezongwa pale, hujui pa kupita wapi, anapita kiongozi mkubwa atapitaje pale, huu si utaratibu.

Leo kituo hujui wapi mtu pa kwenda kujisaidia, hujui wapi mtu anaweza akajificha mvua, wale ni binaadamu. Leo askari wanalia wanatushtakia Waheshimiwa wanatwambia hivi mnavyofanya nyie viongozi ndio ndivyo.

Kuna mambo matatu Mhe. Spika, ni sadaka ya njia, ukikikuta kitu kiovu ukakiondosha, ukienda ukatizama chini vile vile ni sadaka. Ule ni uovu

uliofanywa, haielekei hasa. Baada ya hapo naomba kuchangia kifungu cha 23 (1). Hapa nataka kufahamu kweli uwezo serikali inao baada ya kupitisha sheria hii kwenda kuwavunjia nyumba waliokwishajenga, wakati nyumba zimeshajengwa.

Hapa nataka kuja kuelimishwa, tayari watu wameshajenga nyumba zao kama eneo la Bububu, Magomeni, Kwahani, leo ukienda Wizarani kutaka kiwanja mrundikano uliokuwepo wa habari ya viwanja, utakwenda mpaka kiatu chote kitalika soli kiwanja hukipati na hao waliokuwa navyo wanataka kunyang'anywa.

Nije kwenye habari ya mifugo Mhe. Spika, hapa miye sitokubaliana na mchangiaji mwenzangu aliyepita. Adhabu hii ya kulipishwa shilingi laki tano mpaka milioni moja kwa miezi mitatu, huu ni uonevu, tena ni uonevu wa hali ya juu. Leo ng'ombe kakata kamba, punda kakata kamba, mbwa kapita barabarani kweli hilo ni kosa la mfugaji kweli hilo. Wananchi watatufahamu vipi tunapitisha sheria kama hizi.

Mhe. Spika, kabla ya hapo mimi pia ni mfugaji wa ng'ombe, Uwandani. Ng'ombe wanafuata barabara kutokana na joto wakalala akakimbia zizini. Sasa kwa kuwa ng'ombe kakaa barabarani uje utoleshwe shilingi laki tano, mimi sheria hii sikubaliani nayo Mhe. Spika, kabisa. Uwanja wetu wa ndege kuna wakati kapteni alipata shida mbwa alikatiza katikati ya barabara ikapigwa breki ghafla. Sio mazungumzo ya kubahatisha, nazungumza kitu nilichokiona.

Sasa kweli hivi tunawafanyia wananchi haki kweli na tunachokizungumza humu ndani, wananchi watatuonaje kuhusu mifugo na wao wana haki kuhusu nchi hii. Mimi yameshanikuta, wamemkuta ng'ombe Baraza la Mji wakamchukua mmoja anamvuta mkia, mwengine anamvuta kamba ilikuwa ni mwezi wa Ramadhani, huku ng'ombe anachanika huku mavi yanamtoka, hata hayasemeki Mhe. Spika. Haiwezekani kufanya mambo kama haya kwa sababu na wale wafugaji na wao ni watu.

Baada ya hapo Mhe. Spika, nije kwenye barabara zetu sasa. Sijui tunakwendaje, ukienda njia ya Mwera matuta 24. Skuli zetu huku watoto wanapoteza maisha imekuwa hawana haki. Kima wa Jozani wana thamani kuliko wananchi wa jimbo la Muyuni hasa Pete, wengine wanajengewa matuta wengine wasijengewe matuta.

Tuje barabara ya Mkunazini iliyojengwa kupitia mfuko wa Mhe. Mbunge. Barabara imejengwa imeachwa mashimo, ni hatari kwa usalama wa watu wanaotumia njia kwa miguu. Ikiingia gari haitoki, sasa bora isingejengwa

barabara ile. Tunajenga kitu kizuri baadaye tunashindwa kukiendeleza. Tuje barabara ya Kisiwandui pale ukipinda kuna matuta zaidi ya 24, ishalika hasa barabara, kwani hatuoni tukipita pale. Nataka kumpa taarifa ndugu yangu *Cosmas* aliangalie lile.

Tuje barabara ya Forodhani kuna mashimo maana yake hatari yamewekwa majiti hasa maana asije akatumbukia mtu, kwa hivyo pamewekwa alama.

Nije na barabara yangu ya jimboni kwangu Jambiani nilikuwa nikipiga kelele kama mkwezi wa minazi siku zote. Barabara zile kuna sekta ya utalii wanapata shida watalii, kuna hoteli zaidi ya 15 kule. Leo barabara tokea ilipoanza dunia mpaka leo hata kutiwa kifusi, anasubiriwa Mwakilishi na Mbunge waliofanya mambo yale. Wale watu wakiona mazingira mazuri watakuja kuwekeza zaidi. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, naomba nikae kitako.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano bado yanaendelea kama bado wapo wachangiaji, inaonekana hakuna. Sasa sina hakika kama Waziri yupo tayari, tuna muda karibu wa saa moja hivi tunaweza tukamaliza kazi hii, nadhani hatuwezi. Mhe. Naibu Waziri upo tayari kumsaidia Waziri sasa hivi. Uko tayari, karibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema. Pili, mimi naomba kuchukua nafasi hii mimi binafsi pamoja na wananchi wenzangu wa jimbo la Chwaka kusema kwamba tunaunga mkono marekebisho ya Mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa ujumla kuhusiana na yale mengi ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameweza kuonesha hisia zao. Naamini kwamba madhumuni ya mabadiliko haya sote tukiwa mashahidi asubuhi hii tumeyaweza kuyasikia vizuri wakati Mhe. Waziri, akitoa taarifa yake katika uwasilishaji wa Mswada huu.

Mabadiliko haya yamekuja kutokana na wakati na mahitaji halisi ya nchi yetu wapi ambapo tulipo hivi sasa na wapi ambapo tumelenga kwenda katika hatua za kimaendeleo.

Mhe. Spika, wengi Waheshimiwa Wajumbe ambao wamejaribu kuuliza na kudadisi mipango ambayo iliyopo kuhusiana na mabadiliko ya sheria hii wakijiuliza kwamba hivi mabadiliko haya ambayo yameletwa na serikali kama yanaendana sambamba na ile mipango ya serikali ya mpango mkuu wa usafiri.

Mhe. Spika, ukweli kwamba mabadiliko haya ni sehemu ya mpango mkuu wa usafiri wa Zanzibar. Ukiangalia hatua zilizochukuliwa katika uimarishaji wa Uwanja wa ndege, hatua ambazo serikali inachukua katika uimarishaji wa Bandari, lakini pia hatua ambayo serikali inachukua katika utafutaji wa fedha kwa ajili ya mradi mkubwa wa barabara zinazoingia mjini, tabaan utaona ni uhakika kwamba marekebisho haya yanakwenda sambamba na mipango ya serikali katika mpango mkuu wa usafiri hapa Zanzibar.

Suala jengine Mhe. Spika, lilizungumziwa sana ni suala la fidia, naamini Mhe. Waziri, atakapotoa katika majumuisho yake atakuja na *data*. Lakini utaratibu uliopo kwamba sisi tunafuata maelekezo ya sheria za nchi ziliopo. Sheria ya Ardhi ya mwaka 1992 ndio kielelezo muhimu ambacho kinatuelekeza sisi juu ya utaratibu na mfumo wa kufuata katika ulipaji wa fidia hizo.

Sera yetu ya serikali ipo wazi, kwamba hatutovunja nyumba ya mtu yeyote Zanzibar kwa kupitisha mradi wowote bila ya kumlipa mtu fidia yake hiyo. Tunatambua kwamba kuna fidia za vipando na miti tunachelewa. Lakini sababu zetu za msingi ni kutokana na ukosefu wa fedha.

Lakini ushuhuda ambao Waheshimiwa Wajumbe wameutoa pamoja na mawazo yao kuona kwamba katika ule utaratibu wetu tunaolipa fidia basi ni busara kama vile tunavyohusisha Masheha na wao pia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi nao tutawahusisha, hili hatuna tatizo nalo. Naamini kwamba Mhe. Waziri atalitolea maelezo mazuri lakini sisi kama Wizara tunakubaliana nalo. Kwa sababu tukiwa tunamuhusisha Sheha kama kiongozi katika shehia husika hatuna sababu ya kumkataa Mheshimiwa Mwakilishi kumuhusisha akiwa na yeye kiongozi katika jimbo husika.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa kwa mapana ni suala la hifadhi ya barabara. Kwa mujibu wa sheria iliopo hivi sasa, sheria ambayo imetungwa mwaka 1927 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1958. Imeeleza upana wa hifadhi ya barabara ambapo kwa barabara kubwa ni futi 25 ukizigawanya kwa mita unaweza ukapata takriban mita 8. Bahati mbaya iliyopo kwamba wananchi wengi wameweza kuvamia katika maeneo haya hata hizo mita nane hazitimii.

Kwa hivyo, malengo ya serikali ni kuona kwamba kwanza tunaisimamia sheria iliyopo, lakini tunafanya mabadiliko haya ili kufikia mahitaji ya kutanua barabara haja itakapotokea siku za usoni.

Suala jengine ambalo limeulizwa ni kwamba utaratibu huu wa *road reserve* unaanzia wapi. Napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba malengo

yetu ni kuanza na barabara mpya ambazo hivi sasa zinajengwa kwa mfano barabara zile za Kaskazini Pemba maeneo ya vigingi vya kuonesha hifadhi ya barabara tumeshaanza na mradi wetu wa pili ni kuhakikisha kwamba barabara zote zilizokuwepo mashamba barabara kubwa tunaweka vigingi hivyo.

Kwa upande wa mjini matarajio yetu ni kuona kwamba ule mradi mkubwa wa *town entry roads* utakapokamilika, na kwa sababu itakuwa tayari tumeshalipa fidia, *corridor* imekuwa kubwa, tutahakikisha kwamba maeneo yale hatutoi mwanya kwa wananchi wetu kuyavamia tena, isipokuwa tutaya-*cover* kwa mujibu wa vigezo na ukubwa wa barabara zinazohusika kulingana na masharti kama vile sheria yetu tutakavyokuja kufanya mabadiliko kwa kuona barabara ipi itapewa upana gani, kama hifadhi yake kwa mujibu wa *category* ya ile barabara yenyewe.

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumzwa ni suala la adhabu. Sote tunakiri kwamba adhabu zilizomo katika sheria hii kwa hivi sasa zimepitwa na wakati. Tunalazimika kufanya mabadiliko hayo ili kwenda na wakati. Kwani kwa hakika adhabu hizi nyengine kwa hivi sasa sio adhabu tena isipokuwa ni jambo ambalo haliwezi kumuonesha mkosaji yale machungu yaliyotarajiwa kwamba siku ya pili asirejee yale makosa kulingana na ile adhabu ambayo angekuwa amepewa mwanzo.

Suala jengine Mhe. Spika, limezungumziwa suala la alama za barabarani zilizopo barabarani. Hili Mhe. Spika, lina maeneo mawili, kuna eneo ambalo sisi kama wizara tunachotaka kufanya sisi kujenga ama kuchora, lakini upande wa pili tuiombe jamii nayo itusaidie kutunza miundombinu hiyo. Barabara nyingi ambazo zinajengwa, lakini zikikamilika alama zinakuwepo, mabango yale yanayoashiria kwamba huku pita, usizidi *speed* hii, mbele kuna mpindo, kuna skuli, na nyenginezo.

Lakini haya yote bahati mbaya kwamba baada ya kipindi kifupi tu wenzetu wanakuwa wanayaharibu, wanachukua vyuma vile wanakwenda kuuza kama vyuma chakavu, athari zinarudi kwa watumiaji wengine wa barabara. Na ni kweli barabara zetu zitashuka viwango hasa kwa wageni ambao wanatumia barabara za Zanzibar hawawezi kuthamini jitihada zetu, ikiwa wananchi wenyewe hatukuonesha shukurani kwa serikali katika uwekaji wa miundombinu ya barabara hasa hizi alama ambazo zinaongoza.

Jambo la kusikitisha Mhe. Spika, unaweza ukapita barabarani wakati mwengine ukakuta ile *post* ambayo imewekwa barabarani mfugaji ndio amekwenda kuifanya yeye ndio kisiki cha kufungia ng'ombe, kwa maana kwamba kakosa pahali pa kufungia ng'ombe wake anachukua *post* ile inayoelekeza alama za barabarani yeye ndiyo anayofungia ng'ombe wake.

Jambo hili niombe Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuendelee kuihimiza jamii yetu namna ya kuhifadhi na kutunza sheria pamoja na miundombinu ya barabara.

Mhe. Spika, suala jengine limezungumzwa suala la barabara zetu kongwe. Katika utekelezaji wa mradi kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yanakuwa yanaathirika hasa maeneo ambayo yanakuwa yamepakana na maeneo ambayo tunachukua kifusi, au yanakuwa ni maeneo jirani na maeneo ambayo miradi hii inatekelezwa.

Kwa kweli tunalazimika sisi kama serikali na kama wizara sasa tuliangalie kwa mapana jambo hili, maana inaweza ikawa mmejenga barabara kilomita 20, mkitafakari vizuri mnaweza mkakuta kilomita tano za barabara ambayo ilikuwa ipo ikawa imeharibika.

Mhe. Spika, hili naomba sisi kama wizara tutakaa tuone namna gani ili kuweza kufidia hilo. Lakini msingi mkubwa ni namna ya kuweza kusimamia yale magari makubwa ambayo hayawezi kuakisi uimara au uwezo wa ile barabara husika lazima tusimamie.

Haitokuwa jambo la busara kuona barabara ina uwezo wa kubeba tani kumi tukaliruhusu gari ambalo litakuwa limebeba mzigo wa zaidi ya tani kumi na tano kuweza kupita katika barabara hiyo, itakuwa tumechangia katika uvunjaji na uharibifu wa barabara hiyo. Sisi kama Wizara jambo hilo tunalichukua na tutaona namna gani ya kulifanyia kazi.

Suala jengine Mhe. Spika, limezungumziwa suala la machimbo ya vifusi. Ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo kwa hapa Unguja; Bumbwini, Matemwe, Kibele, Chukwani, Michamvi, Bwejuu, Paje, Jambiani ni maeneo ambayo tumekuwa tuna kawaida kuchukua kifusi. Lakini maeneo hayo ni maeneo kama ilivyo ile dhana ya Sheria ya mwaka 1992, kwamba ardhi tunaamini kwamba ni mali ya serikali.

Na maaneo haya sisi tunapoyaona tunachokifuata sisi ni utaratibu wa kuomba katika sehemu husika waweze kutupatia maeneo yale, na kama kuna vipando vya mwananchi ambavyo vimeendelezwa katika maeneo yale, utaratibu wetu sisi ni kumlipa fidia ili tuweze kupata maeneo hayo kwa ajili ya uchukuaji wa kifusi kwenda kukamilisha miradi.

Ni kweli kwamba kuna changamoto ambayo imejitokeza kuona kwamba miradi inakamilika lakini bahati mbaya kwamba maeneo yale huwa hayapo katika hali nzuri kama kwamba imekuwa yametekelezwa baada ya miradi ile kukamilika. Jambo hili tumelipokea na tutaona namna gani sasa tutaendana na

masharti, kama vile ambavyo wenzetu wa barabara za *MCC* sasa hivi wameweza kutuonesha mfano mzuri kwa namna ya kurejeshea ili mashimo yale yaweze kutumika kwa kazi nyengine zikiwemo za uzalishaji wa mazao na matunda mengine.

Mhe. Spika, limezungumziwa pia suala la matuta. Ninaamini Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho atatoa maelezo mengi mazuri katika eneo hili. Utaratibu wa uwekaji wa matuta upo wazi na tumejitahidi kueleza kwa mara nyingi na imani yetu kwamba kuna haja sasa ya kutafuta namna nyengine ya kuweza kuwasiliana na wenzetu waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Lakini pia na wananchi wetu katika kuona uelewa wa pamoja kwa kiasi gani athari za matuta zinaweza kusababisha majanga mbele ya jamii na kwamba lazima jamii ifahamu, kwamba uwekaji wa matuta ni hatua ya mwisho, hatua ya kwanza kuhakikisha kwamba dereva anafuata taratibu na sheria husika. Dereva anafuata alama ambazo zinawekwa, anafuata maelekezo ambayo atakuwa anapatiwa pamoja na wasimamizi wa barabara zetu. Na pale ambapo tutaona kwamba hakuna namna nyengine ya kuweza kunusuru, basi utafuata uwekaji wa matuta.

Uwekaji huu wa matuta una taratibu zake, kuona kwamba vyombo husika sehemu zile zinazohusiana na masuala ya usafiri barabarani iweze kukaa na bodi, iweze kupitia na kuona kwamba iko haja hiyo na ulazima, vyengine vya *sign* vitawekwa, alama nyengine zimeshawekwa hazikuonesha faida, usimamizi wa wenzetu wa Polisi umeshafanyika haujaonesha tija, ndio tufikie katika hatua ya uwekaji wa matuta.

Ni kweli nimepata maelezo mazuri ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub, hapa kuonesha kilio chake kuona kwamba hatuwathamini wananchi wenzake wa Jimbo la Muyuni labda akilinganisha na wanyama wale wa kimapunju wanawekewa alama.

Lakini mimi inanipa mashaka maana mimi naamini watu wa Muyuni ni watu waelewa ambao ukiwaelekeza jambo wanafahamu na bila shaka watakuwa wanajua taratibu ya matumizi mazuri ya barabara, kama kuna haja ya ulazima kwenda kuweka matuta, basi tumuombe tu Mhe. Jaku niendelee kumkumbusha kwamba tumezungumza karibu mara tatu ndani ya chombo hiki, tufate utaratibu na sisi kama wizara kama kuna haja hiyo hatuoni tabu wala hatuoni shida kwenda kuweka matuta. Lakini msingi ni kuona kwamba tunajiridhisha taratibu ambazo tumejiwekea ziweze kukamilika, uwekaji wa matuta iwe hatua ya mwisho.

Mhe. Spika, pia, zimezungumzwa barabara ambazo hazijakamilika uwekaji wake wa alama, hali mbovu ya barabara kwa mfano barabara ya Mkunazini, barabara ya kuelekea Kisiwandui. Nimuhakikishie Mhe. Jaku kwamba muda si mrefu ataona mabadiliko, tayari tumeshatangaza tenda na tunaamini kama hii barabara ya kwenye mpindo kipindi kisichozidi miezi miwili mitatu itakuwa imepatiwa ufumbuzi.

Yale mengine tutaendclea kuchukua hatua kadri ya upatikanaji wa fedha, uimara wa vifaa vyetu pamoja na nguvu ambazo tutakuwa tumejipangia katika kuona tunakamilisha mipango ya kazi hizo.

Mhe. Spika, pia limeelezwa hapa suala la umiliki wa barabara, naamini Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho atatoa maelezo mazuri namna gani na vigezo ambavyo vitatumika katika upangaji wa madaraja wa barabara hizo. Lakini jambo la msingi naomba nikumbushe Baraza hili kwamba kwa mujibu wa sheria ziliopo, sheria ya Halmashauri pamoja na sheria ya manufaa zimetoa maelekezo barabara zipi ambazo zinamilikiwa na Halmashauri na zipi ambazo zinamilikiwa na sisi.

Kwa kutambua kwamba Halmashauri na Manispaa baadhi ya nyakati zinakuwa na upungufu au ukosefu wa fedha, tunaendelea na utaratibu wetu wa kutoa mchango wa fedha na thamani, kwa kutoa mchango wa vifaa pamoja na wataalamu ili kukamilisha miradi. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache naomba kuendelea kusema kwamba ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninafikiri tukubali kwamba muda tulionao sio mzuri sana kumwita Mhe. Waziri akamaliza hoja hii. Ingewezekana sana kufanya hivyo lakini na pia hata *quorum* tulionayo sio nzuri sana ya kufanya maamuzi. Kwa hivyo, tukubaliane kwamba jambo hili limalizwe kesho. Na baada ya hapa tusitishe ili kumpa Mhe.Waziri muda wa kutosha akajipange kujibu hoja mbali mbali za waheshimiwa wajumbe.

Basi baada ya hayo waheshimiwa wajumbe tusitishe shughuli zetu mpaka kesho siku ya Ijumaa tarehe 13/12/2013 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 12.52 jioni Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 13/12/2013 saa 3.00 za asubuhi)